# Nipashe

Jumatano Julai 10, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579966

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Msaidizi wa Membe anayedaiwa kutekwa Dar ajisalimisha polisi

UKURASA 3


UCHAMBUZI: Mwenge wa Uhuru 2019, hamasa kwa uchaguzi wa serikali za mitaa

Kitaifa

siasa

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Magufuli, Kenyatta wawe mfano kuimarisha EAC

BAADA YA MIAKA 55

Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-4

Ukanda huru wa biashara Barani Afrika wazinduliwa

UKURASA 13

# SIMANZI

• **Zatolewa** kauli nzito kutoneshwa tasnia ya habari... *Endelea ukurasa 2*





Magari yaliyobeba miili ya waliokuwa wafanyakazi watano wa Azam Media, yakiwasili katika ofisi za kampuni hiyo, Tabata, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuagwa. **Picha ndogo:** Majeneza yenye miili hiyo, huku baadhi ya waombolezaji, ndugu jamaa na marafiki wakilia. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Polisi matatani tuhuma rushwa mil. 30/-

UKURASA 2

## JPM awanyooshea kidole Wabunge ujangili hifadhini

UKURASA 2

**MICHEZO** **GADIEL YAMETIMIA SIMBA SC** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Simanzi kuagwa miili wanahabari Azam Media

**Na Beatrice Moses**

HALI ya huzuni, vilio na simazi ilitawala katika viwanja vya ofisi Kampuni ya Azam Media jijini Dar es Salaam jana, wakati wa ibada ya kuanga miili ya wafanyakazi watano wa kampuni hiyo waliokufa kwa ajali juzi mkoani Singida.

Magari matano yaliyobeba miili yanayowasili katika viwanja hivyo vilivyo Tabata TIOT barabara ya Mandela.

Wakati majeneza yanashushwa kwa mpangilio wa aina yake, ndugu jamaa na marafiki kadhaa waliokuwapo waliangua vilio kwa uchungu.

Wafanyakazi waliokufa katika ajali iliyohusisha gari aina ya Toyota Coaster waliyokuwa wamepanda wakisafiri kikazi kuelekea Chato, mkoani Geita iliyogongana ana na lori.

Waliokufa ni Salim Mhando, Charles Wandwi Florence Ndibalema, Sylvanus Kasongo na Said Haji.

Wafanyakazi hao watano ni miongoni mwa watu saba waliofariki katika ajali hiyo.

Vifo hivyo vimetajwa kutonesha mioyo ya wanatasnia ya habari, wengi walia kuwa umekuwa ni mwaka mgumu kutokana na vifo kadhaa vya wanatasnia wakiwamo nguli vilivyotokea tangu mwaka huu uanze.

Baadhi ya wanatasnia waliofariki dunia mwaka huu ni pamoja na Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Regnald Mengi, Mkurugenzi wa vipindi wa Clouds Media Group, Ruge Mutahaba, Mwandishi wa Radio One na ITV ambaye pia alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Arusha Press Club, Charles Ngereza Mwandishi wa Mwananchi Shaaban Ndyamkama.

**JOYCE MHAVILE**

Akizungumza kwa niaba ya vyombo binafsi vya habari nchini, Joyce Mhavile, Mkurugenzi Mtendaji wa ITV na Redio One, alisema vifo hivyo vimeufanya mwaka huu uendelee kuwa mgumu kwa waandishi wa habari.

"Msiba huu umetupiga kwenye tasnia ya habari mwaka huu umekuwa mgumu sana, lakini nawasihi ninyi ambao mmebaki wafanyakazi wa Azam mhakikishe mnafanya kwa bidii kuziba pengo," alisema Muhavile.

**HUMPHREY POLEPOLE**

Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM, Humphrey Polepole, alisema tasnia ya habari huu ni msiba mwingine mkubwa kwa mwaka huu.

Alisema kuwa ni jambo linaloumiza kuwa vijana walikuwa wadogo, wamesoma wameelimika walianza kulitumikia taifa wamepata msiba wakiwa kazini.

Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, alisema anakubaliana na wengine kwamba mwaka huu tasnia ya habari imepata mishtuko mikubwa mingi mizito.

"Ni ushuhuda ulio wazi kuwa tasnia ya habari inapoguswa nchi nzima inatikisika ni ushuhuda tu wa umuhimu wa vyombo vya habari katika nchi yetu, ni ushuhuda jinsi ambavyo vyombo vya habari vinapewa uzito katika taifa namna ambavyo vyombo vya habari vinawajibu wa kipekee katika kulijenga ama kulibomoa taifa," alisema Mbowe.

Mbowe ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chadema alibainisha kuwa: "Taifa letu tunaopenda tunastahili kupendana zaidi, vyombo vya habari ni kiunganishi kizuri sana katika kujenga umoja na mshikamano na upendo katika taifa letu,lakini tukiruhusu vyombo vya habari vitumike kutugawa tutagombana,tutalaumiana tutauma mapendo na mshikamano wetu." alisema.

Aliwasihi viongozi wote wenye mamlaka ya kusimamia vyombo vya habari kuhakikisha wanasimamia vifanye kazi kwa weledi visitumike vibaya, hatua ambayo

INAENDELEA UK. 8



Rais John Magufuli akiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, wakivuta utepe kuashiria uzinduzi wa Hifadhi yaTaifa ya Burigi, ilioyopo Chato, mkoani Geita jana. Wanaoshuhudia ni viongozi mbalimbali wa serikali na chama tawala. **PICHA: IKULU**

# JPM awaonya wabunge uvamizi maeneo hifadhi

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli, amewaonya wabunge wanaoogopa kuwaeleza ukweli wananchi wanaovamia maeneo ya hifadhi za taifa, mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo ya hifadhi yanayomilikiwa na jamii (WMA) kwa kuogopa kunyimwa kura.

Amesema wananchi wamekuwa na tabia za kuvamia maeneo hayo huku wabunge wa maeneo yao wakiogopa kuwaambia ukweli kwa kuhofia kunyimwa kura wakati wa uchaguzi.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana wakati wa hafla uzinduzi wa hifadhi mpya ya Burigi, katika Kijiji cha Mkolani, wilayani Chato, mkoani Geita. Alisema wananchi wanapaswa kulinda hifadhi na maeneo ya mapori ya akiba na tengefu na kuacha kusogelea maeneo ya hifadhi kwa sababu watasababisha maeneo hayo kupotea kutokana na shughuli za binadamu na mifugo.

"Wabunge wamekuwa wakisogelea maeneo ya hifadhi. Na sisi wabunge kwa sababu ya kutaka kura kila siku wanasema wananchi wangu, wananchi wangu 'tusicompromise' (tusijadili) siasa na maendeleo ya Watanzania, tunapotea, waambieni ukweli ili mwananchi akikunyima kura akunyime, lakini hifadhi iendelee kuwapo na taifa lineemeke," alisema Rais Magufuli.

"Hizi siasa za kudanganyana ili tupate kura ni mbaya ndugu zangu wabunge, mimi ni mwanasiasa vile vile, lakini kule Tuangoma niliwaambia ukweli, Kasenga niliwaambia ukweli ifike mahali tuseme ukweli na ukweli utasimama kuwa ukweli."

Alisema serikali iliunda tume ya kuchunguza maeneo ya Hifadhi ya Burigi yaliyovamiwa ripoti ambayo imewasilishwa, hivyo kwa maeneo ambayo yaliyovamiwa yatafanyiwa marekebisho.

Alisema marekebisho hayo ya kuweka mipaka hiyo yatakuwa ya mwisho kwa sababu wakiendelea kuruhusu uvamizi na kufanya marekebisho hifadhi hiyo na nyingine zitapotea.

"Ndugu zangu wa maeneo yote niliyoeleza tuache tabia ya kuyavamia maeneo haya kwa sababu tusipoacha tutayapoteza yote," alisema Rais Magufuli.

Aliwaagiza viongozi wa mikoa ya Kagera na Geita wasimamie maeneo yote ambayo yatawekwa alama ili kusiwapo na watu wanaoendelea kusogea eneo hilo la hifadhi.

Kadhalika aliwakemea viongozi wa vijiji vinavyozunguka maeneo yote ya utalii wenye tabia za kuchukua fedha kutoka kwa wafugaji na kuwaingiza katika maeneo hayo

INAENDELEA UK. 8

## Polisi matatani kwa tuhuma za rushwa ya mil. 30/-

**Na Ibrahim Yassin,** MBOZI

ASKARI polisi wawili wanashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni 30.

Takukuru imewataja askari hao kuwa ni Justin Madauda namba G1466 na Anthony namba H2433 wa mkoani Songwe, ambao wanadaiwa kudai kiasi hicho cha fedha kutoka kwa mtu anayedaiwa kumiliki silaha bila kuwa na kibali.

Kamanda wa Takukuru mkoani Songwe, Damas Suta, amesema askari hao ambao mmoja ni wa kituo cha Tunduma wilayani Momba mkoani Songwe na mwingine ni wa kituo cha polisi Mahenge mkoani Morogoro, ambao walimkamata mwananchi mmoja anayedhaniwa kumiliki silaha kinyume cha sheria, huku wakimuomba rushwa ili wasimkamate.

Kwa mujibu wa kamanda huyo wa Takukuru, wanatarajia kufikishwa mahakamani baada ya taratibu kikamilika.

Kamanda Sutta, amewapongeza wananchi kwa kuonesha ushirikiano wao mzuri kwa maofisa wa taasisi hiyo na kuwataka waendelee kufanya hivyo pindi watakapohitajika, na watakapoona kuna viashiria vya rushwa mahala popote.

Katika hatua nyingine, Kamanda Sutta, amesema halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na Ileje ni miongoni mwa halmashauri ambazo viongozi ama watendaji wake baadhi yao wanaongoza kwa kupokea rushwa.

Pia amewataka watumishi hao kufanya kazi kwa kufuata misingi ya utawala bora na kwamba Halmashauri ya Mbozi pekee Takukuru imeokoa kiasi cha Sh. 51,814,100.

## HABARI KITAIFA

# DC: Tunafanyia kazi madai viongozi Chadema kutekwa

**Na Enock Charles**

MKUU wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Miraj Mtaturu, amesema kuwa ofisi yake imeyasikia madai ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kuhusu viongozi wao kutekwa na kwamba inayafanyia kazi, lakini amekanusha kuhusika kuwasaidia vijana wa ulinzi wa Chama Cha Mapinduzi (green guard) kufanikisha utekwaji wa viongozi hao.

Akizungumza na gazeti hili kwa simu jana, Mkuu huyo wa Wilaya alibainisha kuwa ofisi yake imeyasikia madai hayo ya Chadema na kuwa inayafuatilia kupitia kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili kubaini ukweli wake.

"Kuhusu green guard labda ungemuuliza katibu wa Chama Cha Mapinduzi kwa sababu mimi nafanya kazi yangu kama mkuu wa wilaya na hayo...masuala tumeyasikia na tunachukua hatua ungempata RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa) angekwambia hatua zilizochukuliwa," Mtaturu alisema.

Gazeti hili lilipomtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Switbeth Ngiwike kuhusiana na madai ya Chadema ambaye aliahidi tangu juzi kuwa angelitolea ufafanuzi suala hilo, lakini alisema kwa sasa anashughulikia msiba uliotokana na ajali ya gari ya barabarani mkoani humo lililopelekea vifo vya wafanyakazi watano wa Azam Media.

INAENDELEA UK. 26

# Msaidizi wa Membe ajisalimisha polisi Dar

**Na Romana Mallya**

ALLAN Kiluvya, msaidizi wa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, anayedaiwa kutekwa na watu wasiojulikana siku tatu zilizopita, hatimaye amepatikana.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, Musa Taibu, ameiambia Nipashe jana kuwa, Allan alikwenda polisi juzi usiku na kuwaeleza kuwa alikuwa ametekwa na watu wasiojulikana na kumuachia huru.

"Allan aliyetekwa amepatikana, alikuja mwenyewe polisi jana (juzi) usiku na akasema kuwa alitekwa na watu ambao mpaka wakati huo hajawafahamu kwa sababu wakati wakimchukua walimfunga kitambaa usoni na hata huko alipopelekwa hakujui," alisema.

Kamanda Taibu alisema ingawa bado hajaonana uso kwa uso na Allan, ameambiwa kuwa alipofika kituoni alieleza kuwa amekwenda hapo kutoa taarifa kuwa amepatikana.

"Sijaongea naye kwa sababu leo tangu asubuhi sipo ofisini. Nimeambiwa kuwa Allan amesema aliwekwa katika mazingira ambayo hakuyapenda, sababu za kutekwa hajui, hakuna manyanyaso waliyompatia. Jeshi la Polisi litamuhoji Allan kujua zaidi baada ya kutekwa, hao watekaji walimwambia nini, lengo lao lilikuwa ni lipi? Tunamtaka achukue tahadhari kwa sasa, wakati tukipanga kumuhoji zaidi kuhusu tukio hilo," alisema.

Awali, mjomba wa kijana huyo, Samwel Ng'andu, akizungumza na waandishi wa habari alisema jaribio la kutekwa Allan lilianzia baa ya Rose Garden iliyopo Mikocheni jijini Dar es Salaam.

"Jaribio la kutekwa lilianzia Rose Garden, idadi ya watekaji ilikuwa ni watu wanne walikuwa wakitumia gari aina ya Land Cruiser T810 BQS, rangi ya kijivu na lilikuwa na gurudumu nyuma lililofunikwa kwa kava lenye rangi ya chungwa," alisema.

Aliongeza: "Baada ya tukio hilo kushindikana kijana wetu aliendelea kufanya mizunguko kwa uangalifu hadi siku alipotekwa na gari lile lile la Land Cruiser," alisema.

Jumatatu, Kamanda Taibu aliwaomba mwananchi wenye taarifa mahali alipo, wawasiliane na Jeshi la Polisi kwa sababu hadi siku hiyo walikuwa hawajampata.

"Taarifa tayari tumezipata tunaendelea kuzifanyia kazi, lakini tunaomba hata wewe mwandishi kama una taarifa au fununu wapi alipo utusaidie, kama kuna mwananchi ana taarifa alipo wawasiliane nasi. Lengo ni ili apatikane," alisema.

Jumapili, kulizagaa taarifa mitandaoni ikidai Allan alitekwa na watu wasiojulikana maeneo ya Mbezi Jogoo, jijini Dar es Salaam nje ya nyumba ya rafiki wake.

Katika maelezo yake, Magreth aliyojirekodi kuhusiana na tukio hilo la utekaji alidai kuwa, siku ya tukio walikuwa hoteli ya Mbezi Africana yeye, dada yake Agnes pamoja na Allan na baada ya kunywa, kijana huyo aliwapeleka nyumbani kwao Jogoo.

"Nilikuwa mimi, Allan na dada yangu mwingine anaitwa Agnes, tulikuwa hoteli ya Juliana kule Africana, baada ya kunywa ulifika muda wa kwenda nyumbani, Allan akasema atatupeleka, siyo mbali na hapo Juliana, ni Jogoo kituo kinachofuata. Alitupeleka hadi nyumbani, nikashuka na kufungua geti akaingiza gari akashuka Allan na dada yangu," alisema.

INAENDELEA UK. 8




# TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

**CHUO CHA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVUKAZI (ATTI) – MBEYA**

## TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI KWA WAHANDISI, MAFUNDI SANIFU NA MAKANDARASI WA BARABARA

**1. Utangulizi:**

Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi "Appropriate Technology Training Institute" (ATTI-MBEYA) ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe na Lami, pamoja na kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi. Kozi hizi zimepangwa kufanyika kwa nyakati tofauti kama ifuatavyo: -

| Na. | JINA LA KOZI | MUDA NA TAREHE | MAFUNZO YATAFANYIKA |
|---|---|---|---|
| 1. | Kozi maalumu ya vikundi vya wanwake na vijana ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | **Wiki Tatu (3)**<br>12/08/2019 - 30/08/2019 | ATTI – Mbeya |
| 2. | Kozi ya ujenzi wa Lami ("Bituminous Surfacing for Low Volume Roads"), kwenye barabara za mijini na vijijini kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Nne (4)**<br>02/09/2019 - 27/09 /2019 | ATTI- Mbeya |
| 3. | Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Kumi (10)**<br>07/10/2019 - 13/12/2019 | ATTI- Mbeya |

**2. Malengo ya Kozi na Masomo Yatakayofundishwa: -**

(a) **Kozi Maalumu Ya Vikundi Vya Wanawake Na Vijana**: Masomo yanayofundishwa kwa kozi hii ni masomo ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na masomo shirikishi ambayo ni utaratibu wa kufungua kampuni na vikundi, utaratibu wa kujaza kitabu cha tenda, zege na 'masonry'. Masomo haya yamelenga kumwezesha mshiriki kuweza kufanya kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida (routine/recurent maintenance).

(b) **Kozi ya Mafunzo ya Barabara za Lami:** Masomo yatakayofundishwa ni aina mbalimbali za lami, aina mbalimbali za barabara za lami, aina mbalimbali za viunzi (materials) kwa barabara za lami, kuunda na kutengeneza tabaka la lami (Design of Surface Dressing), kuziba viraka (Pothole Repair in Surface Treatment Pavement), kuziba mipasuko (crack sealing), aina ya Vifaa na mitambo kwa kazi za lami, Usalama kazini, mafunzo haya pia yatahusu mafunzo ya kujenga barabara ya lami kivitendo. Masomo haya yatamwezesha mshiriki kuweza kufanya kazi za lami, kusanifu na kuunda barabara ya lami "Design of surface dressing".

(c) **Kozi ya Mafunzo ya Barabara za Changarawe:** Masomo yatakayofundishwa kwa kozi hii ni ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi, mpango wa kazi (Planning), Uongozi sehemu za kazi na mbinu za usimamiaji wa kazi, vipimo vya kazi, usimamiaji wa mikataba, Uwekaji wa changarawe, ujenzi wa makalavati pamoja na mafunzo ya kujenga barabara kivitendo. Mafunzo haya yatamwezesha mshiriki kuweza kufanya kazi za ukarabati na matengenezo ya barabara kwa ubora unaotakiwa. Kwa wajasiriamali masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi "**SPECIALIST LABOUR BASED CONTRACTORS"** daraja la tatu na kuweza kusajiliwa na bodi ya usajili wa makandarasi (CRB).

**3. Walengwa wa Mafunzo haya ni:-**

a) Wahandisi wa barabara toka TANROADS, TARURA na Wakandarasi,
b) Mafundi Sanifu wa Barabara toka TANROADS, TARURA na Wakandarasi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi nchini,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga uwezo wa kazi zao za matengenezo ya barabara kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu wa kazi za barabara na wanaotaka kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**4. Gharama za Mafunzo:-**

Gharama ya mafunzo ni **Tshs. 500,000/=** Kozi Maalumu ya Vikundi vya Wanawake na Vijana T**shs. 1,000,000/=** kozi ya Lami na **Tshs. 1,600,000/=** Kozi ya Changarawe. **Malipo ya ADA ya ushiriki yalipwe kabla ya kozi kuanza kwa: "Principal ATTI, NBC Tukuyu, A/c No.038101001741"**, tunashauri yalipwe kabla ya wiki mbili na wasilisha hati ya malipo (Bank Slip) unapowasili kwenye kituo cha kozi husika.

**5. Namna ya Kutuma Maombi ya Kozi hizi:-**

Wale wote watakaokuwa tayari kutaka kujiunga na kozi hii wanaombwa kutuma maombi yao Chuoni ATTI – MBEYA kwa kutumia anuani ya Chuo hapa chini na kupitia E-mail na simu zilizoonyeshwa, ili tuweze kuwaingiza kwenye orodha ya washiriki. Kwa kozi hizi kuna nafasi ishirini (20) tu kwa kila kozi; hivyo, wahi mapema kutuma maombi yako.

**Mkuu wa Chuo,**
**ATTI – Mbeya,**
**S.L.P 1957, MBEYA,**
**Tel: +255 732 951 524/717**
**Mob: +255 655 274 280, +255 764 775 354, +255 765 251, 509.**
**Fax: +255 732 950 399**
**E-mail: attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com, sangoatti@yahoo.com, frankkisandu@gmail.com**

215316402

---

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001/2015 Certified

MAKAO MAKUU
Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni Taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea iliyoundwa na Sheria ya EWURA Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA inawajibu wa kuzidhibiti sekta hizi kiufundi na kiuchumi. Mamlaka ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida ya halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/No | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ATN Petroleum Co.Ltd-NALA-Dodoma S.L.P 683, Dodoma | Kiwanja No. 45, Kitalu 'H', Eneo la Nala, Wilaya ya Dodoma, Mkoa wa Dodoma | Abdulatif Twaribu Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 2. | Hope Service Station, S.L.P 839, Iringa | Kiwanja No. 19, 20 & 21, Kitalu 'K', Eneo la Gangilonga, Wilaya ya Iringa, Mkoa wa Iringa | Mohammed Mansour Huwel (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 3. | King J petrol station S.L.P 406 Lindi | Kiwanja Na. 402, Kitalu 'PP', Eneo la Likotwa, Lindi Mjini, Mkoa wa Lindi | Ahmed Raphael Bongi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 4. | Darpco energy co. ltd – Mbagala, Charambe S.L.P 3892 Dar es salaam | Kiwanja Na. 597, Kitalu 'DD', Eneo la Majimatitu, Charambe,Wilaya ya Temeke, Dar es salaam | Thabit George Mkasi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 5. | Augustino A. Ngowi-Ester Filling Station Msumi S.L.P 67315 Dar es salaam | Kiwanja Na. 1199, Kitalu 'K', Eneo la Mbezi Louis, Wilaya ya Kinondoni, Dar es salaam | Augustino A. Ngowi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 6. | Top Oil Petrol Station – Gongo la Mboto S.L.P 42445 Dar es salaam | Kiwanja Na. 2193, Kitalu 'E', Eneo la Gongo la Mboto, Wilaya ya Ilala, Dar es salaam | Mbarak S. Bawazir (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 7. | Penna Pura Oil Tanzania Limited S.L.P 72838 Dar es salaam | Eneo la Tabata, Wilaya ya Ilala, Dar es salaam | Salim Janmohamed (Raia wa Uingereza) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi |
| 8. | Shiloh Trading Co.Ltd S.L.P 36151 Dar es salaam | Kiwanja Na. 85, Kitalu 'A', Eneo la Mjimwama, Wilaya ya Kigamboni, Dar es salaam | Justus Rwegoshora (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Vilainishi |
| 9. | Peace Traders S.L.P 10657 Dar es salaam | Kiwanja Na. 858, Eneo la Upanga Mashariki, Wilaya ya Ilala, Dar es salaam | Saleh Bader (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi |
| 10. | Uheche Service Station S.L.P 397 Masasi | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Eneo la Mtapika, Wilaya ya Masasi, Mkoa wa Mtwara | Ahmed Uheche (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 11. | Kilimanjaro Cables S.L.P 2562 Dar es salaam | Kiwanja Na. 161/1, Kilwa Road, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es salaam | Tahir Chunawalla (Raia wa India) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi |
| 12. | Mount Meru Retailer Company Ltd S.L.P Dar es salaam | Kiwanja Na. 13, Eneo la Gerezani, Wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar es salaam | Atul Movaliya (Raia wa India) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapo juu.

**IMETOLEWA NA**
**MKURUGENZI MKUU**

XXXXXX

## HABARI KITAIFA

# AfDB kuipandisha Tanzania daraja

**Na Mwandishi Maalum**

BENKI ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), inatarajia kuipandisha daraja Tanzania kutoka katika hadhi ya kunufaika na Mfuko wa Maendeleo wa Benki (ADF) hadi kuwa na hadhi itakayoiwezesha Tanzania kupata rasilimali fedha zaidi kupitia dirisha la benki hiyo.

Endapo Tanzania itafanikiwa kupandishwa hadhi, nchi itaweza kunufaika na ongezeko la fedha kutoka AfDB kutoka Dola za Marekani milioni 350 kwa mwaka hadi Dola za Marekani milioni 812 kwa mwaka.

Hayo yamesemwa jijini Dodoma na Mwakilishi Mkazi wa Benki hiyo, Dk. Alex Mubiru, alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango.

Dk. Alex alieleza kuwa hatua hiyo ya kupandishwa hadhi ama kupandishwa daraja inatokana na uchumi wa nchi kufanya vizuri hususani katika maeneo ya kasi ya ukuaji wa uchumi na kuwa na deni himilivu.

"Hatua hiyo itaiwezesha Tanzania kupata fedha zaidi kutoka katika Benki hiyo na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na vipaumble kwa Serikali," alisisitiza Mubiru.

Mubiru, alisema kuwa benki hiyo inajivunia kufanya kazi na Tanzania ambayo ni miongoni mwa nchi waasisi wa Benki hiyo.

Kwa upande wake, Dk. Mpango alieleza kuwa Serikali inajivunia kufanya kazi pamoja na Benki ya AfDB kwa kuwa benki hiyo imekuwa na masharti rafiki katika upatikanaji wa mikopo.

Dk. Mpango alisema kuwa Benki hiyo ina mtazamo chanya katika maendeleo ya watu na kuwa dira katika mipango ya maendeleo na kuahidi kushirikiana nao vyema katika kukuza uchumi wa nchi.

Aidha, Waziri Mpango aliipongeza benki hiyo kwa kukubali kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara ya mzunguko Dodoma (km110.2) kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Dodoma (Msalato) na kubainisha kuwa uamuzi huo ni mzuri kwani licha ya Dodoma kuwa ni Makao Makuu ya nchi, lakini pia miundombinu hii itaunganisha na kuchochea ukuaji wa uchumi na biashara katika mikoa mingi nchini pamoja na nchi jirani.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akibadilishana mawazo na Rais Emmason Mnangagwa wa Zimbabwe, walipokuta katika chakula cha jioni kilichoandaliwa na Rais Mahamadou Issoufour wa Niger, kwenye mkutano wa 12 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU), uliojadili kuhusu Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) mjini Niamey, Niger, juzi. **PICHA: OMR**

# Ufaransa yataja maeneo 9 ya ushirikiano na Tz

**Na Salome Kitomari**

UBALOZI wa Ufaransa nchini Julai 14, mwaka huu, utasherehekea siku ya kitaifa, huku ukieleza maeneo tisa ya ushirikiano baina yake na Tanzania ikiwamo kuunga mkono jitihada za serikali kwenye mapinduzi ya uchumi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika ofisi za Ubalozi huo jijini Dar es Salaam, Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alisema siku hiyo inafahamika kama Bastille ikiwa ni kukumbuka Mapinduzi ya Ufaransa mwaka 1789.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni haki za binadamu, kisiasa, uwekezaji na biashara, elimu, nishati, maji, kilimo, utalii na afya, ambayo nchi hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa kuleta maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Balozi Clavier alisema Ufaransa inaunga mkono jitihada za Rais John Magufuli kuifanya nchi kuwa ya uchumi wa kati ifikapo 2025, na kwamba Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), litafadhili na kutoa kipaumbele kwa miradi ya maendeleo kwenye sekta za kipaumbele za nishati, usafiri na maji.

"Lengo letu ni kuhakikisha huduma muhimu na miundombinu kwa jamii katika maendeleo ya kiuchumi, tumeongeza zaidi ya mara mbili msaada wetu kwa Tanzania ambao umefikia mkopo wa Dola za Marekani milioni 110 kwa mwaka na Dola milioni 23 za msaada," alibainisha.

Kwa mujibu wa balozi huyo, mafanikio hayo yamedumu kwa miezi 12 na kwamba Septemba mwaka jana rais alizindua mradi wa maji wa Musoma uliogharimu Dola za Marekani milioni 27 ikiwa ni fedha kutoka AFD.

Pia alisema Bodi ya AFD imepitisha mkopo wa Euro milioni 100 kwa mradi wa umeme kati ya Zambia na Tanzania na kuongeza umeme kwenye gridi ya taifa.

Vile vile, alisema kuwa eneo la afya, nchi hiyo imetoa mkopo wa Dola za Marekani milioni 53 kwa ajili ya upanuzi wa hospitali ya Aga Khan kwa kuongeza vitanda 170 na vituo 27 nchini.

Kadhalika kwenye eneo la kilimo nchi hiyo itaendelea kusaidia miradi ya kijamii katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kupunguza umaskini na kwamba Dola milioni moja zimetolewa kwa wakulima wadogo 6,000 mkoani Mtwara.

"Biashara kati ya Tanzania na Ufaransa imeongezeka kwa asilimia 30 mwaka 2018 kwa thamani ya Dola za Marekani milioni 200. Umoja wa wafanyabiashara wa nchi hizi watakutana mwezi ujao katika mkutano utakaoleta pamoja kampuni 40 za Ufaransa zinazofanyakazi nchini," alisema na kuongeza:

"Ujumbe wa wafanyabiashara kutoka Tanzania uko katika maandalizi ya mwisho kwenda Ufaransa ikiwa ni matokeo ya ujio wa ujumbe wa wafanyabiashara 35 kutoka nchini humo waliotembelea mwaka jana kuangalia uwekezaji wa uwekezaji."

Kwa upande wa elimu, alisema kuna shule ya misngi iliyojengwa na kwa elimu ya juu wameendelea kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (Muhas), ikiwa ni pamoja na kutoa ufadhili kwa wanafunzi kusoma nchini humo.


## LAS VEGAS CASINO

## EMPLOYMENT OPPORTUNIES

1 EXPERIENCED-DEALERS
2 TRAINEE DEALER
3 CASHIERS
4 ATTENDANTS
5 WAITRESSES
6 BAR SUPERVISOR
7 SECURITY

We are looking for suitable Applicants to fill the above positions. Applicant should indicate the position interested.

**Qualifications:** Applicants should be educated of not less than Form IV and above, with good knowledge of English and Mathematical calculations.

**Minimum age 20 years old.**

***Attractive salaries and benefits await those to be selected.***

***All suitable applicants will be contacted for a formal interview.***

**General Requirements:**

**Application should be accompanied by:**

- Detailed C.V.
- Copies of relevant certificates: Academic and Work related (if any)
- 2 passport size coloured photographs
- 2 names of referees and their tel. numbers
- Applicant's Day-time telephone number.

Letter of Application should be addressed to Casino Manager and handed to reception desk from 9:am to 4:pm, at Las Vegas Casino, Ali Hassan Mwinyi Road, Upanga, not later than **30/07/2019.**

115311602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hifadhi ya Burigi fursa mpya

**JANA** Rais John Magufuli alizindua hifadhi ya Taifa ya Burigi-Chato yenye ukubwa wa kilomita za mrada 4,702 na kufanya Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) kusimamia hifadhi 19.

Hifadhi ya Burigi-Chato imezaliwa ikiwa ni muunganiko wa mapori ya akiba ya Burigi na Biharamulo, katika kipindi ambacho Tanapa inatimiza miaka 60 tangu kuanzishwa kwake.

Aidha, ni katika kipindi ambacho sekta ya utalii inaongoza kuliingizia taifa fedha za kigeni kwa asilimia 25, inachangia pato la taifa kwa asilimia 17.6, kutoa ajira za moja kwa moja zaidi ya 600,000 na ajira zisizo za moja kwa moja milioni 2.

Ongezeko la hifadhi za taifa unakuja wakati ambao Tanapa imebadilika kimuundo na kimfumo na kuwa jeshi la hifadhi na misitu yaani Jeshi Usu lililozinduliwa mwaka jana, ambalo litatumia mbinu za kijeshi kulinda rasilimali ya wanyamapori na misitu.

Vile vile, hifadhi hiyo imezinduliwa katika wakati ambao Tanapa iko katika mpango wa kufungua utalii ukanda wa kusini kwa gharama za Dola za Marekani milioni 150, huku hifadhi zitakazopewa kipaumbele kwenye maboresho mbalimbali ni Hifadhi za taifa za Ruaha, Udzungwa, Mikumi na Pori la Akiba la Selous.

Kuongezeka kwa hifadhi hiyo kanda ya Ziwa ni habari njema la ongezeko la idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kutembelea hifadhi nyingi kwa wakati mmoja tofauti na awali baada ya kutembelea Hifadhi ya Kisiwa cha Saanane walilazimika kwenda ukanda wa kusini au kaskazini. Ongezeko la maeneo yaliyohifadhiwa nchini kunafanya Tanzania kuendelea kung'ara na kujulikana ulimwenguni kwa kuwa na vivutio vingi na vizuri na sasa idadi ya watalii itaongezeka.

Aidha, kutaongeza ukuaji wa pato la taifa na wananchi kwa ujumla ambao kwa walio jirani na hifadhi za taifa watanufaika na mpango wa ujirani mwema, ambao hutekeleza miradi inayoibuliwa na wananchi wa maeneo husika na kuunda vikundi vya kuwawezesha kuondokana na umaskini.

Lengo hasa ni kuwashirikisha wananchi kuwa walinzi wa rasilimali hiyo muhimu kwa maendeleo ya nchi, ikiwamo kutoa taarifa za majangili na hujuma nyinginezo.

Watanzania watanufaika na mgawo wa keki ya taifa kwa kuwa sehemu ya fedha inayopatikana itaelekezwa kwenye huduma za maendeleo, jambo linaloonyesha ni muhimu sana kwa umoja wetu tukalinda vivutio hivi ili viwe endelevu kwa vizazi cha sasa na vijavyo.

Pia, kuongezeka kwa watalii wanaotembelea hifadhi za kanda ya ziwa kutaongeza ajira za moja kwa moja na ajira zisizo rasmi, ikiwamo wananchi kuuza bidhaa kwa watalii na hoteli za kitalii zitakazojengwa.

Faida nyingine ya hifadhi hiyo ni kuongezeka kwa mzinguko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji zitakazofanyika eneo hilo kwa maana ya hoteli na huduma za kitalii, ikiwamo wananchi kuuza bidhaa na huduma mbalimbali kwa watalii.

Wito wetu ni kwa wananchi kutambua sasa Hifadhi ya Taifa ya Burigi-Chato itakuwa chini ya Tanapa ambayo kwa mujibu wa sheria namba 5 ya wanyamapori, hairuhusiwi kufanya shughuli zozote za kibinadamu na iwapo watafanya hivyo hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

Kadhalika, wananchi wanatakiwa kuwa mabalozi wazuri wa Tanapa kwa kuhakikisha hawashirikiani na majangili au wahujumu wa namna yoyote, bali kulinda rasilimali hiyo.

Kwa mamlaka za usimamizi wa hifadhi zinapaswa kulinda na kuishi maadili ya kazi zao kwa kuhakikisha hawahusiki kwa namna yoyote kwenye hujuma ya rasilimali za wanyama na misitu hasa wanyama waliohatarini kupotea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanasiasa mmesikia somo la Prof. Ibrahim Lipumba?

Na Sabato Kasika

**HIVI** karibuni Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi CUF, Profesa Ibrahim Lipumba alisema utafiti unaonyesha Tanzania ni ya nne kutoka chini kati ya nchi 153 zenye furaha duniani.

Mwanasiasa huyo anazitaja nchi nyingine za chini kuwa Jamhuri ya Afrika ya Kati, Sudani Kusini na Afighanistan kwamba zina changamoto hiyo, kwa sababu zina vita.

Prof. Lipumba ambaye ni mtaalam wa mambo ya uchumi, anafafanua kuwa Tanzania ambayo ina amani, na utulivu, lakini watu hawana furaha, wengine hata wakitekenywa hawacheki.

Anasema kutokana na hali hiyo, CUF inakuja na sera ambayo imejikita katika masuala ya afya, elimu, ajira, miundombinu na Tehama ikigusia maisha halisi ya Mtanzania.

Kwa mujibu wa Prof. Lipumba sera hiyo inalenga kuhakikisha wajawazito wanapata lishe bora, kujifungua salama, elimu bora ya kusaidia watoto kuwa na ujuzi wa kutosha.

"Vilevile mazingira ya sekta binafsi kutoa ajira kwa wingi, ujenzi wa miundombinu, pensheni kwa wazee na matumizi ya Tehama katika kuwezesha vijana kuendelea kujifunza," anasema Prof. Lipumba.

Anasema, CUF inaamini kuwekeza katika afya ya mama na mtoto kuna thamani kubwa kwa taifa na kunasaidia kupata nguvu kazi yenye tija.

Anatoa wito Watanzania kutumia utaalamu na ujuzi walionao ili kujenga nchi ambayo wananchi wake watakuwa na furaha wakati wote.

Pamoja na hayo, kuna mambo ambayo Prof. Lipumba aligusia na ni vyema wanasiasa wakayazingatia ili kusaidia nchi kusonga mbele badala ya kupinga kila jambo hata lile lenye manufaa kwa taifa.

Prof. Lipumba anasema haiwezekani wanasiasa kusimama na kupinga yale mazuri ambayo yameanza kufanyiwa kazi, bali wanapaswa kusisitiza ili yatekelezwe kikamilifu.

Jambo la msingi la kulitambua hapa ni kwamba maendeleo hayana vyama, hivyo kero ambazo wapinzani walikuwa wakilalamikia wanapoona zinatatuliwa, wasisite kuunga mkono bila kujali zimetatuliwa na nani.

Kuitwa mpinzani haina maana kuwa ni kupinga kila kitu, kwani mtindo wa aina hii unaweza kusababisha hata vyama vya upinzani kuchokwa.

Suala la maendeleo siyo la chama fulani, ni la Watanzania wote. Binafsi ninaunga mkono kauli ya Prof. Lipumba kwamba haiwezekani kusimama na kupinga yale mazuri yaliyofanyiwa kazi, ambayo zamani upinzani ulikuwa ukilalamikia.

Prof. Lipumba anashauri wanasiasa kuunga mkono juhudi za serikali kutoa elimu bure ili watoto wengi waende shule, na anashauri kuwekeza kwa walimu ili wawe na ari ya kufundisha, hivyo ninamtakia kila la heri kwa sera hiyo.

Ushauri wa aina hiyo unatia moyo, lakini kupinga tu na tena wakati mwingine kwa lugha isiyofaa, siyo vizuri, hivyo ni vyema kutafakari na kisha kuchukua hatua ili kwenda sambamba na lengo la vyama vya upinzani.

Niwakumbushe wanasiasa kuwa lengo la kuwa na vyama vingi vya siasa (upinzani) ni kuleta ushindani wa kisiasa, ili kuleta maendeleo ya nchi, hivyo upinzani wa kisiasa si uadui.

Vipo baadhi ya vyama vya siasa ambavyo vimekuwa vikichukuliwa kama si vya upinzani, eti kwa sababu tu vinaunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali za kuleta maendeleo.

Lakini wanaofanya hivyo wanasahau kwamba upinzani si uadui na maendeleo hayana chama bali yanahusisha Watanzania wote wa vyama mbalimbali na itikadi tofauti za kidini.

Hivyo, kwa somo alilotoa Prof. Lipumba kwamba upinzani siyo kupinga kila kitu, basi wanasiasa wenye mtazamo wa kupingapinga wajifunze kitu na kuachana na mawazo hayo.

Tanzania ni ya wote wakiwamo wanasiasa, wasio wanasiasa na watu wa dini mbalimbali, hivyo linapokuja suala la maendeleo, halina chama wala dini, bali Watanzania wote wanaungana kwa ajili ya maendeleo ya nchi yao.

Siasa za kupinga kitu zimepitwa na wakati, na zinaweza kuwa siasa za majitaka, ambazo hazipaswi kukumbatiwa na wanasiasa waliokomaa kisiasa.

# BARUA & MJADALA

BARUA YA WAZI KWA MKUU WA MKOA WA MOROGORO

## *Mgogoro wa ardhi Kiegea 'B'*

*KICHWA cha habari hapo juu chahusika. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, rejea mkutano uliofanya na wananchi wa Kiegea 'B' Kata ya Mkundi, mwezi wa pili mwaka 2016.*

*Mkuu wa mkoa ulitoa maelekezo ya kutoendelezwa kwa eneo la Kiegea 'B' kwa makazi mpaka zoezi la uhakiki na upimaji lifanyike.*

*Hata hivyo, mpaka leo baada ya zoezi la uhakiki, zoezi la upimaji halijafanyika.*

*Kwa niaba ya wananchi wa Kiegea 'B' ninakuomba uje utueleze ulikokwama ili tushauriane, ikiwezekana tuweze kumshirikisha hata Waziri wa Ardhi atusaidie.*

*Hiyo ni kwa sababu kwa kuchelewa kwako kuja kutatua mgogoro huu, kunasababisha hata serikali ishindwe kukusanya kodi ya majengo, ardhi na hata kuchelewesha maendeleo ya wananchi kwa ujumla.*

***Wako mwananchi,***
***Augustino Ally, 0682103239***
***Mwananchi Kiegea 'B'***
***S.L.P 166,***
***Morogoro***
***22/06/2019***

## *Maofisa wa Polisi wanahitajika Kwembe*

***Mhariri habari***

*NINAJITOKEZA kueleza kero tunayokumbana nayo sisi wakazi wa Kwembe jijini Dar es Salaam katika eneo zima la huduma za kiusalama kutoka kwa walinzi wa maisha na mali zetu kwa maana ya Jeshi la Polisi.*

*Tuna Kituo cha Polisi hapa Kwembe ambacho kimejengwa katika eneo letu lakini hakifanyi kazi kwa sababu ya kutopangiwa maofisa wa polisi ili waweze kutuhudumia inavyostahili pindi tunapohitaji huduma za kipolisi. Kutokana na kutokuwapo na maofisa hao katika kituo hiki tulichojenga inatulazimu tusafiri kwenda Kituo cha Polisi Mbezi Kwa Yusufu ili tukapate huduma hiyo pale tunapokumbwa na matatizo ya kiusalama.*


*Sasa Mbezi kwa Yusufu kuna umbali kutoka hapa kwetu Kwembe kiasi kwamba huduma hiyo muhimu inapatikana kwa shida pale hitaji la kiusalama linapojitokeza.*

*Ninaomba mamlaka husika na hasa Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, kutuletea maofisa wa polisi katika kituo chetu ili waweze kutuhudumia na hivyo kutuepusha na adha ya kusafiri hadi Mbezi kwa Yusufu kufuata huduma hiyo.*

***Raia- Kwembe, D'Salaam***
***22/06/2019***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Kisiwa cha Saanane Mwanza kina mengi, tukitembelee

**Na Mashaka Mgeta**

**JULAI 7,** mwaka huu, ni siku ya ukumbusho wangu kufika kwa mara ya kwanza kwenye kisiwa cha Saanane kilichopo ndani ya mipaka ya jiji la Mwanza.

Nimewahi kuwa jijini humo kwa miaka mingi, lakini sikuwahi kufika kisiwani Saanane. Ilikuwa faraja kubwa.

Nilikiwa na waandishi waandamizi na wahariri wa vyombo mbalimbali waliofanya utalii wa ndani kisiwani humo, kwa uratibu na udhamini wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA). Nahodha wa boti ya kisasa ya MV Saanane 2503, Zakayo Haule, akatusafirisha zamu kwa zamu kutoka upande wa nchi kavu kwenda kisiwani.

Haule ni nahodha kama walivyo wengine, lakini namna anavyokiongoza chombo hicho cha majini, inaweza kuwa sehemu ya kivutio kwa mtu kufika mahali hapo ili kumshuhudia.

Pamoja na uwezo mkubwa wa mwendokasi wa MV Saanane 2503, Haule anamudu kukiongoza vema huku 'akipiga misele' kila anapokaribia kufika kwenye gati ili kuwapakia ama kuwashusha abiria.

Ingawa boti nyingine zinazosafirisha abiria kati ya maeneo hayo hutumia kati ya dakika nane na 10, kwa Zakayo, MV Saanane 2503 inatumia dakika nne tu, ikiwa katika hali ya utulivu kwenye ziwa Viktoria.

Kisiwa hicho chenye wanyama pori waliohamishiwa hapo kutoka hifadhi tofauti, kina maeneo kadhaa ambayo watalii wa ndani na nje wanatembezwa.

**Pembeni ya mti huo lipo jiwe kubwa ambalo mtalii anaposimama, anauona upande wa ng'ambo kwenye nyumba za wenyeji zilizojengwa kwenye vilima vya jiji la Mwanza.**

Jambo lenye maana kubwa sana ni kwamba wanaowaongoza watalii hao ni vijana wa Kitanzania hasa wanaosoma ngazi tofauti katika taaluma za utalii na uhifadhi kwenye vyuo vilivyopo jijini humo.

Wanapokuwa katika siku za mapumziko ya mwisho wa juma, vijana hao wa kike na kiume wanakwenda kujitolea, wakifanya kazi inayowaongezea maarifa ya kuzijua rasilimali za nchi, lakini pia kupata kipato kisichopungua Sh.30,000 kutoka kwa watalii.

Ingawa ni hivyo, wapo wanaowalipa kidogo ama zaidi ya hapo, lakini jambo la msingi kwao ni kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao wa kutoa maelezo sahihi kwa wageni wanaofika kisiwani Saanane.

Helena Majagi, mwanafunzi wa shahada ya kwanza ya utalii anayesoma mwaka wa pili katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agostino, ni miongoni mwa waongoza watalii anayetufikisha kwenye maeneo tofauti kwa safari 'iliyochukia' kuanzia saa nne asubuhi hadi saa nane mchana.

Unapoianza safari hiyo, sehemu ya kwanza ni wanapohifadhiwa simba, wanyama walio miongoni mwa wanaoogopwa kwa kurarua, kujeruhi na kuua.

Tofauti na simba wanaopatikana kwenye hifadhi za Taifa hivyo kutofikiwa kwa karibu, simba waliopo Saanane wamewekwa mahali maalum palipozungushiwa nyaya na nguzo imara ambazo zinawazuiwa wasiwafikie watalii.

Lakini watalii wanaweza kusogea kwa karibu kwenye nyaya hizo na kuwaona simba hao vizuri, pasipo kuhatarisha maisha yao.

Pia safari ya utalii kisiwani humo inafikisha hadi mahali tulivu pa kulitazama jua linapozama. Eneo hilo kwa kiingereza wanaliita sunset view.

Ni eneo lililozungukwa na miamba mikubwa ya mawe kwa upande mmoja, huku upande mwingine ukiwa wazi kutazama ziwa Viktoria.

Licha ya eneo hilo kuwa mahsusi kwa ajili ya kulitazama jua likizama, pia lina utulivu unaoweza kutumika kwa tafakari ya maisha ama usuluhishi kwa waliogombana kuanzia ngazi ya familia, jumuiya za watu na kwingineko. Kutokana na umaarufu wake, eneo hilo ndilo linaloitwa pia 'kona ya siri.' Unaweza kuketi na kuyatafakari yaliyomo sirini mwako pasipo bughudha yoyote.

Mwongozaji watalii, Helena akatufikisha eneo jingine linaloitwa 'viboko wa Mwalimu Nyerere.' Hii ni sehemu ambapo wanyama aina ya viboko aliowahi kutunukiwa Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Nyerere, walihifadhiwa hapo, lakini kutokana na sababu za kimazingira na hali ya hewa, walikufa mwaka 1979.

Vivutio vilivyopo kisiwani Saanane vinajumuisha pia mti wa ajabu ulioota katika umbile la twiga. Unaitwa 'mti wa twiga.'

Pembeni ya mti huo lipo jiwe kubwa ambalo mtalii anaposimama, anauona upande wa ng'ambo kwenye nyumba za wenyeji zilizojengwa kwenye vilima vya jiji la Mwanza.

Licha ya mwonekano huo, jiwe hilo ndilo linatumika kama sehemu ya kuhitimisha ziara ya kitalii ambapo watu hupatumia kwa kupiga picha wakiwa wameruka juu.

Jiwe hilo linajulikana kama 'jiwe la kurukia' ambalo mwongoza watalii, Helena anasema ni kivutio kikubwa kwa wanaofika kisiwani humo.

Hiyo ndio safari ya kitalii katika kisiwa cha Saanane, chenye wanyama tofauti wa kuvutia na ambao wanapita karibu na watalii wanapopiga picha za kumbukumbu.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Simanzi kuagwa

INATOKA UK. 2

itasaidia katika kujenga taifa bora.

**DK. MWAKYEMBE**

Serikali imetumia nafasi hiyo kutoa onyo la mwisho kwa wamiliki wa simu za mkononi za kisasa(smart phone) wenye tabia ya kupiga picha za maiti katika matukio ya ajali.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alitoa onyo hilo wakati akizungumza kwa niaba ya serikali katika ibada hiyo.

Alisema kuna watu wamepoteza utu inapotokea ajali wanakimbilia kupiga picha za miili ya wahusika na kuzisambaza kwenye mitandao ya jamii.

**MASAUNI**

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alibainisha kuwa tayari dereva wa lori ambaye alikimbia baada ya ajali hiyo amekamatwa na polisi.

Mkuu wa kikosi cha usalama barabarani nchini, Fortunatus Muslim alisema amesikitishwa na ajali hiyo kwa kuwa vijana hao wamekuwa wakishirikiana na kikosi hicho katika kuelimisha jamii masuala ya usalama wa barabarani.

"Tumepoteza wataalam ambao walikuwa na nguvu za kufanya kazi, tulikuwa tunafanya nao kazi za usalama barabarani.

**BOSI TRAFIKI**

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Muslim, alisema ajali imewakuta wakiwahi kwenye matukio kule Chato walikuwa ni wachapakazi wanaopenda taaluma yao baadaye wangekuwa ni nguli kwenye masuala ya tasnia.

Aliwataka madereva waone kuwa wana dhamana kubwa wamebeba roho na maisha ya watu, wataendelea kuwadhibiti madereva ambao hawafuati sheria za usalama barabarani.

Watu mbalimbali wakiwamo viongozi kutoka Serikali walihudhuria msiba huo,miongoni mwao ni Waziri wa Muungano na Mazingira January Makamba, viongozi wa taasisi za habari ikiwamo Baraza la Habari Tanzania(MCT).

Wengine ni kutoka Jukwaa la Wahariri (TEF) na Chama cha Waandishi wa habari Wanawake (TAMWA) na Chama cha wamiliki wa vyombo vya habari nchini MOAT na waandishi wa habari kutoka katika vyombo mbalimbali vya habari nchini.

Mmiliki na Mwenyekiti wa makampuni ya Bakhresa, Said Salim Bakhresa, Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahimu Lipumba, Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, Naibu katibu Mkuu wa chama hicho, Magdalena Sakaya ambaye pia ni Mbunge wa Kaliua.

# Msaidizi wa Membe ajisalimisha polisi Dar

INATOKA UK. 3

Magreth aliendelea kusimulia: "Allan alitaka kumsalimia mama yake ambaye wakati huo alikuwa hajalala, alimsalimia wakaongea muda wa kuondoka aliniambia nimfungulie geti ili atoke, nilifungua na kulifunga, nilikuwa nimemuomba fedha, si unajua ile kikaka kaka aniachie pocket money (fedha za matumizi) kidogo, akaniambia niende nje tuongee. Akarudi kinyume nyume, nikafunga geti, nikatoka nje. Nilipotoka nikasogelea gari lake kwa mbele ambako Allan alikuwa anaelekea kulikuwa na gari iliyokuwa ikipandisha kwa sababu kuna kibonde, ilikuwa inaelekea upande wa kulia alikokuwa Allan."

Vile vile aliendelea kusimulia kuwa, baada ya gari hiyo kupita, ilikuja nyingine aina ya Land Cruiser ikitokea nyuma ya gari la Allan.

"Hiyo Land Cruiser ilikuwa na rangi kama ya khaki, brown au gold hivi, nikamwambia Allan kuwa kuna gari nyingine nyuma ili asogee mbele aipishe, Allan aliniambia mbona njia ni kubwa sana, nikamwambia asogee ili kuepusha ugomvi, akasogea, aliposogea kama anarudi getini ile gari nayo ikasogea, nikamwambia asogee tena ili kuepusha ugomvi, aliposogeza gari alishuka na yule mtu kwenye Land Crusier naye akashuka," anasimulia.

Magreth alieleza kuwa, baada ya dereva wa gari la Land Cruiser kushuka aliangalia mbele na nyuma na akawauliza kwani vipi.

"Allan naye alimuuliza kwani vipi, na mimi nilimuuliza mbona tumekupisha hujapita, wakati namalizia kujibu nilipomgeukia Allan, nikaona watu wamezunguka gari, wawili pembeni yetu, wawili nyuma yangu na wengine walikuwa kama saba na yule kaka wa kwanza. Wakamvamia Allan na kumpiga, Allan alikuwa anasema Mage nisaidie, yule kaka wa kwanza akaninyooshea bastola, nikasikia mmoja anasema mchukue na huyo (yaani mimi), huyu hakutii alichoambiwa na mwenzake, akaniambia nifanye haraka niingie ndani, nikanyata kurudi ndani sikufunga geti na komeo, nilipofika mlango wa kuingia ndani ya nyumba nikapiga kelele Allan ametekwa."

Magreth anadai kuwa, walipotoka walikuta wameshaondoka ingawa kuna watu wa bodaboda walijitokeza na kueleza kuwa gari hilo lilipita mtaani hapo kama mara tatu. Tukio hili ni la pili baada ya la Juni 24, la mfanyabiashara Raphael Ongangi, raia wa Kenya aliyedaiwa kutekwa maeneo ya Oysterbay, jijini Dar es Salaam na watu wenye silaha akiwa na mke wake, Veronica Kundya na kupatikana Jumanne iliyopita huko Mombasa.






# JPM awaonya wabunge

INATOKA UK. 2

kuacha mara moja.

"Kumekuwapo na tabia ya viongozi wa vijiji wanapokea hela kutoka kwa wafugaji wanawaruhusu wananchi wapeleke ng'ombe zao katikati, msiruhusu ng'ombe waende huko," alisema Rais Magufuli.

Vile vile, alisema anatambua uhitaji wa maeneo ya kufugia mifugo na tayari serikali ina mpango wa kuainisha baadhi ya maeneo ya hifadhi kwa ajili ya ufugaji.

"Tunaangalia katika hii tume iliyoundwa na mawaziri wanane, tutaangalia baadhi ya maeneo ya hifadhi za misitu ambayo tutayatenga ili mifugo ipelekwe huko, watu wakafuge ng'ombe zao na tutayatangaza baadaye," alisema Rais Magufuli.

Alisema changamoto iliyokuwapo maeneo ya hifadhi yalikuwa yanapanuliwa, lakini ya wafugaji na makazi ya watu yalikuwa hayapanuliwi.Alisema kwa sasa nchini ng'ombe wamefika milioni 30.5 na kuna watu milioni 55, hivyo kama maeneo ya mifugo na ya kuishi watu hayataongezwa uvamizi utaongezeka.

Rais Magufuli aliwasihi Watanzania kuendelea kutunza maeneo yote yaliyoainishwa na serikali kuwa sehemu za vivutio sambamba na kulinda amani kwa lengo la kujiongezea kasi ya kupata watalii wengi na kusaidia kukuza uchumi wa taifa.

Alisema sekta ya utalii inachagia kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi wa taifa na asilimia 25 ya fedha za kigeni nchini zinatokana na utalii hivyo kushika nafasi ya kwanza pamoja na kutoa ajira nyingi.

Alisema kutokana na umuhimu wa hifadhi mpya tatu, serikali inaendeleza mpango wa kuendeleza utalii kwa upande wa Kusini mwa Tanzania, mpango ambao ulizinduliwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan.

Alisema mradi huo utatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 340 inayohusisha miundombinu na uwezeshaji wa wananchi.

Rais Magufuli pia aliitaka Hifadhi ya Taifa (Tanapa) kuwahamasisha Watanzania kutembelea vivutio vya hifadhi kwa kupunguza gharama za utalii kwa wazawa.

Kadhalika aliwasihi Watanzania kuanzisha hifadhi ndogo ndogo ikiwa ni sehemu ya kukuza utalii nchini.

**VIONGOZI WALIOFANIKISHA HIFADHI**

Pia, aliitaka wizara kumpongeza kwa mchango wake mkubwa wa kuwezesha kupatikana kwa hifadhi hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Adelardus Kilangi.

Wengine waliopongezwa ni aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerani mstaafu, Salum Kijuu, ambaye alipatiwa cheti na hundi Sh. milioni 10 kwa mchango wake mkubwa katika hifadhi hiyo. Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Biharamuro, Saada Malunde, ambaye alikuwa mhamasishaji na kuwasaidia wananchi wasiingie katika hifadhi hiyo, alipatiwa cheti na hundi ya thamani ya Sh. milioni tano.

Faustine Masalu Kaimu Kamishna wa operesheni za ulinzi wa hifadhi, alipongezwa kwa kuwa kiungo cha hifadhi hiyo ambaye alipatiwa cheti na hundi ya Sh. milioni 2.5

Naye Bilamungu Kagoma ambaye alikuwa Msimamizi wa pori kwa kukamata wanyama ambao hawakuwa wanakamatika ambaye alipigwa vita na kusimamishwa kazi na baadaye Rais Magufuli aliagiza arudishwe kazini, alipatiwa cheti na hundi ya Sh. milioni mbili.

Awali Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala, alisema hifadhi ya Burigi Chato iliyopandishwa hadhi kutoka katika mapori ya akiba ya BBK yaliyojumuisha Biharamuri, Burigi na Kimuso,

Awali zilikuwa zikifanyika shughuli za uwindaji katika mapori hayo, hivyo shughuli hizo zitabadilika, kutakuwa na ulinzi wa kutosha na usalama wa eneo lote.

Alisema hifadhi hiyo ya tatu kwa ukubwa nchini ikitanguliwa Ruaha na Serengeti itakuza sekta ya utalii kwa sababu wana uhusiano wa karibu na wakazi wa mikoa inayozungukwa na hifadhi hiyo.

## Majaliwa ataja mambo 3 yaliyopaisha uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa, amesema hatua ya kudhibiti upotevu wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali, uboreshwaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji pamoja na kusimamia uwajibikaji kwa watumishi wa umma kumesababisha kukua kwa uchumi.

Amesema Tanzania ni nchi yenye amani na utulivu na Serikali imeendelea kuongeza nguvu katika kudumisha amani na utulivu kwenye maeneo yote nchini, hali inayotoa fursa kwa wananchi wake kuendeleza shughuli zao za maendeleo.

Waziri Mkuu aliyasema hayo juzi alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri Mkuu wa Misri, Dk. Mostafa Madbouly, akiwa katika siku yake ya kwanza ya ziara yake ya kikazi nchini Misri.

Hivyo, amemuhakikishia Waziri Mkuu wa Misri kwamba Serikali ya Tanzanzia na wananchi wake wapo tayari kuendelea kushirikiana na Serikali ya nchi hiyo na wananchi wake katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi hizo mbili.

Alisema Tanzania na Misri zinahitaji kutumia nafasi ya ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji katika ukuzaji wa uchumi, hivyo Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kuwakaribisha wawekezaji na wafanyabiashara kutoka Misri waje kuwekeza nchini.

Amesema Serikali ya Tanzania imefanikiwa kiuchumi na kwa sasa ni nchi ya pili ambayo uchumi wake unakua kwa kasi barani Afrika, ikitanguliwa na nchi ya Ivory Coast. Uchumi wa Tanzania ulitarajiwa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka jana kutoka asilimia saba.

"Hali ya uchumi wa Tanzania inaendelea vizuri, tumeendelea kushuhudia kushuka kwa mfumuko wa bei ambapo kwa sasa tumefikia asilimia 3.2, kiwango hiki ni matokeo ya kukuza sekta za madini, ujenzi, mawasiliano, utalii pamoja na kushuka kwa bidhaa za chakula na mafuta. Tunatarajia kiwango hiki kitashuka zaidi kwa sababu ya uwekezaji."

### KUELEKEA MKUTANO SADC:

# Waziri ataka fursa zitangazwe

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WIZARA ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, imetoa wito kwa vyombo vya habari nchini kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo Tanzania wakati wa mkutano ujao wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

**Watu wengi hawaijui SADC na umuhimu wake. Ni kupitia vyombo vya habari watu wanaweza kujua umuhimu wa jumuiya hii.**

Mkutano huo wa siku mbili wa wakuu wa nchi za jumuiya hiyo, umepangwa jijini Dar es Salaam kuanzia Agosti 17, ukitanguliwa na mikutano ya mawaziri wa SADC na sekretarieti ya jumuiya hiyo itakayoanza Agosti 9 hadi 16, mwaka huu.

Rai hiyo ilitolewa jana mjini Morogoro na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, alipofungua siku tatu ya kuwajenga uwezo waandishi wa habari kuhusu mkutano huo na SADC kwa ujumla.

Mafunzo hayo yameandaliwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU), Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la Misaada (GIZ).

"Vyombo vya habari vina jukumu kubwa la kuufahamisha umma kuhusu fursa ya kiuchumi, siasa na kijamii zinazopatikana ndani ya SADC. Ni vizuri wananchi wakaelewa umuhimu wa Tanzania kuwa mwanachama wa jumuiya," Shonza alisema.

Naibu waziri huyo alisema Tanzania inapaswa kuutumia mkutano huo kutangaza fursa za kiuchumi na uwekezaji zinazopatikana nchini na kutengeneza mazingira mazuri ya kunufaika zaidi na soko la biashara ndani ya jumuiya hiyo ambayo kwa sasa inakadiriwa kuwa na idadi ya watu inayofikia milioni 450.

Shonza alisema vyombo vya habari vinapaswa kutangaza fursa zilizopo nchini wakati wa mkutano huo, akiwataka waandishi wa habari kuwa wazalendo kwa kuhakikisha wanatangaza na kuchapisha masuala yenye maslahi kwa nchi.

"Ni mkutano muhimu na ni heshima kwa Tanzania kuwa mwenyeji, ni fursa ya kipekee kwa sababu mara ya mwisho ulifanyika nchini mwaka 2003. Tuutumie mkutano huu kutangaza sera ya uchumi wa kati unaochagizwa na viwanda kufikia mwaka 2025 kwa kutafuta masoko ya nje kwa bidhaa tunazozalisha," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ushirikiano wa Kikanda katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Agnes Kayola, alisema mafunzo hayo yameandaliwa kwa lengo la kuwajenga uwezo waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu SADC.

Alisema mkutano huo unahusisha waandishi wa habari 60 kutoka vyombo mbalimbali nchini na utafanyika kwa awamu mbili.

Dagmore Tagwoneuzi, mwakilishi wa GIZ kutoka ofisi ya shirika hilo ya Gabarone, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya mradi wao wa kuwajenga uwezo wanachama wa SADC kuhusu masuala yanayoihusu jumuiya hiyo.

"Watu wengi hawaijui SADC na umuhimu wake. Ni kupitia vyombo vya habari watu wanaweza kujua umuhimu wa jumuiya hii," alisema.

Wakati wa mkutano huo unaotarajiwa kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 1,000, Rais John Magufuli atakabidhiwa uenyekiti wa SADC.

Rais Magufuli aliteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa jumuiya hiyo



Machinga wakinadi shuka kwa staili yao, wakati wakisubiri wateja kando ya Barabara ya Msimbazi, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. Shuka moja liliuzwa kwa Sh. 8,000/- hadi Sh. 10,000/-. **PICHA: JOHN BADI**

# Waziri atoa siku saba Shirika la Posta

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, ametoa siku saba kwa uongozi na bodi ya Shirika la Posta Tanzania kumpelekea orodha ya wakuu wa idara na mameneja waliokopeshana fedha za shirika kinyume cha utaratibu.

Kauli hiyo aliitoa jijini hapa wakati akifungua mafunzo ya siku sita ya wakuu wa idara na mameneja wa Shirika hilo. Alisema ameshangazwa na tabia ya viongozi hao kukopeshana fedha wakati hakuna mfumo wa aina hiyo.

"Nasikia nyie mameneja mnakopeshana fedha nyie kwa nyie, eti Katibu Mkuu wewe umewahi kukopa?, nimeshangaa kweli hatuwezi kukopeshana fedha kwa mfumo huo mnaofanya, naagiza kuanzia leo ni marufuku," aliagiza Kamwelwe.

Alisema hatua ya viongozi wa shirika kukopeshana si sahihi kwa fedha ya serikali. Aliagiza kupatiwa orodha ya viongozi wa shirika hilo waliokopeshwa fedha ndani ya siku saba.

Hata hivyo, Kamwelwe alisema ili kudhibiti hali hiyo ni vyema Shirika hilo likahakikisha linafunga mifumo laini ya kieletroniki ya ukusanyaji mapato na kubainisha maeneo ambayo itakuwa ni vigumu kukusanya kwa mfumo huo.

Alisema alishatoa maagizo kuhakikisha taasisi zote zilizochini ya wizara yake zinakuwa na mifumo laini ya ukusanyaji mapato.

"Tungekuwa na mifumo kama hii hata Posta Masta Mkuu angejua kuna fedha watu wanakopeshana, lakini pia mfumo laini utasaidia kudhibiti wa fedha maana kwa kupokea fedha taslimu kunafanya wafanyakazi wasio waaminifu kupiga juu kwa juu," alisema.

Akizungumzia kuhusu magari ya shirika kuhusika katika biashara ya kubeba abiria na mizigo haramu, alionya tabia hiyo huku akisema amemwambia Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), magari hayo kukaguliwa ikiwamo yanayosafirisha magazeti.

"Shirika hili linabeba mizigo nyeti, lakini nimeshuhudia magari ya shirika na yale ya kusafirisha magazeti yakitumika kufanya biashara ya kubeba abiria na mizigo haramu kwa sababu ya kutokaguliwa na ndio maana nimemwambia IGP kufanya ukaguzi mara moja moja," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Kamwelwe aliagiza watumishi wote walioajiriwa na shirika hilo hivi karibuni kupelekwa kuhakikiwa kwenye Sekretarieti ya Ajira kwa ajili ya uhakiki hata kama wamepewa mikataba ya ajira.

"Hili shirika lilikuwa na shida ya kupeana ajira kindugu ndugu, tatizo hilo pia lipo Shirika la Simu (TTCL) na Mamlaka ya Bandari na ndio maana nimeagiza taasisi zilizo chini yangu hata ngazi ya mhudumu ajira ipitie sekretarieti ya ajira,"alisema.

Kamwelwe alitoa mwezi mmoja kwa uongozi wa shirika hilo na bodi kuhakikisha wanasimamia kwa karibu kitengo cha manunuzi.

SABASABA

# Wafanyabiashara watakiwa kutangaza Kiswahili kimataifa

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, amewataka wafanyabiashara kuipeperusha lugha ya Kiswahili kimataifa.

Alisema kwa kufanya hivyo, watatangaza lugha ya Kiswahili katika mataifa ambayo bidhaa zao zinapelekwa

Manyanya alitoa kauli hiyo katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), katika viwanja vya Sabasaba. Manyanya alisema licha ya kutumika kwa lugha ya Kiswahili katika matangazo mbalimbali ya bidhaa hizo lakini pia zinatakiwa kuambatanishwa na lugha nyingine kwa ajili ya kulenga hitaji la soko

**Kwa kufanya hivyo, watatangaza lugha ya Kiswahili katika mataifa ambayo bidhaa zao zinapelekwa.**

Aliiagiza Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kuwapima washiriki mmoja mmoja kila maonesho yanapoisha ili kujua wamekuwa au kuongezeka kibiashara kwa kiasi gani ili kubainia upungufu na kuwasaidia

Pia alisema kwa sasa serikali ina mkakati kwa Bandari na Mamlaka za Anga kuangalia namna ya kusafirisha bidhaa za mbogamboga zinazoharibika haraka kwa kwa kuweka vifaa maalum vya



Habari na Elizabeth Zaya

kusafirisha bidhaa hizo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TANTRADE, Edwin Rutageruka, alisema mamlaka hiyo imeweka mikakati mbalimbali kuongeza masoko katika mazao ya kimkakati kwa kuwa na mtu mmoja anayeshughulikia bidhaa hizo na kuwa na intelijensia na masoko.

Alisema mkakati huo unalenga kufahamu hitaji la soko na washindani waliopo pamoja na kushauri wafanyabiashara kutafuta masoko.



Wananchi wakijaza fomu za kuomba vyeti vya kuzaliwa kwa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TPDC yahamasisha matumizi gesi asilia

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), limewataka Watanzania kuhamasika kutumia nishati ya gesi asilia katika Viwanda, Gari, Majumbani na shuleni ili kupunguza gharama kwa kuwa ni nafuu zaidi.

Shirika hilo limesema EWURA imeshaweka sheria ya punguzo la asilimia kubwa ya gharama kwa watumiaji hao.

Akizungumza katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF), Mhandisi wa TPDC, Evaline Rweikiza, alisema gharama zimepunguzwa ili kumfanya Mtanzania amudu na kuhamasika kutumia nishati hiyo.

Alisema kwa watumiaji wa viwanda ambao walikuwa wakitumia mafuta mazito watapata punguzo la asilimia 30 kutoka bei waliyokuwa wakinunua mafuta, huku wenye magari waliokuwa wakitumia petroli au dizeli, watapata punguzo la asilimia 40 tofauti na gharama ya awali Aliongeza kuwa kwa taasisi kama shule au vyuo watapata punguzo la asilimia 30 kutoka gharama waliyokuwa wakinunulia nishati hiyo na majumbani wanaotumia mkaa watapata punguzo la asilimia 35.

Alisema hadi sasa tayari magari 200 yametengenezwa kutumia nishati ya gesi

Aliongeza matumizi ya majumbani kwa mikoa ya Dar es Salaam na Mtwara yameongezeka kutoka nyumba 70 mwaka 2014 hadi nyumba 96 mwaka huu.

Alisema mpango wao ni kuongeza nyumba 337 zitakazotumia gesi asilia kufikia Septemba mwaka na nyumba 1,000 kufikia mwisho mwa mwaka kesho.

Alisema wanatarajia kusambaza gesi asilia kwa mikoa mitano mingine ya Tanga, Dodoma, Morogoro, Pwani na Lindi.

## Bidhaa za wazawa zapigiwa debe

WATANZANIA wametakiwa kutumia bidhaa ambazo zinazalishwa na wazawa na kuachana na dhana kuwa zinazozalishwa nje ya nchi ni bora zaidi.

Akizungumza katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara, Mwenyekiti wa Bodi wa Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Peter Maduki, alisema wananchi wanapaswa kutambua ubora katika bidhaa hizo

Alisema ujuzi unaotolewa nje ya nchi upo kwa wataalamu wazawa na wamekuwa wakibuni na kutengeneza bidhaa za viwango vikubwa.

Alisema VETA imekuwa ikishirikiana na wadau ambao wamekuwa wakizalisha kwa wingi bidhaa za ndani ili kusaidia kuboresha zaidi.

"Tayari tumeshirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na wameanza kutusaidia kuboresha ubunifu kwa walengwa ili kufikia kiwango kikubwa zaidi , serikali yetu imetuwezesha sasa kazi yetu ni kusonga mbele," alisema Maduki.

Aliongeza VETA imekuwa ikitoa somo la ujasiliamali ambapo imeingia mkataba na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kwa ajili ya kuwasaidia wabunifu kuzalisha bidhaa bora zaidi.

Akizungumzia kuhusiana na vitu ambavyo vimekuwa vikizalishwa na VETA, Maduki alisema vijana wanajifunza vitu ambavyo wanaweza kuvitumia kupitia ubunifu walioufanya.

## VETA ilivyojipanga kutatua changamoto

MKURUGENZI Idara ya Elimu Mbadala na elimu ya Watu Wazima Zanzibar, Mashavu Ahamada Fakh, amesema Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) imejipanga katika kutatua changamoto katika jamii katika ubunifu uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Mashavu aliyasema hayo wakati alipotembelea Banda la VETA katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa, kwamba wanachofanya VETA kinatakiwa kifanyike na Zanzibar ili kuwasaidia vijana wabunifu.

Alisema kwa hatua waliofikia VETA wanakwenda katika uchumi wa viwanda kutokana na uzalishaji wa vijana kuchangamkia fursa mbalimbali.

Mashavu alisema vijana wanaopita VETA wanauwezo mkubwa katika sekta ya ajira kwa kujiajiri kutokana na ujuzi walioupata.

Meneja wa Mawasiliano wa VETA, Sitta Peter, alisema kwa sasa wana ujenzi wa vyuo vya mikoa mbalimbali lengo ni kuwasaidia vijana kupata mafunzo ya ufundi stadi.

Alisema kuwa maonyesho hayo yanatoa fursa kwa wazazi na vijana kuona VETA na kuchukua nafasi kupata mafunzo na kuwasaidia vijana wao kutoa ushauri kuhusu umuhimu wa mafunzo ya ufundi stadi.

## Mahakama yasisitiza matumizi ya Tehama

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Eliezer Feleshi, amesema wamejipanga kuboresha mahakama zote nchini kuanzia ngazi ya wilaya kutumia mfumo wa kielektroniki kuweka taarifa zake zote mtandaoni ikiwamo kusajili kesi na kuweka maamuzi ya kesi mbalimbali zinazotolewa mahakamani

Feleshi alitoa kauli hiyo alipotembelea banda la Mahakama katika Maonyesho ya 43 Biasahara ya Kimataifa Dar es Salaam.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuwapa fursa wananchi kusoma maamuzi ya kesi zote zinazotolewa mahakamani kupitia njia ya mtandao badala ya kutumia muda mwingi kusafiri kwenda mahakamani kufuatilia

Pia katika mfumo huo wa kielektroniki alisema wananchi watautumia katika malipo mbalimbali kwa ajili ya kulipia huduma za kimahakama, kuwasilisha malalamiko na huduma mbalimbali

"Lengo ni kumrahisishia mwanchi kutafuta kesi yoyote iliyokwisha amriwa mahakamani na kuisoma bila kwenda mahakamani," alisema Feleshi na kuongeza:

"Na ndiyo maana ninasema kwamba mahakama zetu zote zinatakiwa kutumia mfumo huu wa mtandao ili kuondoa habari za watu kulalamika kuzungushwa kupatiwa kesi zilizokwishapatiwa uamuzi."

# Serikali yataifisha madini ya zaidi ya mil. 53/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha jana imetaifisha madini ya Tanzanite na mengine yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 53, ambayo yamekutwa nyumbani kwa mfanyabiashara wa madini hayo, anayemiliki kampuni ya Sky Gems Ltd.

Madini hayo yametaifishwa na kuwa mali ya serikali, baada ya ya mfanyabiashara huyo Ushma Patel(40) pamoja na mume wake Vijan Patel (48), kukiri kuhifadhi madini hayo bila ya kuweka kumbukumbu ya taarifa sahihi ya usajili wa kuyamiliki.

Wakisomewa mshtaka yao mawili mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama yaArusha, Niku Mwakatobe, Wakili wa Serikali Tarsila Asenga, akiongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Materus Marandu na wakili Shedrack Maro, alidai mahakamani hapo kuwa Patel na mume wake wanakabiliwa na makosa mawili.

Alidai kosa la kwanza ni kukutwa na madini ya Tanzanite na mengine bila ya kuweka kumbukumbu na shtaka pili ni kuhifadhi madini hayo nyumbani bila kufuata taratibu za madini. Wakili Asenga alidai kuwa tarehe Aprili 16 mwaka huu, Mkurugenzi huyo anayemiliki kampuni ya Sky Gems Ltd, yenye leseni namba DL 00000573, alikutwa na madini ya Tanzanite kilogramu 17.970 yenye thamani ya Sh. 26,198,300.729

Madini mengine ni aina ya Grossulate yenye kilo 4. 170 na thamani ya Sh. 6,436,837.478, madini ya Tsavorite yenye thamani ya Sh. 8,629,092.387, Green Garnet kilo 70 yenye thamani ya Sh. 29,144 .801,kilogramu moja na gramu 307.2 ya madini aina ya Spessartite yenye thamani ya Sh. 919,383.904.

Mengine ni kilogramu 5.490 za madini aina ya Amethyst yenye thamani ya Sh. milioni 10 na baada ya kusomewa aina za madini hayo na kuchukuliwa kama vielelezo mahakamani hapo, washtakiwa hao walikiri makosa yao na ndipo hakimu Mwakatobe aliamuru wakili huyo, kuwasomea maelezo ya awali washtakiwa hao.

Washtakiwa hao walikiri kuhifadhi madini hayo nyumbani kwao jijini Arusha kinyume na utaratibu na kuiomba mahakama hiyo, kutowapa adhabu kali kwa kuwa ni kosa lao la kwanza na wana wazazi wanaowategemea.

# Miundombinu maji ya mifugo kutumia Mil.107/-

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WIZARA ya Maji inatarajia kutoa Sh.million 107, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mifugo kunywa maji, wilayani Longido na kuondoa migogoro baina ya wafugaji na serikali ya uharibifu wa miundombinu ya mradi wa maji, kutoka Mto Simba, Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro, uliogharimu zaidi ya Sh.bilioni 16.

"Mradi huu ni fedha zetu za ndani hakuna fedha ya wafadhili, sheria ipo wazi kwa wale watakaohujumu mradi kwa kutoboa mabomba, sheria inafafanua kuwa faini ni kuanzia Sh.500,000 hadi Sh.milioni 50, au kifungo cha miaka miwili na ikiwezekana vyote kwa pamoja," alisema Prof. Mkumbo.

**Mradi huu ni fedha zetu za ndani hakuna fedha ya wafadhili, sheria ipo wazi kwa wale watakaohujumu mradi kwa kutoboa mabomba.**

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema hayo katika hafla ya makabidhiano ya mradi huo kati ya Mamlaka ya maji Wilaya ya Longido na Mamlaka ya majisafi na usafi wa mazingira Mkoa wa Arusha (AUWSA), ambao watasimamia mradi.

Prof. Kitila alisema huo ni uamuzi wa serikali, ikiwa ni sehemu ya agizo la Rais John Magufuli wa kutaka mamlaka zote za maji zijitegemee.

Alisema lengo hasa ni kuanzishwa kwa wakala wa majisafi na usafi wa mazingira vijijini, ikiwa ni kupanga na kusimamia uwezeshwaji wa maji vijijini na serikali ipo katika hatua ya kusimika mamlaka hiyo rasmi, hivyo mamlaka ya maji Longido, kuanzia sasa itakua chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Maji Mkoa wa Arusha (AUWSA).

"Maeneo mengine ambayo yatakuwa chini ya AUWSA ni Ngaramtoni, Usariver, Monduli pamoja na Longido," alisema Prof. Kitila

Pia alisema changamoto kubwa katika sekta ya maji ni baadhi ya miradi ya miaka ya nyuma kutokamilika kwa wakati, kutokana na baadhi ya makandarasi kushindwa kutekeleza majukumu yao. Akitoa mfano alisema mradi wa maji Mkoa wa Kilimanjaro, ulioanza tangu mwaka 2014, hadi sasa hauja kamilika.

"Nawapongeza viongozi wote Mkoa wa Arusha na hata ngazi ya Wilaya ya Longido,mradi huu mmeusimamia vizuri, lakini naomba hadi itakapofika mwisho wa mwezi huu, wale wote waliokuwa wamejiandikisha katika mpango wa kupata maji waunganishiwe na kwa sasa wauziwe ndoo ya maji Sh. 20 wakati AUWSA ikiendelea na mikakati ya kupanga bei kwa kushirikiana na Ewura," aliomba Prof. Kitila.

Alitangaza rasmi jana kuwa mradi mkubwa wa maji kutoka chanzo cha maji Mto Simba Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, uliotekelezwa na serikali kuu, katika Wilaya ya Longido wenye thamani zaidi ya Sh.bilioni 16 ikiwa ni fedha za ndani, umekamilika na utakuwa chini ya usimamaizi wa AUWSA.

Mkurugenzi waAUWSA, Mhandisi Ruthi Koya, alisema Wilaya ya Longido ilikuwa na upungufu wa majisafi na salama, lakini kupitia mradi huo, majisafi na salama yapo na yanatarajiwa kuhudumia watu 26,142 ifikapo mwaka 2024.



Mtunza Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, Nasoro Mkwenda, akisoma taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2017/2018, katika kikao cha baraza la madiwani juzi, ambapo wilaya hiyo imepata hati safi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Watakiwa kuhamasisha chanjo saratani shingo ya kizazi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAZAZI na walimu wametakiwa kuwa mstari wa mbele kuwahamasisha wasichana wenye miaka 14 kupata chanjo ya kuwakinga na saratani ya shingo ya kizazi, ambayo kwa sasa ni tishio kwa uhai wa watoto wa kike watakaoikosa.

Mratibu wa chanjo wa Halmashauri ya Mji wa Babati na Ofisa Afya wa Mji huo, Grace Ngoo, alisema hayo wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu chanjo hiyo.

"Baadhi ya wazazi, walezi na walimu ni kikwazo cha kuwaandaa wasichana, wanaotakiwa kupata chanjo kwa kuingiza imani za kishirikina," alisema Grace.

Alisema chanjo ambayo inatakiwa waipate ni HPV, ambayo inawakinga na saratani ya shingo ya kizazi na wanaotakiwa kuchanjwa ni kuanzia miaka tisa hadi miaka 14.

"Kwa Tanzania hasa Manyara sisi tunachanja wale waliotimiza miaka 14, kutokana na upatikanaji wa hizo chanjo na hii ni mpya na ina gharama kubwa," alisema.

Pia alisema chupa moja inatumika na msichana mmoja na kila moja inauzwa Sh. 10,890 au Dola za Kimarekani 4.95," alisema.

Grace alisema mwitikio wa wazazi kuwahamasisha watoto wao bado ni mdogo, pamoja na chanjo kuwapo ingawa awali zilikuwapo chache.

Alisema wasichana waliochanjwa mwaka 2018, walikuwa 692 sawa na asilimia 66 na waliokuwa wamelengwa ni wasichana 1,063 kwa chanjo ya HPV1, na HPV2 waliochanjwa wasichana 153, sawa na asilimia 14 waliokuwa wamelengwa ni 1,063.

Vile vile alisema kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu, wasichana waliolengwa ni 379, waliochanjwa HPV1 ni 84 sawa na asilimia 22, chanjo ya HPV2 waliolengwa 379 na waliochanjwa ni 133 sawa na asilimia 35.

Alizitaja miongoni mwa changamoto zinazowakabili ni wanafunzi wanapomaliza shule, wanaenda kusoma mbali na hawarudi kupata chanjo hiyo na wengine wanaenda kufanyishwa kazi za ndani.

"Na wanaochanjwa ni vizuri tutambue kuwa siyo wanafunzi tu bali na waliopo nyumbani, ilimradi wawe wametimiza miaka 14," alisisitiza.

Alisema changamoto nyingine waliyonayo kutokuwa na gari la kwenda kuhamasisha chanjo.

Naye Martha Damian, aliwataka wataalamu wa afya, kutoka ofisini na kuingia mitaani kutoa elimu, ili jamii iweze kubadilika na kupata chanjo hiyo.

# Wataka waliotia hasara shule kubomoa madarasa

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WANANCHI wa Kijiji cha Namwai katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, wamegoma kubomoa madarasa mawili ya Shule ya Sekondari Namwai, yanayodaiwa kujengwa chini ya kiwango, wakitaka waliohusika kuitia hasara serikali wabomoe wenyewe.

Uamuzi wa wananchi hao unatokana na amri iliyotolewa na serikali ya kijiji hicho kutaka wakazi wake washiriki kubomoa madarasa hayo ili kupisha ujenzi mpya.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho (VEO), Seif Mwamgamba, alisema sababu kubwa iliyochangia madarasa hayo kuonekana yako chini ya kiwango ni aina ya malighafi iliyotumika kujengea kama mchanga kukosa ubora.

**Leo hii viongozi wetu wanadai sisi wananchi tukabomoe majengo hayo, tumekataa tumewaambia wale waliohusika kwa sababu wapo wakabomoe wao.**

"Ni kweli majengo hayo yalianza kujengwa mwaka 2010, yako katika hatua ya lenta yakisubiri kupauliwa na kufikia usawa wa kupauliwa. Kimsingi mchanga wa maeneo haya sio mzuri katika ujenzi hata nyumba zetu zinachoka mapema, ndio maana na hii imekumbwa na tatizo hilo," alisema Mwamgamba.

Akitoa ufafanuzi kuhusu taarifa hiyo, Mhandisi wa ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Mbaraka Kiure, alithibitisha kuwa, baada ya kutembelea shule hiyo aliona majengo hayo hayafai, kwa kuwa wakati wowote yanaweza kuanguka.

Alisema kwa sasa, zipo fedha zilizotumwa na serikali kiasi cha Sh.milioni 25 zitatumika kwaajili ya ujenzi mpya wa madarasa hayo.

Kutokana na mvutano huo, baadhi ya wananchi wa Namwai wametaka watu wote waliohusika kujenga madarasa hayo mawili chini ya kiwango wachukuliwe hatua.

Mmoja wa wananchi wa kijiji hicho, John Sunguya, alisema walichanga fedha za ujenzi huo kwa zaidi ya awamu tatu, na kila awamu, kila kaya ilichangia kiasi cha Sh.5,000.

"Leo hii viongozi wetu wanadai sisi wananchi tukabomoe majengo hayo, tumekataa tumewaambia wale waliohusika kwa sababu wapo wakabomoe wao.

"Hata mchango mingine hatutachanga kama watu hao hawatachukuliwa hatua za kisheria, tulibambuliwa vitu vyetu kwa wale ambao hawakuwa na fedha na hadi sasa vipo ofisi ya kijiji," alisema.



Mhasibu Mkuu wa Serikali, Francis Mwakapalila, akizungumza na washiriki wa mafunzo ya Mfumo mpya wa Ulipaji Serikalini (MUSE), kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), mkoani Morogoro jana. **PICHA: TARURA**

# CCM yafafanua mil. 50/- kila kijiji

**Na Paul William,** MOSHI

CHAMA cha Mapinduzi (CCM), kimesema ahadi ya Sh. milioni 50 kwa kila kijiji inayotajwa katika ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2015, inaendelea kutekelezwa kupitia miradi ya maendeleo na si kama inavyotafsiriwa vibaya na wanasiasa wa vyama vya upinzani nchini.

Akizungumza na wanachama wa chama hicho kwa nyakati tofauti jana katika maeneo ya Moshi Mjini na Moshi Vijijini, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alisema fedha hizo zimeshapelekwa katika miradi ya maendeleo.

Akiwa katika mkutano huo, Dk.Bashiru alisema chama hicho katika kampeni zake za mwaka 2015 kiliahidi kutoa Sh. milioni 50 kwa kila kijiji, lakini hakikueleza bayana kama fedha hizo zitakabidhiwa tasilimu. Badala yake ahadi hiyo, ikatekelezwa kwa fedha hizo kuelekezwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuwanufaisha wananchi wote.

Kuhusu malalamiko ya wananchi wa Vunjo kuchangishwa fedha kinyume na utaratibu wa serikali ili kuchangia ujenzi wa miundombinu ya barabara, Dk. Bashiru ameagiza Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira na Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, kukutana na uongozi wa Taasisi ya Maendeleo ya Vunjo (VDF).

"Kufanya kazi bila kufuata utaratibu wa serikali ni makosa, Mkuu wa mkoa na wilaya husika, waiteni viongozi wa taasisi hiyo na muwape taratibu zinazotakiwa kufuatwa kwa ajili ya maslahi mapana ya umma.

"Huwezi kuleta maendeleo kwa wananchi, nje ya mfumo wa serikali na wala sio shida, zungumzeni naye azifuate kanuni ili atekeleze vizuri ilani ya CCM," alisema.

Katika mkutano huo, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya kichama ya Moshi Vijijini, Sirili Mushi, alisema taasisi hiyo ya maendeleo ya Vunjo imekuwa ikikiuka masharti ya usajili na imekuwa ikikusanya fedha kwa wananchi bila kuwa na kibali cha serikali.

Pia, alieleza kuwa taasisi hiyo imekuwa ikifanya kazi za Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), ili kuichafua serikali.

# PM kuzindua uboreshaji Daftari la Wapigakura

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuzindua rasmi uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura Julai 28, katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Taarifa iliyothibitishwa jana na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage, imeeleza kuwa Kilimanjaro ni mkoa wa kwanza ulioteuliwa kuanza mpango huo na baadaye kufuatiwa na mikoa mingine.

Uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura unafanyika wakati taifa linajiandaa kushuhudia uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwezi Oktoba, mwaka huu.

"Mipango yote inayohusiana na zoezi hili imekamilika na Tume kwa upande wetu tunaahidi kuzingatia sheria za uchaguzi na kanuni zake, hivyo niwaombe wadau wote wakiwamo viongozi wa vyama vya kisiasa kuungana na NEC katika zoezi hili ili liweze kufanikiwa," alisema.

"Tume kama ilivyo ada, kabla ya kuanza kwa zoezi hili itaendelea kuwashirikisha wadau wake kwa njia mbalimbali," alisema.

Kwa mujibu wa Jaji Kaijage, Tume hiyo pia itaendelea kutoa elimu kwa wapigakura kwa kutumia njia mbalimbali ikiwamo vyombo vya habari ili kuwafikia walengwa.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dk. Athuman Kihamia, alisema baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, kumefanyika uhakiki wa vituo vya kuandikishia wapiga kura kwa lengo la kuviweka vituo katika maeneo yanayokubalika.

Alisema kuwa uhakiki huo pia ulilenga kuweka angalau kituo kimoja katika kila mtaa au kijiji, kwa kuzingatia umbali na idadi ya watu katika eneo husika.

"Matokeo ya uhakiki wa vituo hivi vya kupigia kura yanaonyesha eneo la Tanzania Bara, vituo hivyo vimeongezeka kutoka 36,549 mwaka wa 2015 na kufikia vituo 37,407 mwaka wa 2018," alisema.

Pia, alisema katika kipindi hicho, vituo 6,208 vimebadilishwa majina, 817 vimehamishwa ndani ya kata husika na 19 vimehamishwa nje ya kata husika.

Kwa upande wa Zanzibar, vituo hivyo vimeongezeka kutoka 380 mwaka wa 2015 na kufikia vituo 407 mwaka wa 2018.

Ukurasa 18



**Ujerumani yapata kiwewe Kansela Merkel kutetemeka mara mbili**

## UCHAMBUZI:

Mwenge wa Uhuru 2019, hamasa kwa uchaguzi wa serikali za mitaa



Ukurasa 19

**Kitaifa**



**Magufuli, Kenyatta wawe mfano kuiimarisha EAC**

Ukurasa 14


# siasa

JUMATANO JULAI 10, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




**Ukanda huru wa biashara Barani Afrika wazinduliwa**

Ukurasa 17

## BAADA YA MIAKA 55


# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-4

MZEE Pius Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Pia, Mzee Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu na kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho HISTORIA YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa

Endelea 16



Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa.
**PICHA: MTANDAO**

**Uingereza, China zahitilafiana mzozo wa kuhamisha watuhumiwa ukipamba moto**

Ukurasa 20

# Magufuli, Kenyatta wawe mfano kuiimarisha EAC

Na Mashaka Mgeta

WIKI iliyopita, marais wa Tanzania na Kenya, Dk John Magufuli na Uhuru Kenyatta, walikutana Chato mkoani Geita na kufanya mazungumzo yaliyolenga kuchagiza ushirikiano katika nyanja tofauti kwa mataifa hayo yaliyo wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Mazungumzo hayo yalikuwa ni sehemu ya ziara ya siku mbili ya Rais Kenyatta aliyoifanya nchini kati ya Julai 5 na 6 mwaka huu na kukutana na Rais Magufuli aliyekuwa mapumziko nyumbani kwake, Chato mkoani Geita.

Rais Kenyatta akafurahishwa kufika Chato umbali wa takribani kilomita 129 kwa kusafiri kwa ndege kutoka jijini Mwanza lilipo ziwa Viktoria.

Akasema furaha yake ilichochewa na ukarimu wa Watanzania waliompokea na kula samaki wa kutoka ziwa Viktoria, hivyo akamualika Rais Magufuli naye kumtembelea nyumbani kwake, kijiji cha Ichaweri, Kaunti ya Kiambu wanapoishi zaidi Wakenya wa jamii wa Gikuyu ambao chakula chao maarufu ni githeri.

Haikuwa mara ya kwanza kwa marais hao kukutana ama kwa Rais Kenyatta kufika hapa nchini.

Lakini ziara hiyo ilikuwa na maana kubwa hasa kutokana na ukweli kwamba ilifanyika siku chache baada ya Mbunge wa Jimbo la Starehe nchini Kenya, Charles Njagua maarufu kama Jaguar 'kutangaza vita' dhidi ya wafanyabiashara wa kigeni wakiwamo Watanzania, wanaofanya shughuli zao nchini humo.

Njagua alitoa karipio hilo lililosambaa zaidi kupitia mitandao ya kijamii, akielezea kuwa wafanyabiashara hao wa kigeni walipaswa kujiondoa wenyewe kutoka kwenye soko la Gikomba na mengineyo nchini humo, vinginevyo wangeondolewa kwa kupigwa.

Rais Kenyatta akagusia suala la Mbunge huyo pasipo kumtaja, akishangaa kwa kusema , "mtu fulani anatazama pale anapoishi tu, anafikiri ndipo ilipo mipaka ya mwisho wa dunia... mmewasikia miongoni mwao wakiropoka. Unawaambiaje Watanzania wasifanye biashara zao Kenya."

Kauli ya Mbunge huyo ingeweza kupuuzwa hasa kutokana na uhusiano wa muda mrefu na mwingiliano wa kijamii uliopo kati ya raia wa Kenya na Tanzania, lakini kumbukumbu za matukio yaliyotokana na kauli kama yake ililazimu kuchukua hatua za haraka kuokoa madhara ambayo yangeweza kutokea.

Ikumbukwe kwamba miongoni mwa matukio ya kibaguzi dhidi ya raia wa kigeni, wengi wao wakiwa kutoka ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika, yamewahi kutokea Afrika Kusini na kusababisha hasara kubwa ikiwamo kujeruhi na vifo.

Hivyo, Rais Kenyatta alipofanya ziara yake nchini Tanzania, halikuwa jambo la kawaida, ama kuchukuliwa kama ishara ya 'kumpaisha' Mbunge Njagua, isipokuwa kuyafikia matamanio ya kuwa na Afrika Mashariki yenye amani, utulivu na mshikamano.



Rais John Magufuli (kulia), akiagana na mgeni wake Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya. **PICHA: MTANDAO**

Godfrey Masatu, mfanyabiashara wa jijini Mwanza anasema kwa muda mrefu amekuwa akifanya shughuli zake kati ya Tanzania na Kenya na kuwa na uhusiano wa karibu wa kibiashara na wenzake wa upande wa Kenya.

"Ninapofika Kenya kuanzia Isibania, Migori, Kisii, Kisumu hadi Nairobi huwa nanijisikia kama nipo Tanzania na uhusiano wetu wa kawaida na raia wa Kenya ni mzuri usiotiliwa shaka," anasema.

Anasema hali kama hiyo ndio iliyopo kwa wafanyabiashara wa Kenya wanaofika Tarime, Musoma, Bunda, Simiyu, Mwanza na maeneo mengine ya ukanda wa Ziwa Viktoria kufanya biashara pasipo kubughudhiwa.

Masatu anasema baada ya kauli ya Mbunge Njagua, licha ya kutopewa nafasi kubwa katika uhusiano huo, iliibua hofu miongoni mwao kwa kuhisi kwamba huenda wakajitokeza watu wenye nia ovu, wakawajeruhi kwa kisingizio cha kuhamasishwa na mbunge huyo.

Agnes Benedict, mfanyabiashara wa mazao ya chakula na viungo jijini Mwanza, anasema amekuwa akilima katika ukanda wa Magharibi mwa Kenya na bonde la ufa kwa miaka mingi, kisha mazao ama viungo anavyovuna kuvisafirisha hadi jijini humo penye soko la uhakika.

"Mie nimelima sana mazao viazi mviringo na karoti kwenye maeneo yakiwamo ya kaunti za Nakuru na Naivasha, lakini sijawahi kupata shida yoyote kutoka kwa Wakenya, sasa kauli ya Mbunge huyu ilitushangaza na kutushtua sana," anasema.

Wafanyabiashara hao ni miongoni mwa wanaoizungumzia ziara ya Rais Kenyatta nchini Tanzania kuwa ni yenye manufaa na itakayorejesha hali ya amani na kuaminiana kabla ya kutolewa kwa hamasa ya Njagua.

Mwanaharakati ambaye pia ni mtaaluma wa masuala ya siasa na uchumi, Silas Chaka anasema licha ya kuwa shughuli nyingi za uchumi zinazowaunganisha raia wa mataifa hayo ni zilizo kwenye kiwango cha biashara ndogo na za kati, lakini zinachangia kukuza uhusiano na kuboresha maisha yao.

"Rais wa nchi hizi wanatoka kwenye nchi zenye uchumi mdogo, kwa hiyo hata mitaji yao ni midogo inayowafanya wengi wao washiriki shughuli za biashara ndogo na za kati, lakini zinazochochea ustawi wa maisha yao," anasema Chaka.

Chaka anasema licha ya hali hiyo, lakini zipo fursa kadhaa ambazo wananchi hao wanaweza kuzitumia katika kutanua wigo wa ushirikiano na uhusiano wao, kadri ya mabadiliko yanayotokea duniani.

"Inaweza ukafika wakati fursa za kushirikiana kati ya raia wa kawaida zikawa kubwa zaidi, hivyo hakuna sababu ya kuanza kuingiza 'chokochoko' zinazoleta kuwatenganisha wananchi wa EAC, badala yake zitumike kauli za kuwaunganisha," anasema Chaka.

> "Rais wa nchi hizi wanatoka kwenye nchi zenye uchumi mdogo, kwa hiyo hata mitaji yao ni midogo inayowafanya wengi wao washiriki shughuli za biashara ndogo na za kati, lakini zinazochochea ustawi wa maisha yao," anasema Chaka.

Akizungumzia ziara ya Rais Kenyatta, Rais Magufuli alisema imekuja wakati muafaka ambapo ushirikiano wa nchi za kikanda unapaswa kuboreshwa ili kuimarisha shughuli za kiuchumi kati yao.

Rais Magufuli alitoa mfano kuwa, miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa katika mazungumzo yake na Rais Kenyatta, ni kuiwezesha Kenya kuwa miongoni mwa wanunuzi wa gesi asilia inayozalishwa hapa nchini.

Naye Kenyatta alisema Kenya ilikuwa katika mpango wa kutaka kununua gesi kutoka 'mataifa ya mbali' lakini baada ya rasilimali kugundulika hapa nchini, imeona umuhimu wa kuwa miongoni mwa wateja wake.

### MZOZO WA KIUCHUMI

Licha ya kauli ya Njagua kuibua taharuki, Kenya na Tanzania zimewahi kupitia katika hali iliyotafsiriwa kutikisa uhusiano wa kiuchumi na kidiplomasia.

Kwa mfano, Septemba mwaka jana, Kenya iliweka kiwango kikubwa cha ushuru kwa maua na bidhaa nyingine zilizotoka Tanzania, ikielezwa kwamba ni 'kujibu mapigo' ya kuzuiliwa kwa bidhaa zilizotengenezwa za chocolate, barafu, biskuti na pipi kutoka Kenya kuingizwa nchini.

### KUDHIBITI UHALIFU

Ziara ya Kenyatta hapa nchini ilitumika pia kuimarisha mipango yenye lengo la kudhibiti vitendo vya uhalifu, kwa vile mataifa hayo yanatenganishwa na maeneo mengi ya mipaka ya nchi kavu na majini.

Marais wote wawili, wakaelezea utayari wao wa kushirikiana ili kila raia atakayepatikana na kosa la jinai ashtakiwe kwa mujibu wa sheria za nchi husika, kule atakashukiwa kufanya makosa.

"Kama Mtanzania atashukiwa kufanya makosa ya jinai huko Kenya, atawajibika kushtakiwa kwa mujibu wa sheria za Kenya, kama Mkenya atapatikana na shutuma kwa upande wetu, atashtakiwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania," akasema Rais Magufuli.

Yapo mambo mengi ya ushirikiano waliyoyajadili na viongozi hao, lakini kwa ujumla wake ni kwamba mambo yote mema yaliyojitokeza wakati wa ziara hiyo, yanapaswa kuwa mfano wa nyenzo ya kuimarisha ushirikiano kati ya nchi wanachama wa EAC.

**Mwandishi wa makala haya anapatikana kwa simu namba +255754691540 ama barua pepe: mgeta2000@yahoo.com.**

UCHAMBUZI

# Wananchi wachangamkie fursa hii ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi

• Ni ile ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura
• Na elimu ya mpigakura

**Na Enock Charles**

HIVI Karibuni Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilitangaza kuanza kwa shughuli ya Uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapigakura kwa kutumia teknolojia ya kielektroniki ambayo huchukua taarifa za kibaiolojia za mtu, kuanzia Julai mwaka huu.

Aidha, Tume hiyo ilitoa vibali kwa asasi 28 zikiwemo 24 kutoka Tanzania bara na 4 kutoka Zanzibar ili zitoe elimu ya mpigakura nchini, lengo likiwa kuhamasisha wananchi kujiandikisha na pia kutekeleza wajibu wao wa kikatiba wa kuchagua viongozi wanaowaona kuwa wanafaa kuwaongoza kwa kipindi kingine cha miaka mitano ijayo.

Katika kujiandaa na uboreshaji wa daftari hili, NEC iliendesha kazi ya uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapiga kura nchi nzima ili kuona kama vituo hivyo bado vina hadhi.

Kwamba na kama bado vina hadhi ya kuwa vituo vya kuandikisha wapigakura kwa mujibu wa sheria na vilevile iwapo kuna maeneo yanayohitaji kuongeza vituo.

Uhakiki wa vituo kwa upande wa Tanzania bara umesababisha kuongeza vituo vya kuandikisha wapigakura kutoka vituo 36,549 hadi vituo 37,407.

Aidha, kwa upande wa Zanzibar, vituo vimeongezeka kutoka 380 hadi vituo 407.

Kimsingi, elimu ya mpigakura ni ya muhimu kuelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu lakini pia Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge, madiwani na wawakilishi mwakani.

Elimu hii ni ya msingi kwa sababu inawawezesha wapigakura kutambua umuhimu wa kujiandikisha, kufahamu orodha ya wapigakura na namna ya kushiriki na kupigakura kwa usahihi.

Miongoni mwa majukumu ya NEC ni pamoja na kutoa elimu ya mpigakura, lakini kuratibu na kusimamia watu watakaokasimishwa kutoa elimu hiyo pamoja na wadau mbalimbali vikiwamo vyombo vya habari.

Kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, kifungu cha 4C, Sura ya 343, NEC imepewa jukumu la kutoa Elimu ya Mpigakura nchi nzima.

Sheria hiyo pia inatoa nafasi kwa Tume kukasimisha program ya utoaji wa elimu ya mpigakura kwa taasisi na asasi zenye nia ya kutoa elimu hiyo.

Elimu ya mpigakura ni sehemu tu katika elimu ya uraia ambayo kwa kawaida inapaswa kutolewa wakati wote.

Hata hivyo, katika kikao chake na asasi za kiraia, NEC ilitoa angalizo kwa asasi hizo kujikita katika elimu ya mpigakura badala ya elimu ya uraia na ikatoa onyo kwa asasi hizo kutojiingiza katika mrengo wowote wa kisiasa wakati wote wa utoaji wa elimu hiyo.

Elimu hii inapaswa kulenga katika suala la kuhamasisha wapigakura kushiriki kwenye uchaguzi kwa kuzingatia uimarishaji wa demokrasia na uhusiano kati ya uchaguzi na haki za binadamu.

Hii ni tofauti na elimu ya uraia ambayo imebeba maudhui mengi ikiwamo muundo wa Serikali, mamlaka zinazochaguliwa kushika dola, masuala ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, itikadi na mahusiano kati ya nchi na nchi nyingine.

Vyombo vya habari pia ni mdau muhimu katika masuala yahusuyo uchaguzi kwa kuwa ni kama mlinzi wa uchaguzi wa kidemokrasia na haki kwa kuweka uwazi wa yale yote yanayofanyika wakati, kabla na baada ya uchaguzi.



Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Athuman Kihamia.**PICHA: MTANDAO**

Ni muhimu kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika zoezi hili la uandikishaji wapigakura katika Daftari la Kudumu ili hatimaye kupata sifa ya kuweza kupigakura na kutimiza wajibu wa kikatiba wa kuchagua viongozi na tena viongozi bora na si bora viongozi.

Mara nyingi baadhi ya watu hugundua umuhimu wa kupigakura katikati ya kipindi cha kampeni, kipindi ambacho hakuna tena fursa ya kujiandikisha na uwezo wa kuamua ni nani awe kiongozi hubakia kwa wale tu walio na kadi za kupigiakura, almaarufu kama 'kichinjio.'

Ikiwa mtu hakujitokeza wakati wa zoezi la kujiandikisha, matokeo yake ni kuishia kulalamika tu baada ya viongozi kuchaguliwa na watu wengine, jambo ambalo halina msaada wowote.

Halina msaada wowote kwa kuwa tayari viongozi watakuwa wamechaguliwa na itakuwa ni wakati wao kutekeleza wajibu wao wa kuwatumikia wananchi kama viongozi halali.

> Hii ni tofauti na elimu ya uraia ambayo imebeba maudhui mengi ikiwamo muundo wa Serikali, mamlaka zinazochaguliwa kushika dola, masuala ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, itikadi na mahusiano kati ya nchi na nchi nyingine.

Imekuwa ni kawaida nchini kwa baadhi ya watu kudharau shughuli ya kujiandikisha na kupigakura hivyo wengi kubaki na manung'uniko pindi viongozi wanapokuwa wamekwisha kuchaguliwa wakati hawawakubali.

Baadhi ya watu hudiriki kusema kuwa siasa haiwahusu na hivyo kususia mchakato mzima wa kidemokrasia wa kuchagua viongozi .

Ili kujiepusha na manung'uniko hapo baadaye ni vyema kila raia mwenye sifa akashiriki katika mchakato wa kidemokrasia wa kuchagua viongozi, hata kama atakayemchagua kwa bahati mbaya akashindwa.

Kwamba walau katika mazingira haya atakuwa na amani ya moyo kwa kushiriki kutimiza haki na wajibu wake wa kikatiba wa kuchagua viongozi.

Vinginevyo atakuwa ni mtu wa kuishia kulalamika tu kwamba kiongozi yule na yule hafai, japokuwa sasa ndio watakao kuwa na jukumu la kuongoza na kuamua mambo mengi na ya muhimu yanayohusu maisha yake na ya wengine.

UCHAMBUZI

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-4

**Inatoka Uk. 13**

na leo hii tunakuletea sehemu ya nne ya mfululizo huu inayoanza na Sura ya 4. Fuatilia ….

**SURA YA NNE**

**SUALA LA MUUNDO WA MUUNGANO**

**4.1.** Usuli

Tumekwishakuona kwamba, muundo wa 'Serikali mbili' uliwekwa na Mkataba wenyewe wa Makubaliano ya Muungano, na kufafanuliwa zaidi na sheria ya "The interim Constitution of the United Republic of Tanganyika and Zanzibar" iliyotangazwa tarehe 1 Mei, 1964, na hatimaye kuingizwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977.

**4.2.** Mjadala kuhusu muundo huu wa 'Serikali mbili'

Mjadala kuhusu muundo huu wa 'Serikali mbili' umekuwa ukiendelea kwa muda mrefu tangu ulipowekwa katika Katiba. Na husiusan, katika miaka ya hivi karibuni, watu wengi walishuhudia jinsi mjadala ulivyokuwa katika Bunge Maalum la Katiba lililofanyika mwaka 2004 kwa lengo la kutengeneza Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ambapo karibu muda wote ulitumika katika malumbano baina ya Wajumbe wa Bunge hilo wanaotaka kuendelea na muundo wa Muungano wa 'Serikali mbili;' na wale wanaotaka mabadiliko ya kwenda kwenye muundo wa 'Serikali tatu.' Kwa kifupi, historia ya mjadala huu ni kama ifuatavyo:

**4.2.1.** Chanzo na Sababu za Muundo wa Serikali Mbili na Matumaini ya baadaye.

Maelezo ya Mwalimu Nyerere mwenyewe yanasema hivi:

"Hatukutunga mfumo uliopo kama wapumbavu. Tulitazama hali yetu halisi ilivyokuwa na tukatunga mfumo uliotufaa zaidi katika hali hiyo."

Maelezo hayo yamo katika makala maalum iliyoandikwa na Mwalimu Nyerere kwa ajili ya kueleza mantiki iliyotumika katika kufanya uamuzi wa kuwa na muundo wa Serikali mbili. Makala hiyo ilikuwa na kichwa cha habari kisemacho, "Asili ya Muungano wa Serikali Mbili" ambamo Mwalimu alitoa ufafanuzi kama ifuatavyo:

"Nchi mbili zinapoungana na kuwa nchi moja, mifumo ya kawaida ya muundo wa Serikali huwa ni miwili: ama muundo wa Serikali Moja; au Shirikisho la Serikali Tatu. Kwa mfumo wa kwanza (wa Serikali moja) kila nchi itafuta Serikali yake iliyokuwapo, na nchi mpya inayozaliwa itakuwa ni nchi moja yenye Serikali moja.

Katika mfumo wa pili (wa Shirikisho), kila nchi itajivua madaraka fulani ambayo yatakabidhiwa kwa Serikali ya Shirikisho. Lakini, itaendelea kuwa na Serikali yake itakayoshughulikia mambo yale yaliyobaki. Mambo yatakayokabidhiwa kwa Serikali ya Shirikisho ni yale ambayo yakibaki katika nchi zilizoungana, basi, kwa kweli nchi hizo zitakuwa hazikuungana kuwa nchi moja, bali zitaendelea kuwa nchi mbili zenye ushirikiano mkubwa katika mambo fulanifulani.

> "Mzee Karume alikuwa ni mtu jasiri sana. Hakuwa na woga.Ukitaka kugawanya sifa baina yake na mimi katika juhudi za kuleta Muungano huu, Mzee Karume anastahili kupewa sehemu kubwa zaidi ya sifa hizo. Katika kujibu swali la nini maoni yake kuhusu muundo wa Muungano, Mzee Karume alitamka bila kusita kwamba, maoni yake yeye ni Muungano wa nchi moja na Serikali moja. Mwalimu wewe utakuwa Rais na mimi Makamu wako."



Mwalimu Julius Nyerere (kushoto) akiwa na Abeid Karume. **PICHA: MTANDAO**

Nchi za Afrika Mashariki zilikuwa katika hali kama hiyo kabla ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Zilikuwa ni nchi tatu zenye ushirikiano mkubwa, lakini, hazikuwa nchi tatu zilizoungana kuwa nchi moja yenye muundo wa Shirikisho.

Shirikisho halisi la nchi mbili litakuwa ni nchi moja yenye Serikali tatu, ambazo ni Serikali ya Shirikisho na Serikali mbili za awali zilizoungana kuzaa nchi moja.

Tanganyika na Zanzibar zilipoamua kuungana na kuwa nchi moja, tungeweza kufuata mojawapo ya mifumo hiyo ya kawaida. Lakini, tulishindwa kufanya hivyo kwa sababu ya udogo wa Zanzibar na ukubwa wa Tanganyika. Zanzibar wakati huo ilikuwa na watu laki tatu (300,000); wakati Tanganyika ilikuwa na watu milioni kumi na mbili (12,000,000). Muungano wa Serikali moja ungefanya ionekane kuwa, Tanganyika imeimeza Zanzibar. Tulikuwa tunapigania Uhuru na Umoja wa Afrika. Kwahiyo, hatukutaka tudhaniwe, hata kwa makosa, kwamba, tumeanzisha ubeberu mpya!

Kwa sababu hiyo, mimi nilipinga mfumo wa Serikali moja. Lakini, hatukutaka kwenda kwenye Shirikisho la Serikali tatu kwa sababu mfumo huo ungekuwa ni wa gharama kubwa mno kwa Tanganyika. Katika mfumo huo, Zanzibar ingeendesha Serikali yake, na pia, kuchangia gharama za kuendesha Serikali ya Shirikisho.Tanganyika pia, ingefanya hivyohivyo. Lakini, ni dhahiri kwamba, mchango wa Tanganyika ndio hasa ungeendesha Serikali ya Shirikisho, kwani Tanganyika ingeendesha Serikali yake ya watu milioni 12,000,000, na pia ndiyo ingetoa sehemu kubwa ya kuendesha Shirikisho la watu milioni 12,300,000.

Ni watu wanaofikiri kwa ndimi zao wanaodhani kuwa, gharama ya Serikali yoyote kati ya hizo ingekuwa ndogo. Gharama ya kuendesha Serikali ya Tanganyika, isingekuwa ndogo, na wala gharama ya kuendesha Serikali ya Shirikisho isingekuwa ndogo. Na gharama zote hizo kwa kweli zingebebwa na Tanganyika.

Kwahiyo, ilitupasa tujiulize kwa nini tunataka kuibebesha Tanganyika gharama zote hizo? Hivi tuna hofu kwamba, Tanganyika bila kuwa na Serikali yake, itaonekana kuwa imemezwa na Zanzibar? Hofu yetu ilikuwa ni kwamba, kwa kuwa tukiwa na Serikali moja, Tanganyika itaonekana kuwa imeimeza Zanzibar, basi, ni vema tutafute muundo ambao utaiondolea Zanzibar hofu hii ya kumezwa, lakini, bila kuibebesha Tanganyika mzigo wa kuendesha Serikali mbili zenye uzito unaolingana.

Hivyo ndivyo tulivyofanya, na hiyo ndiyo asili ya muundo wetu wa Serikali mbili. Hatukutunga mfumo uliopo kama wapumbavu. Tulitazama hali yetu halisi ilivyokuwa, na tukabuni mfumo uliotufaa zaidi katika hali hiyo."

Tutarejea baadaye kuzungumzia mjadala ambao umekuwa ukiibuliwa mara kwa mara, wa kujaribu kubadilisha muundo huu wa Serikali mbili. Lakini, kwanza tuzingatie mambo muhimu yaliyomo katika maelezo hayo ya Mwalimu Nyerere, ambayo ni haya yafuatayo:

- Katika hali ya kawaida nchi mbili zinapoungana, muundo wake unakuwa ama ni wa Serikali moja; au wa Serikali mbili. (hiyo ndiyo miundo ya kawaida)
- Kwamba, muundo wetu wa Serikali mbili ulitokana na sababu maalum, ambazo amezieleza vizuri (yaani, huu haukuwa ni muundo wa kawaida).
- Kwamba, kulikuwa na matumaini kuwa, hapo baadaye, tutarejea kwenye muundo (wa kawaida) wa serikali moja; wakati sababu hizo maalum zitakapokuwa zimeondoka.

**4.2.2.** Matumaini ya baadaye yalikuwa ni kurejea Kwenye Muundo wa serikali moja

Baadhi ya kauli za Mwalimu Nyerere na baadhi ya kauli za Rais Karume, zinaonyesha dhahiri kwamba, walikuwa na matumaini makubwa kuwa hapo baadaye, Muungano wetu ungeondoka katika mfumo wa Serikali mbili, na kuingia katika mfumo (wa kawaida) wa Serikali moja. Matumaini hayo yanajidhihirisha katika matukio matatu yafuatayo:

**(A)**Kauli ya Rais Abeid Karume

Kauli husika ya Rais Karume ilinukuliwa na Rais Nyerere katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM uliofanyika Dodoma mwezi Januari 1984. Mwalimu Nyerere alinukuliwa na kauli hiyo alipokuwa akitoa maelezo kuhusu sehemu ya mazungumzo yake na Rais Karume juu ya kuanzishwa kwa muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Mwalimu alisema hivi:

"Mzee Karume alikuwa ni mtu jasiri sana. Hakuwa na woga.Ukitaka kugawanya sifa baina yake na mimi katika juhudi za kuleta Muungano huu, Mzee Karume anastahili kupewa sehemu kubwa zaidi ya sifa hizo. Katika kujibu swali la nini maoni yake kuhusu muundo wa Muungano, Mzee Karume alitamka bila kusita kwamba, maoni yake yeye ni Muungano wa nchi moja na Serikali moja. Mwalimu wewe utakuwa Rais na mimi Makamu wako."

Nukuu hiyo inaonesha kwamba, Rais Karume alikuwa na wazo la Serikali moja; na kwamba, ni Mwalimu Nyerere aliyekataa wazo hilo, kutokana na hofu ya kuonekana kuwa Zanzibar imemezwa na Tanganyika. Lakini, sababu yake ya kukataa, pia inaonesha kwamba, kauli hiyo ya Mzee Karume ilimpa Mwalimu Nyerere Matumaini ya hapo baadaye, hofu ya Zanzibar kumezwa ikishaondoka, itawezekana kurudi kwenye muundo wa Serikali moja.

**(B)** Maudhui ya Hati ya Mkataba wa Muungano

Hati ya Mkataba wa Makubaliano ya Muungano (Articles of Union), ilisema wazi kwamba, ukiondoa kifungu chake cha kwanza, vifungu vyake vingine vyote vilikusudiwa kutumika katika kipindi cha mpito tu (Interim period). Kifungu cha kwanza hakikuwekwa katika mfumo wa mpito kwa sababu ndicho kilichotamka kuundwa kwa Muungano wenyewe, kwa hiyo, kifungu hicho kilikuwa ni cha kudumu.

'Kipindi cha mpito' kiliainishwa kuwa ni hadi hapo Katiba ya Kudumu ya Jamhuri ya Muungano huu itakapokuwa imetungwa ndani ya mwaka mmoja kuanzia siku ambapo Muungano ulizaliwa, yaani tarehe 26 Aprili, 1964.

Kifungu kilichoweka muundo wa Serikali mbili kilikuwa ni kifungu cha (iv), ambacho pia, kilitamka kuwa katika kipindi hicho cha mpito, Katiba ya Tanganyika ndiyo itatumika kama Katiba ya muda ya Jamhuri ya Muungano baada ya kufanyiwa marekebisho kadhaa ambayo yalitajwa.

**ITAENDELEA WIKI IJAYO**



Rais wa Misri, Abdel Fattah al-Sissi.**PICHA: MTANDAO**

## Ukanda huru wa biashara Barani Afrika wazinduliwa

VIONGOZI wa Afrika wamezindua mpango wa bara hilo kuwa kanda ya biashara huru, ambao iwapo utatekelezwa kwa mafanikio utawaunganisha watu bilioni 1.3 barani humo.

Mkataba huo pia unatarajiwa kutengeneza kundi la kanda ya kiuchumi yenye thamani ya kiasi cha dola trilioni 3.4, na kuwa mwanzo mpya wa enzi ya maendeleo kwenye bara hilo.

Baada ya miaka minne ya mazungumzo, hatimaye makubaliano ya kuanzishwa kwa ukanda huru wa kibiashara unaojumuisha mataifa 55 ya Afrika yalifikiwa mwezi Machi.

Hatua ya kufungua njia ya kuanzishwa kwa ukanda huo kwenye mkutano wa kilele wa Umoja wa Afrika (AU) ilifanyika nchini Niger, ambako Ghana ilitangazwa kuwa mwenyeji wa makao makuu wa Umoja huo na majadiliano yalifanyika juu ya vipi makubaliano hayo yatafanya kazi.

Inatarajiwa chini ya mkataba huo ujulikanao kama AfCFTA, na ambao ni mkubwa kabisa tangu kulipoanzishwa mkataba wa biashara huru wa kimataifa mwaka 1994, utasaidia kuibua na kuimarisha ushirikiano wa kibiashara, mnyororo wa usambazaji bidhaa na utaalamu miongoni mwa bara hilo.

Rais wa Misri na Mwenyekiti wa AU, Abdel Fattah al-Sissi amesifu hatua hiyo aliyoitaja ni mwanzo mzuri.

Rais al-Sissi na mwenyekiti wa tume ya umoja huo Moussa Faki Mahamat, walikuwa miongoni mwa waliozinduwa rasmi mkataba huo.

"Tuko katika njia nzuri kuelekea hali bora ya baadaye… kuazishwa kwa ukanda huu wa biashara huru kunafungua dirisha jipya la maendeleo na ufanisi badala ya mkwamo wa kiuchumi pamoja na mizozo," anasema Rais al-Sissi.

Anaongeza kuwa macho ya ulimwengu sasa yanageukia Afrika.

Wachumi wanaonya kuhusu urasimu wa mipakani unaoweza kuzuia utekelezwaji wa mkataba.

Kulingana na wanauchumi, Afrika bado inakabiliwa na changamoto kubwa, ambazo ni pamoja na ubovu wa barabara zinazounganisha mataifa ya bara hilo, mizozo katika maeneo mengi, urasimu uliopitiliza wa mipakani na rushwa ndogondogo, ambavyo kwa pamoja vinarudisha nyuma ukuaji na utangamano.

Wajumbe kwenye mkutano huo wa 12 usio wa kawaida wa kilele wamekubaliana kuondoa ushuru kwenye bidhaa nyingi ili kuongeza biashara baina ya mataifa kwa kati ya asilimia 12 hadi 25 katika kipindi cha kati.

Hata hivyo, kulingana na makadirio ya Shirika la Fedha Duniani (IMF) hiyo ingeongeza kwa zaidi ya mara mbili, iwapo changamoto hizo zingekabiliwa vilivyo.

Katika ripoti yake ya mwezi Mei, IMF imeeleza umuhimu wa ukanda wa biashara huru kwenye mabadiliko ya kiuchumi na kusema kwa kiasi kikubwa umechangia kuimarika kwa ukuaji barani Ulaya na Amerika Kaskazini.

Hata hivyo, imeonya kwamba kuondoshwa kwa ushuru pekee haitoshi.

Eritrea ambayo ndiyo nchi pekee ambayo haijasaini makubaliano hayo, imesema itazingatia kusaini makubaliano hayo.

AU inakadiria kwamba makubaliano hayo yanayoondoa ushuru baina ya mataifa hayo, yatachangia kuimarika kwa biashara ya ndani kwa asilimia 60 ifikapo mwaka 2022. DW

# Ujerumani yapata kiwewe Kansela Merkel kutetemeka mara mbili

Na Nimi Mweta

WATAZAMAJI wa televisheni wamepata kigugumizi cha aina yake baada ya Kansela (Waziri Mkuu) Angela Merkel, kutetemeka hadharani mara mbili mfululizo kwa njia inayoleta wasiwasi wa kina kuhusu afya yake.

Maswali yamefurika chanzo cha hali hiyo, kama ni hali yake ya afya, au kama ni wasiwasi kuhusu kinachoendelea nchini, au ni kielelezo cha mkanganyiko uliopo katika mwelekeo wa Ujerumani na Ulaya kwa jumla katika mahusiano yao na mataifa shindani ya Marekani, China na Russia.

Ilielekea tatizo hilo sasa linamshinda Kansela Merkel na kuanza kuiathiri afya yake kwa hisia kuwa Ujerumani haina uwezo wa kufuata mwelekeo huru, ifaulu.

Inaelekea kuwa hali ya Kansela Merkel haikuwa inaonyesha udhaifu huo moja kwa moja, hivyo matukio ya kutetemeka kwa nguvu hadharani mara mbili ni jambo lisilotazamiwa, na hivyo kuleta kihoro kuwa anaweza kuondoka madarakani mapema kuliko inavyotazamiwa.

xxx

Bado kuna ngwe ya kutafuta warithi wa viongozi wa sasa wa Umoja wa Ulaya (EU) ambako mvutano wa wazi kati ya nchi za kiliberali za Ulaya Magharibi na za mrengo wa kizalendo au kitaifa huko Ulaya Mashariki kuhusu wanaofaa kuongoza unaendelea.

Njia za kutatua migogoro ambazo Kansela Merkel amezoea zinaanza kupwaya, kama ilivyokuwa nchini Ufaransa wakati wa maandamano ya Vikoti vya Njano, harakati ambayo inaendena na uzalendo mkali unaoshika kasi barani Ulaya.

Cha kushangaza ni kuwa kutetema hadharani kwa Kansela Merkel hakukusababisha mjadala wa siasa kwa haraka na badala yake ni mshtuko na hisia za huruma kutoka pande zote nchini humo, makundi tofauti ya jamii yakihoji kama Kansela ametendewa haki katika kazi yake, au imekuwa ngumu mno.

Msemaji wa ofisi ya Kansela Merkel ambaye anafikia umri wa miaka 65 wiki mbili zijazo (Julai 17) alisema mwishoni mwa wiki kuwa waziri mkuu ana afya nzuri na anafanya kazi zake kama kawaida.

Kiongozi wa chama cha kimazingira (Green Party) Annalena Baerbock aliomba radhi katika ukurasa wake wa twitter kwa kudai kuwa kutetemeka kwa Kansela Merkel huenda kumesababishwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Ujerumani ina joto kali sana mwaka huu.

Baerbock alisema katika mkutano na waandishi wa habari kutambulisha mpango wa kulinda hali ya hewa isiharibike zaidi, kuwa 'unaona hali hii ya joto – tunaona kutoka kwa Kansela kuwa hali hii ya kiangazi imeleta madhara ya kiafya.'

Kiongozi huyo mwanamazingira pia alitaja safari aliyofanya Iraq ambako viwango joto vimefikia nyuzi 48 Celsius, akiongeza kuwa endapo joto la aina hiyo litafika Ujerumani, mtu yeyote akikaa kwenye jua kwa saa nzima ataanza kutetemeka.

'Joto halichelei makansela vile vile,' aliongea mwanamazingira huyo, ikaonekana kama mzaha.

Ila alilenga bila shaka kuwafikia wapiga kura na raia kwa jumla kuona athari hizo za kiafya kwa Kansela Merkel kuwa kweli zina uhusiano na hali ya hewa, licha ya kuwa haikusemwa hivyo na daktari yeyote, na si hali ambayo imemsumbua Merkel kivile, ni kama ni mshtuko wa kupita.

Baadhi walitaka wazungumzaji wamwache Kansela Merkel aendelee na shughuli zake, wakisema kuwa akitaka kuongea neno lolote kuhusu tatizo hilo ataongea, na akiona hakuna haja ya kufafanua lolote basi ataliachia hapo.

Baadhi walikumbusha kuwa kiongozi huyo wa Ujerumani mara ya mwisho alionekana kuwa dhaifu hadharani miaka mitano iliyopita, na kwa maana hiyo afya yake imekuwa nzuri kwa muda mrefu, na haileti wasiwasi wowote.



Kansela Angela Merkel wa Ujerumani (kushoto), akiwa na Rais Donald Trump wa Marekani. **PICHA: MTANDAO**

Hata hivyo, juhudi hizo za kuonyesha kuwa kila kitu kiko sawa hazikuzuia mjadala kuanza kuhusu wanasiasa wa chama chake cha Christian Democratic Union (CDU) cha mrengo wa kulia wanaoweza kuchukua nafasi yake, kama ambavyo mwenzake wa Uingereza Theresa May anarithiwa hivi karibuni.

Uchovu wa Kansela Merkel kwa upande mmoja ulionekana kuhusika na kutokutaka kuwepo katika mkutano wa G20 nchi zenye uchumi mkubwa duniani kwani katika mikutano iliyopita aliwahi kueleza kuwa ni kama alifuata tu 'livu' nchini Argentina, mkutano uliofanyika Buenos Aires.

Alisikika akieleza kuwa alifurahi kumwachia waziri wake wa masuala ya uchumi aendelee na vikao hiyo alivyoviona visivyo na tija, kurembaremba tu maneno, na baadhi walisema kuwa hasa alikuwa anamkwepa Rais Xi Jinping wa China – ila naye hakuwa mkutanoni wakati huo.

Alitumia muda wake katika bustani za hoteli, ambako inaelekea alikuwa na mazungumzo ya hapa na pale.

Kwa undani zaidi, uhusiano mbaya kati ya Ujerumani na Marekani kipindi hiki cha utawala wa Rais Donald Trump kunaweza kumpa wasiwasi Kansela Merkel kuhusu mwelekeo mzima wa kile anachosimamia kuhusu umoja wa kujihami wa NATO pamoja na mfumo wa biashara huru duniani.

Rais Trump amepinga Ujerumani kuingia mkataba wa kupata asilimia 70 ya mahitaji yake ya gesi kutoka Russia (mshindani mkuu katika NATO na pia mwingiliaji wa mifumo ya mawasilianao na hata uchaguzi nchi za Ulaya na Marekani.

Ni kuleta serikali za kizalendo ili zifute mifumo kama Umoja wa Ulaya, NATO, n.k.)

Isitoshe, Kansela Merkel hana raha kuwa biashara kati ya Ujerumani na Iran imeporomoka, kwani kampuni za Ujerumani zinachelea vikwazo vya Marekani endapo zinathibitika kufanya biashara nchini Iran, zijifunge kwa biashara na Marekani.

> Alisikika akieleza kuwa alifurahi kumwachia waziri wake wa masuala ya uchumi aendelee na vikao hiyo alivyoviona visivyo na tija, kurembaremba tu maneno, na baadhi walisema kuwa hasa alikuwa anamkwepa Rais Xi Jinping wa China – ila naye hakuwa mkutanoni wakati huo.

Baadhi nchini Ujerumani walikuwa wameanza kuweka nukta katika utawala wa Kansela Merkel ambao umedumu miaka 14, kwani kipindi hicho kimekuwa chenye misukosuko mingi na hivyo amechoka.

Lakini wengi kati ya wachunguzi wanaona kuwa ujio wa Rais Trump umeongeza joto la kisiasa kwa uongozi wake.

Inakuwa kana kwamba Ujerumani inatakiwa tu ifuate maelekezo kutoka Marekani kwa mfano kuhusu mahusiano ya kibiashara na Russia, na hata kulazimika kuondoa biashara na Iran kwa sababu Marekani inataka kumalizana na utawala huo unaowasha mioto kote Mashariki ya Kati.

Ujerumani haina nafasi kupanga sera zake yenyewe, na ziheshimiwe kimataifa.

Baadhi ya vyombo vya habari vilikumbusha kuwa tangu miezi ya awali mwaka jana, Mei 2018 kulikuwa na kila dalili kuwa Kansela Merkel alikuwa amechoshwa kabisa na siasa za Rais Trump, hivyo akafanya ziara China na Russia labda kuweka mambo sawa na kuweka wazi baadhi ya maeneo ambako Ujerumani iko tayari kufuata njia yake yenyewe bila kuisikiliza Marekani.

Mojawapo ni kutaka Iran iendelee kuheshimu mkataba wa kutokutengeneza silaha za nyuklia (kutoongeza kiwango cha kurutubisha madini ya uranium au mengine hata kama Marekani imetosa rasmi mkataba wa kimataifa wa mwaka 2015.

Iran imekataa mpango huo na inataka Umoja wa Ulaya ulete mabadiliko katika vikwazo, jambo ambalo Marekani haitasikiliza.

Hatari ya vita inaongezeka katika eneo hilo na Kansela Merkel anajua vyama vya kisiasa vya mrengo wa kulia, kifashisti, vitapinga kupokea wakimbizi hata kuwe na maafa kiasi gani.

Kansela Merkel hana njia ya kuboresha kinachotokea duniani, kulinda mikataba au kupokea wakimbizi.

UCHAMBUZI

# Mwenge wa Uhuru 2019, hamasa kwa uchaguzi wa serikali za mitaa

Na Mwalimu Reubeni Lumbagala

MWENGE wa Uhuru ni miongoni mwa alama zinazolitambulisha Taifa letu kote duniani.

Ni ishara ya kuonyesha nchi yetu iko huru na kuleta nuru pia matumaini kwa Watanzania waliokuwa wamechoshwa na maisha ya ukoloni yaliyojaa kila aina ya mateso.

Mwaka huu, Mbio za Mwenge zilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan katika uwanja wa Mlowo mkoani Songwe.

Katika uzinduzi huo, Mama Samia alitoa rai kwa jamii kutumia Mbio za Mwenge kumkumbuka na kumuenzi Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kupinga vitendo vya ufisadi, chuki, dhuluma, dharau, rushwa na maradhi.

Kauli mbiu ya Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2019 ni "Maji ni haki ya kila mtu. Tutunze vyanzo vyake na tukumbuke kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa." Makala haya yanaangazia kauli mbiu ya Mwenge wa Uhuru katika kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Uchaguzi ni fursa kwa wananchi kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na pia kuwachagua viongozi bora kwa ajili ya kushirikiana nao katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto katika maeneo yao wanayoishi.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Mzee Mkongea Ali na timu yake wanapokwenda kushiriki katika uzinduzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo, hupata nafasi ya kuongea na wananchi wa maeneo hayo kabla ya kuzindua miradi kama vile vituo vya afya, zahanati, madarasa, viwanda, ofisi za umma, miradi ya maji, umeme nk.

Kutokana na kauli mbiu ya mwaka huu, wananchi wanapata darasa la hamasa kuhusu umuhimu wa ushiriki wao katika kufanikisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mwenge wa Uhuru unatoa hamasa ya kila Mtanzania mwenye sifa zilizoainishwa katika kugombea nafasi mbalimbali ajitokeze kugombea kwani ni haki yao ya msingi kuwania nafasi za uongozi.

Sambamba na hilo, wananchi wanahamasishwa kujitokeza kwa kuwasikiliza wagombea wa nafasi za uongozi ili waweze kuwapima na hatimaye kuchagua viongozi wanaokidhi matarajio yao.

Njia pekee ya wananchi kupata viongozi bora ni kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi na kuwapigia kura wale wanaowafaa.

Wananchi hawatawapata viongozi bora kwa kususia kwenda kupigakura bali kujitokeza kupigakura.

Hivyo, hamasa inayotolewa na viongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu, itasaidia sana katika kufanikisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa wananchi kujitokeza kugombea na kupigakura.



Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan (kulia), akimkabidhi Mwenge kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa kwa mwaka 2019, Mzee Mkongea Ali kutoka Mjini Magharibi kuashiria kuanza kwa mbio za Mwenge wa Uhuru 2019. **PICHA: MTANDAO**

Aidha, Mbio za Mwenge wa Uhuru zinatoa elimu kwa wagombea kufanya kampeni za kistarabu katika kujenga hoja zao bila kuvunja sheria za uchaguzi na za nchi kwa ujumla wake.

Wagombea wawapo katika majukwaa ya kujinadi, hawapaswi kubezana bali kila mmoja ajikite katika hoja ambazo zitawashawishi wananchi kumchagua na hatimaye kupata ridhaa ya kuongoza wananchi kwa miaka mitano.

Wananchi wanazo kero mbalimbali ambazo wanataka kupata viongozi wa kuwasaidia katika kuzitafutia ufumbuzi wake.

Hivyo basi, wagombea watakaoelekeza nguvu zao katika kuwabeza wagombea na vyama vingine waelewe kuwa hawana nafasi, kwani wananchi wamepata elimu ya kutosha kupitia viongozi wa Mbio za Mwenge wanaoendelea na kazi ya kukimbiza katika mikoa yote hapa nchini.

> Uchaguzi ni fursa kwa wananchi kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na pia kuwachagua viongozi bora kwa ajili ya kushirikiana nao katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto katika maeneo yao wanayoishi.

Zama za wagombea kupiga porojo majukwaani zimepitwa na wakati.

Wananchi wanataka kusikia mgombea makini anayejibu kero zao kwa wakati.

Mwenge wa Uhuru unatoa rai kwa wananchi kuwapima wagombea bora ili kupata viongozi bora na hatimaye maendeleo ya uhakika kwa ustawi bora wa maisha ya wananchi.

Pia, Mwenge wa Uhuru unapiga vita suala la rushwa katika uchaguzi kwani rushwa ni adui wa kupata viongozi bora na makini kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Kwa jitihada za viongozi wa Mbio za Mwenge za kukemea rushwa katika jamii na katika uchaguzi, ni matumaini ya wengi kuwa wananchi hawatapokea rushwa wala zawadi kutoka kwa mgombea yeyote kwani maisha ya wananchi yana thamani kuliko vitu wala fedha zinazotolewa na wagombea wenye uchu wa kupata madaraka kwa kuwanunua wapigakura.

Wananchi wazingatie nasaha nzuri zilizotolewa na viongozi wa Mbio za Mwenge tunapoelekea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Kiu ya wananchi ya kupata maendeleo itaweza kufanikiwa kwa kupata viongozi bora. Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema; Ili nchi iweze kuendelea kimaendeleo inahitaji vitu vinne ambavyo ni; Watu, Ardhi, Siasa Safi na Uongozi Bora.

Uongozi bora unajengwa na viongozi bora na viongozi bora wanahitajika katika Serikali za Mitaa pia.

Wananchi tuchague viongozi bora katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huu, 2019. Tafakari

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilayani Kongwa, mkoani Dodoma.***
***Maoni: (+255) 764 666349.***

# Uingereza, China zahitilafiana mzozo wa kuhamisha watuhumiwa ukipamba moto

**Na Nimi Mweta**

UINGEREZA na China zimebadilishana maneno makali na hisia za dhihaka kuhusu hali ilivyo katika eneo maalum la Hong Kong, koloni la zamani ambalo Uingereza ililirudisha kwa China mwaka 1997.

Ilikuwa ni baada ya waandamanaji jijini Hong Kong kuvamia jengo la Baraza la Kutunga Sheria la Hong Kong, hatua ambayo iliikasirisha serikali ya China, huku Uingereza ikiitaka China kuheshimu mfumo wa 'nchi moja, mifumo miwili' na kuacha kuingiza Hong Kong kichwakichwa katika mfumo wa sheria za jinai wa Jamhuri ya Watu wa China.

Balozi wa China nchini Uingereza akajibu kuwa Uingereza siyo tu kuwa inaingilia mambo ya ndani ya Hong Kong, bali inawaunga mkono wahalifu waliohariibu mali za serikali.

Lugha ya China dhidi ya alichosema Waziri Mkuu Theresa May bungeni akielezea wasiwasi wake kuhusu juhudi za China kuweka eneo la Hong Kong katika utawala mmoja kupitia mabadiliko ya taratibu za kutumia endapo Mahakama za China zinamtaka mtu fulani wa Hong Kong kama mhalifu ilikuwa kali kuliko alivyowazungumzia waandamanaji Hong Kong.

Alifikia kiasi cha kusema kuwa matamshi ya May yalikuwa na chembe za 'ukoloni,' na Wizara ya Mambo ya Nje ya Uingereza ikamwita kwa mahojiano kuhusu alichokisema.

Ilikuwa ni ishara kuwa juhudi za China 'kuimeza' Hong Kong, zitaleta mvurugano.

Uhusiano kati ya Uingereza na China kuhusu Hong Kong haujawahi kuwa wa kupendeza, kwani eneo hilo ni kielelezo cha unyanyasaji wa China kihistoria, ila Waingereza walitumia udhaifu ndani ya jamii na dola ya zamani China, na siyo kwa kutumia mtutu peke yake.

Ni pamoja na vita vya miaka ya 1840 ambako Uingereza, ikiwa imejichimbia katika kituo cha kijeshi na koloni la Hong Kong iliingia vitani na Himaya ya China kutetea 'soko huria,' ambako Uingereza ilikuwa inauza bangi na dawa zingine za kulevya, na maofisa wa China wanalipa kwa fedha halisi (za shaba, fedha na dhahabu, siyo noti za karne hii iliyopita).

Himaya ya China ilifilisika hatua kwa hatua ikitoa hazina yake yote kununua bangi, heroin...

Ndiyo maana hadi sasa China ina uchumi unaosimamiwa na dola, na haitaki kusikia dhana kadhaa za uhuru kwani inakumbuka kwa machungu 'soko huria' la maharamia wa Uingereza lilileta madhara kiasi kwa himaya hiyo, dola asilia iliyosheheni utamaduni wake wa karne nyingi.

Ila kinachoonekana pia ni hali ya mkwamo wa matarajio ya China kuwa kadri muda unavyokwenda ndivyo Hong Kong itakuwa sehemu ya China kwa hatua kadhaa, na hapa na pale itabidi kulazimisha.



Maandamano dhidi ya sheria Hongkong yaliyosababisha majibizano kati ya Uingereza na China. **PICHA: MTANDAO**

Ambacho fikra hiyo inaelekea haikuwa imeelewa ni kuwa matarajio hayo yanashindana na matarajio ya demokrasia katika maeneo mengi na makundi makubwa tofauti ya jamii, wanaiona Hong Kong kama kielelezo cha wanachokitaka.

Viongozi wa chama tawala cha Kikomunisti nchini humo hawajalala usingizi hata kidogo kuhusu suala hilo, hivyo wanajua kuwa wakijaribu kulazimisha mfumo wa China ufuatwe Hong Kong, wanaweza wakavuna siyo tu machafuko jijini humo yanayoweza kuanza kuharibu nafasi ya Hong Kong katika biashara na masoko ya hisa ya kampuni Asia ya Mbali.

Inawezekana pia machafuko hayo yakaenea miji mingine mikubwa kwani katika vipindi vilivyotangulia, kwa mfano eneo la wazi la kufanyia mikutano na magwaride ya kijeshi la Tienanmen mwaka 1989, ambako harakati hiyo ilivunjwa kwa mtutu wa bunduki.

Kutokana na kutokuwapo kwa uhuru wa vyombo vya habari vya nchi za Magharibi kufuatilia kwa undani taarifa zinazotolewa na vyombo vya dola, haijulikani ni wangapi waliuawa.

Makisio yanatofautiana, baadhi ikiwa ni pamoja na serikali ya China walisema ni mamia kadhaa, lakini baadhi ya wachunguzi wa mataifa ya nje, wakitofautiana kulingana na mashirika yao ya utetezi wa wafungwa, uhuru wa vyombo vya habari au demokrasia, walisema waliokufa ni 10,000 na zaidi.

Kwa maana hiyo China itakuwa na tahadhari katika suala la Hong Kong, isipandikize mizizi ya uamsho kote nchini humo kwani hitaji la demokrasia si la Hong Kong peke yake. Wanaelewa hivyo; hawatumii nguvu.

Baadhi ya wachunguzi wa habari wanaona kuwa matazamio kuwa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, Boris Johnson, kuchukua wadhifa wa uwaziri mkuu kuelekea mwisho wa mwezi huu kunaashiria hali ngumu zaidi kwa China na baadhi ya marafiki zake, hasa Iran.

Kujitoa kwa Uingereza kutoka Umoja wa Ulaya (EU) hata kama hakuna mkataba rasmi na umoja huo ni kwa mpangilio gani wa forodha na maeneo mengine wanajitoa, kunatazamiwa kuiweka Uingereza karibu zaidi na utawala wa Rais Donald Trump nchini Marekani.

Hafichi kuchoshwa kwake na umoja huo ambao anahisi mifumo yake na mipangilio ya kufanya maamuzi inaendana mno na siasa za China kupenya kila mahali, tena bila kufanya mageuzi ya sera za uchumi nchini humo ili nchi za Magharibi zifanye biashara vyema China. Juhudi za China kuiambia Uingereza isiingilie masuala ya Hong Kong ni kutaka suala hilo libaki kama ajenda ya ndani ya China, inayomaanisha kuwa utawala wa Kikomunisti nchini humo uwe na kazi ya kuwaeleza wananchi iwe ni jijini Hong Kong au China yenyewe, nini kimetokea.

Uingereza inakuwa ni sauti ya ziada ya makundi ya waandamanaji, inadidimiza usikivu wa watu wa Hong Kong kwa kile utawala wa Hong Kong, ambao ni tiifu kwa Jamhuri ya Watu wa China, unachosema, na badala yake wasikie sauti zao wenyewe zikirudiwa kwa lafudhi ya ki-Malkia na viongozi wakuu nchini Uingereza.

Kama ilivyo jadi katika historia ya China, wimbi la uamsho limeteka hasa wanafunzi wa vyuo vikuu, ila majuzi ilifikia mahali wazazi wao, hasa kina mama, wakajiunga na maandamano kuwasaidia vijana wao katika suala hilo.

Katika mazingira hayo si rahisi kuwatenga, kuwarushia maneno ya kudakiza kuwa wameingiliwa na nguvu hii au ile kwani wanachosema kinaanza kukubalika kwa jamii yote ya Hong Kong isipokuwa wale wanaoshika nyadhifa kwa misingi ya utii, uzalendo kwa China kwa jumla kama jambo la msingi zaidi ya vipengele kadhaa au vyote vya demokrasia Hong Kong.

Ndicho ambacho hasa kinapiganiwa, kama Hong Kong ina mfumo wake au inaweza kupelekeshwa tu na serikali ya China.

Isitoshe, wimbi hili limeshika kasi katika miezi ya Mei na Juni, ambako katika historia ya China ndiyo miezi ya harakati kuu, kama May Fourth (movement) ya mwaka 1919 iliyopelekea hadi kuundwa kwa Chama cha Kikomunisti kwani kile cha kizalendo (Kuomintang) kilichohamishia maskani Taiwan mwaka 1949 baada ya mapinduzi kilionekana dhaifu mbele ya uvamizi wa Japan na ubeberu wa Uingereza ambao katu haukuwahi kuondoka, ukabakia Hong Kong baada ya China kugubikwa na mapinduzi, chini ya wimbo/kaulimbiu, 'The East is Red,' yaani Mashariki ya Mbali ni ya kimapinduzi.

Mwaka 1989 uamsho pia ulijikita miezi ya Mei na Juni, mauaji ya waandamanaji yakafanyika Juni 4, walipopandisha sanamu 'Statue of Liberty' ya Marekani uwanja mtukufu wa mapinduzi China, dola ikasema 'sasa basi.'

Kwa upande mwingine watu wa Hong Kong na makundi ya waandamanaji wanajua ni aina gani ya serikali wanajibizana nayo, hivyo wamepania kwani wanajua muswada kuhamishiwa watuhumiwa Bara utakuwa kifaa muhimu cha ukandamizaji wa uhuru wa mawasiliano na majumuiko ya kijamii.

Hata hivyo, inaelekea katika kupania huku walivuka mpaka kiasi fulani kwa kuruhusu vikundi vya wakereketwa kushambulia jengo la Baraza la Kutunga Sheria, ikiwa ni kielelezo cha usemi kuwa 'Hong Kong is not China' ambao utawala wa Kikomunisti unapata tabu kuuvumilia, na muda ukifika hawatasita katu kuubamiza kwa nguvu zote.

Tatizo ni kuwa wanafunzi wa Hong Kong wana wafuasi lukuki China kwenyewe, na endapo makosa ya kisiasa yatafanywa kwa 'kiherehere cha kipolisi,' italeta madhara.

Ila labda isemwe kuwa mwezeshaji halisi wa maandamano ya Hong Kong siyo Waziri Mkuu Theresa May ila Rais Donald Trump wa Marekani ambaye ameipelekea China vita ya kiuchumi iliyofaulu kwa kiasi kikubwa kuyumbisha uwezo wa kujiamini wa utawala wa Rais Xi Jinping.

Wakati thamani ya hisa za kampuni za China zinashuka katika masoko ya Shanghai, Guangzhou au Shenzhen, haitakuwa busara kwa China kutetemesha soko la mitaji la Hong Kong kwa kutaka tu kuwabamiza viongozi wa vikundi vya kidemokrasia eneo la Hong Kong.

Ni mwisho wa kujitanua kwa China kwa kutumia nyenzo zilizobuniwa na kusanifiwa na kiongozi mkuu wa pili Deng Xiaoping mwaka 1978/9 akiwa madarakani kufuatia kifo cha Mwenyekiti Mao mwaka 1976.

Ni kuingia katika mfumo wa kibepari duniani (baadaye ukaitwa utandawazi) kwa kutumia nguvu za kiuchumi za mfumo wa dola, na bila kubadilisha mfumo.



## Bosi mpya wa maji ateuliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amemteua Mhandisi Ndele Mengo kuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) kuziba nafasi ya Mhandisi Simon Shauri ambaye amepumzishwa.

Akizungumza juzi wakati wa makabidhiano ya Ofisi kati ya Mhandisi Shauri na Ndele, Ofisa Utumishi wa Mbeya- WSSA, Patal Patal alisema walipokea barua ya mabadiliko ya viongozi hao Juni 25, mwaka huu huku ikieleza kuwa uteuzi wa Mengo unaanza Juni 26.

Alisema Waziri Mbarawa aliamua kumpumzisha Mhandisi Shauri kwa sababu muda wake wa kutumikia Mamlaka hiyo umeisha na anaelekea kustaafu.

"Tunamshukuru mzee wetu Mhandisi Shauri kwa kazi kubwa aliyoifanyia Mamlaka yetu, ameitumikia kwa mafanikio makubwa tangu mwaka 2007 alipoteuliwa kuitumikia, sasa hivi Waziri amempumzisha, lakini ataendelea kushirikiana nasi mpaka atakapostaafu," alisema Patel.

Alisema Mhandisi Mengo ataendelea kutumikia nafasi hiyo mpaka atakapoteuliwa mtu mwingine wa kuziba nafasi hiyo na kwamba wanahitaji busara za Mhandisi Shauri ziendelee kwa ajili ya kuboresha mamlaka.

Akikabidhi Ofisi kwa mrithi wake, Mhandisi Shauri aliwashukuru watumishi wote wa Mbeya- WSSA pamoja na Bodi ya Mamlaka hiyo kwa ushirikiano waliompatia kwa madai kuwa walikuwa wanafanya kazi kwa ushirikiano.

Alimshauri mrithi wake kuhakikisha anasimamia vizuri mapato ya mamlaka hiyo ili kuhakikisha Mamlaka hiyo inafikia malengo ya kukusanya Sh.bilioni 1.6 kwa mwezi kama walivyosainishwa Mkataba na Wizara ya Maji.

Alisema awali walikuwa wanakusanya Sh. milioni 800 lakini mpaka anakabidhi ofisi Mamlaka hiyo inakusanya Sh.bilioni 1.1 na hivyo akamshauri Mengo kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato na kufikia lengo.

"Ipo mipango ambayo tulikuwa tumejiwekea ili kufikia lengo hilo, namuomba mkurugenzi wetu mpya aendelee kusimamia utekelezaji wa mipango yetu maana kwa sasa tunachechemea kidogo, tunatakiwa tujitahidi kufikia hiyo bilioni 1.6," alisema Mhandisi Shauri.

Kwa Upande wake Mhandisi Mengo ambaye kabla ya kuteuliwa alikuwa Meneja Ufundi wa Mamlaka hiyo, alimshukuru Waziri Mbarawa kwa kumwamini na kumteua kushika nafasi hiyo ya Kaimu Mkurugenzi.

# Familia ya askofu yamwangukia JPM

**Nebart Msokwa,** MBEYA

FAMILIA ya Askofu Mullilege Kameka na waumini wa Kanisa la House of Player katika Kijiji cha Maenje wilayani Mbozi, wamemuomba Rais John Magufuli kuingilia kati hatma ya askofu huyo ambaye anashikiliwa na Jeshi la Polisi.

Anashikiliwa jijini Dar es Salaam kwa zaidi ya miezi saba sasa bila kutoa maelezo ya aina yoyote kwa familia.

Baba mzazi wa Askofu Kameka, Mzee Ambindwile Kameka, alisema kuwa mwanae Askofu Kameka alikamatwa na Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam tangu Januari mwaka huu, akituhumiwa kuwa sio raia wa Tanzania.

Alisema baada ya kukamatwa alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ambako alishtakiwa kwa kuishi nchini kinyume cha sheria na kesi hiyo ikaendeshwa mahakamani hapo kwa uwazi.

Mzee Ambindwile alisema April mwaka huu mwanaye alishinda kesi hiyo na Mahakama ikathibitisha kuwa Askofu Kameka ni raia halali wa Tanzania na ikaamuru aachiwe huru.

**Tukienda kumsalimia pale Segerea haturuhusiwi kuonana naye, hili linatufanya tuwe na wasiwasi kama ni mzima na sababu za kushikiliwa kwake kwa muda mrefu bila kufikishwa mahakamani.**

Alisema hata hivyo, Polisi walimkamata tena na kumpeleka katika gereza la Segerea ambako wamemshikilia tangu aliposhinda kesi yake hadi sasa bila kutoa maelezo yoyote wala kumfikisha mahakamani.

"LAicha ya kushinda kesi yake aliyostakiwa kuwa sio Mtanzania, Polisi wanaendelea kumshikilia mwanangu bila ya sisi kama wanafamilia kupewa maelezo yoyote, hivyo namuomba Rais Magufuli aingilie kati anisaidie mwanagu aachiwe huru kwa sababu naamini anashikiliwa bila kosa lolote," alisema Mzee Ambindwile.

Mama mlezi wa Askofu huyo, Maria Nzunda, alisema kuwa wanafamilia wakienda kumtembelea Askofu Kameka wanazuiwa kuonana naye, lakini hawaelewi sababu za Polisi kuendelea kumweka mahabusu ndugu yao.

"Tukienda kumsalimia pale Segerea haturuhusiwi kuonana naye, hili linatufanya tuwe na wasiwasi kama ni mzima na sababu za kushikiliwa kwake kwa muda mrefu bila kufikishwa mahakamani," alisema Maria.

Mchungaji Simon Mwaipungu ambaye ni msaidizi wa Askofu Kameka, alisema wachungaji wa kanisa hilo walichukua hatua mbalimbali za kupata msaada kwa viongozi wa juu wa Serikali bila mafanikio.

Alisema jopo la wachungaji liliondoka kwenda Dodoma kuonana na Waziri Mkuu kumuomba msaada, lakini hawakufanikiwa kuonana naye baada ya kuwambiwa na wasaidizi wa ofisi yake kuwa hawana ahadi ya kuonana na Waziri Mkuu.

Alisema badala yake waliandika barua na kuziacha katika ofisi ya Waziri Mkuu, lakini hazijawahi kujibiwa hadi sasa.

Gazeti hili liliwasiliana kwa njia ya simu na Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, ambaye alikiri Jeshi la Polisi kumshikilia Askofu Kameka.

Hata hivyo, Mambosasa hakutaka kuzungumzia suala hilo kwa maelezo kuwa alikuwa nje ya ofisi na badala yake akamtaka mwandishi wa habari kuwasiliana naye wakati mwingine atakapokuwa ofisini.

"Siwezi kuzungumzia suala hili kwa sababu kwa sasa nipo nje ya ofisi, tuwasiliane baadaye kuanzia kesho nitakupa maelezo unayoyahitaji," alisema Mambosasa.



Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Mbeya (Mbeya- WSSA), Mhandisi Simon Shauri (kushoto), akimkabidhi baadhi ya nyaraka Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Ndele Mengo, katika makabidhiano jana. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Dk. Lwitiko Mwakalukwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Teku yatimiza masharti ya TCU udahili wanafunzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TUME ya vyuo vikuu nchini (TCU), imekiruhusu Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (Teku) kilichopo mkoani Mbeya kuendelea kudahili wanafunzi ngazi mbalimbali ya elimu kuanzia mwaka wa masomo 2019/2020 baada ya kuridhika na utekelezaji wa maelekezo ambayo kilipewa.

Chuo hicho kilisitishiwa kudahili wanafunzi tangu mwaka 2017 kutokana na upungufu mbalimbali uliyokuwapo chuoni hapo ikiwemo kuajiri wahadhiri wasiokuwa na sifa za kufundisha chuo kikuu kama miongozo inavyotaka.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Helmas Mwansoko, alisema jana kuwa chuo hicho kilikuwa na upungufu ukubwa wakati kinasitishiwa udahili na kwamba sasa wameshayashughulikia.

Alisema taratibu za vyuo vikuu zinataka viongozi watatu wa ngazi za juu za chuo wawe ni maprofesa, lakini wao walikuwa na viongozi ambao hawakuwa na sifa hiyo na kwamba chuo kizima kilikuwa na maprofesa wawili pekee.

Prof. Mwansoko alisema wameshafanya maboresho kwa kuajiri maprofesa watano wenye sifa, wahadhiri wandamizi sita na wahadhiri wasaidizi 30 pamoja na kuboresha baadhi ya maeneo ikiwamo kununua vitabu vya kutosha na kuajiri mkutubi mwenye sifa.

"Tulipokea barua ya kuruhusiwa kuendelea na udahili wa wanafunzi Juni 19, mwaka huu, na hii ilikuwa ni baada ya TCU kujiridhisha na utekelezaji wa maelekezo waliyotupa hivyo tunaishukuru sana Serikali na tunawakaribisha wanafunzi kuomba nafasi," alisema Prof. Mwansoko.

Aliishukuru Serikali namna inavyosimamia na kuhakikisha ubora wa elimu katika ngazi za vyuo vikuu na kwamba utaratibu huo wa kuvifungia vyuo visivyokuwa na sifa unasaidia kuwaamusha wamiliki wa vyuo hivyo.

Pamoja na neema ya kufunguliwa kwa chuo hicho pia lisema baadhi ya waliokuwa watumishi wa chuo hicho ambao walikuwa hawana sifa, wamepoteza vibarua vyao kwa kusitishiwa ajira. Aidha Prof. Mwansoko aliwataka Watanzania kuchangamkia fursa ya kufundisha lugha ya Kiswahili kwenye mataifa mbalimbali yaliyotangaza kuanza kufundisha Kiswahili kwenye shule zao kwa madai kuwa ni fursa ya ajira.

Aliyataja baadhi ya mataifa yaliyotangaza kuanza kufundisha Kiswahili kuwa ni Afrika Kusini, Namibia, Sudan Kusini, China na mataifa mengine.



HABARI DODOMA

# Neema kwa vijana wabunifu kilimo

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

WIZARA ya Kilimo imesema ipo tayari kufanya kazi na vijana wabunifu katika utekelezaji wa sera yake mpya ya kilimo nchini ambayo matumizi ya teknolojia yamepewa kipaumbele.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mathew Mtigumwe, alitoa kauli hiyo jana katika kikao maalum kilichoitishwa na wizara hiyo ili kupata ufahamu kuhusu mradi wa E-Kilimo Accelerator ambao unalenga kutafuta suluhu za teknolojia za kidijitali zinazosaidia kupambana na changamoto kwenye kilimo.

**Serikali inatamani kuona vijana wetu wakichangamkia fursa hizi haraka bila kuchelewa.**

Mradi huo wa E-Kilimo Accelerator umefadhiliwa na Ubalozi wa Denmark nchini na kuendeshwa na Shirika la Sahara Consulting la jijini Dar es Salaam.

Alisema ni wakati wa vijana kujikita zaidi katika ubunifu na kuonyesha vipaji vyao kwa kuwa kilimo ndiyo injini inayoweza kuifanya Tanzania kufikia azma yake ya kuwa na uchumi wa viwanda.

"Vijana ndiyo nguvu kazi na rasilimali yenye manufaa na faida kubwa kwa nchi hivyo wakiwa na teknolojia yenye maboresho na faida, hata taifa litapata matokeo chanya kwa kuwa utaalamu utakuwa umeingia mahali salama kwa watu wenye ujuzi na utaalamu," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara hiyo, Assery Obey, alisema serikali ingependa kuona ubunifu uliopatikana kupitia mradi huo unatumika ipasavyo.

"Serikali inatamani kuona vijana wetu wakichangamkia fursa hizi haraka bila kuchelewa," alisema Assery.

Naye, Mkurugenzi wa Shirika la Sahara Consulting, Adam Mbyallu, alisema ili kufikia maendeleo endelevu, ni lazima kila kijana ajihusishe na kilimo cha moja kwa moja.

Mbyallu alisema vijana kwa taaluma zao wanaweza wakabuni namna bora ya kusaidia mnyororo wa kilimo kupitia bunifu na teknolojia zao.



Mwenyekiti wa Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), Mkoa wa Dodoma, Justous Silungwe, akizungumza katika kikao cha wajumbe wa Baraza la Mkoa huo, juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Watakiwa kuchagua viongozi watii

Na Augusta Njoji, MPWAPWA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewataka wakazi wa Dodoma kutumia uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika mwishoni mwa mwaka huu kuchagua viongozi watakaotii serikali iliyopo madarakani.

Dk. Mahenge alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kikazi wilayani Mpwapwa ya kukagua ujenzi wa miradi ya maendeleo na kuzungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara.

Alisema moja ya kitu kinachochelewesha wananchi katika maendeleo ni kuwa na viongozi wabishi wasiotii serikali inayotawala hivyo wawe makini katika uchaguzi huo.

"Novemba mwaka huu tuna uchaguzi wa serikali za mitaa moja ya vitu vinavyowachelewesha kwenye maendeleo ni kuwa na viongozi wabishi kwenye maendeleo," alisema.

Vile vile, alisema wakiwa na viongozi wanaobishana na serikali inayotawala watachelewa kimaendeleo.

"Miradi hii mnayoipata inavutwa na mbunge sasa kukiwa na wabishi mradi unahama unaenda sehemu nyingine, kwa hiyo chagueni viongozi ambao watakuwa watiifu kwa Serikali ya CCM," alisisitiza.

Akiahirisha mkutano wa Bunge la Bajeti Juni mwaka huu bungeni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitoa wito kwa wadau mbalimbali na wananchi kwa ujumla hususan wale wenye sifa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha na kupiga kura ili waweze kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua au kuchaguliwa katika uchaguzi huo.

Aliwataka wale wenye nia ya kugombea ni lazima wajue majukumu wanayoomba yanahitaji umakini mkubwa na uchapaji kazi.

"Serikali imewekeza miradi mingi kote nchini. Hivyo, kunahitajika watu walio tayari kuhakikisha wanasimamia miradi hiyo ili itoe matokeo yanayokusudiwa," alisema.

## Bil.161/- zahitajika kuondoa umaskini kwa mwezi

Na Augusta Njoji, DODOMA

UTAFITI wa Mapato na Matumizi ya Kaya binafsi kwa mwaka 2017/18, unaonyesha kuwa kiasi cha Sh. bilioni 161.1 kwa mwezi kinahitajika kuondoa umaskini wa mahitaji ya msingi kwa watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini Tanzania Bara.

Katika ripoti iliyotolewa hivi karibuni na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kuhusu utafiti huo, inasema kiasi hicho cha fedha ambacho ni sawa na Dola za Kimarekani milioni 70.1 kwa mwezi, zinahitajika kuondoa umaskini huo na kuwaleta kwenye mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi.

Utafiti unaonyesha asilimia 26.4 ya watu wa Tanzania Bara wana umaskini wa mahitaji ya msingi.

Umaskini wa mahitaji ya msingi ni mkubwa vijijini kwa asilimia 31.3 kuliko mijini na ni asilimia 15.8.

Pia, Mkoa wa Rukwa una kiwango kikubwa zaidi cha umaskini wa mahitaji ya msingi kwa asilimia 45 huku Dar es Salaam ikiwa ina asilimia nane ambachi ni kiwango kidogo zaidi.

Pia, utafiti unaonyesha mgawanyo wa kina cha umaskini miongoni mwa watu maskini wa vijijini kwa asilimia 7.4 ni mkubwa kuliko wastani wa taifa kwa asilimia 6.2 na ni zaidi ya mara mbili ya ule wa mijini kwa asilimia 3.5.

Aidha, kina cha umaskini kitaifa kwa kuzingatia tofauti ya kipato ni asilimia 2.1 na kwa maeneo ya vijijini ni kikubwa zaidi ya asilimia 2.6 kuliko katika maeneo ya mijini ambayo ni asilimia 1.2.

Pamoja na hayo, kumekuwa na ongezeko la kaya zinazoishi katika makazi yaliyojengwa kwa vifaa vya kisasa kwa asilimia 84.1 kwa mwaka 2017/18.

Vifaa hivyo ni pamoja na zege, mawe, saruji na vyuma ikilinganishwa na asilimia 68 ya kaya kwa mwaka 2011/12.

Utafiti huo pia unaonesha kuwa asilimia 78.8 ya kaya zinaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa kuta imara mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 46 mwaka 2011/12.

Vile vile, asilimia 50.1 ya kaya zinaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa sakafu imara mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 40 mwaka 2011/12.





## Watakiwa kushirikiana kutoa watalaam bora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amewataka walimu kuwa na ushirikiano kazini ili kuleta ufanisi wa kazi zao na kusaidia kutoa wataalam walio bora katika fani mbalimbali.

Akizungumza katika mkutano na watendaji wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume (KIST), katika ukumbi wa Taasisi hiyo Mbweni, nje kidogo ya Mji wa Zanzibar, alisema ni vyema kuondoa ubinafsi baina yao ili kuleta maendeleo katika elimu nchini.

Aliwataka walimu kufuata mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na kuwa wabunifu kwa kutumia mbinu mbadala katika ufundishaji kutaweza kuwasaidia kuleta mapinduzi katika masomo na kuwafanya wanafunzi wao waweze kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea ajira kutoka serikalini.

Aidha, aliwataka walimu hao kuzidisha bidii katika kazi yao pamoja na kuwa na subira kutokana na matatizo yaliopo katika taasisi hiyo, huku akiwaahidi kuwa wizara yake itaendelea kuyatatua matatizo hayo hatua kwa hatua.

Akizungumzia ombi kwa taasisi hiyo kushiriki katika maonyesho ya Sababa jijini Dar es Salaam, Simai aliwahakikishia kuwa wizara itajitahidi kufanya uwezekano ili taasisi hiyo mwakani iweze kushiriki katika maonyesho hayo.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Dk. Idrissa Muslim Hija, akijibu baadhi ya hoja za wafanyakazi hao suala la bima ya afya, alisema hivi sasa sera ya Serikali ni kutoa huduma ya matibabu bure hivyo si ruhusa kwa taasisi yoyote ya Serikali kuwalipia wafanyakazi wake bima ya afya kutoka katika pesa za serikali.

Alieleza kuwa mfanyakazi yeyote anaruhusiwa kukata bima kwa malipo yake mwenyewe, au taasisi ikiwa na mfumo wa kukusanya pesa wao wenyewe kwa utaratibu waliokubaliana, hakutakuwa na tatizo kufanya hivyo.

# Diwani asimamishwa tuhuma za kimaadili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi Zanzibar kimemsimamisha nafasi ya udiwani, Diwani wa Wadi ya Mtoni, Hamza Khamis Juma (40), kwa tuhuma za kwenda kinyume na maadili ya uongozi wa chama hicho.

Akitoa uamuzi huo, Katibu wa CCM Mkoa wa Magharibi kichama, Mgei Mussa Haji, alisema maamuzi hayo yamezingatia kanuni ya kamati ya ulinzi na maadili ya uongozi ya chama hicho kwa mujibu wa ibara ya 97 (7) ya kanuni ya CCM.

"Kiongozi yeyote ambaye anatuhumiwa anapaswa kuitwa katika kamati ya ulinzi na maadili ya uongozi ya chama hiki, mtuhumiwa kupewa nafasi ya kusikilizwa kwa hivyo tulimpa nafasi hiyo na kisha kuchukua maamuzi haya," alisema.

Diwani huyo anakabiliwa na mashtaka mawili ya madai ya kumtorosha na kumbaka mtoto wa kike wa miaka 16 ambaye yupo chini ya ungalizi wa wazazi wake.

**Hizi ni tuhumu tu hivyo zitabaki kuwa tuhuma, lakini kwa kuwa kesi ipo mahakamani tusubiri maamuzi ya mahakama kama itabaini kuwa sina hatia nitaendelea kuwa raia mwema.**

Katibu huyo wa CCM alieleza kuwa pamoja na kwamba kesi ya mtuhumiwa huyo ipo mahakamani, lakini chama kimetoa uamuzi huo kutokana na kuwa hakikubaliani na vitendo hivyo vya udhalilishaji na serikali pamoja na Chama cha Mapinduzi, kinapiga vita vitendo hivyo.

"Tunaiachia mahakama ifanye kazi yake endapo mtuhumiwa atakua hana hatia atarejeshwa nafasi yake ya uongozi, lakini endapo atakutwa na hatia chama kitamtafuta uongozi wake," alisema.

Pia, aliwataka viongozi wengine katika chama hicho kujitambua kuwa wao ni viongozi wamepewa dhamana ya kuwaongoza wananchi katika misingi mizuri na kuepukana na vitendo vya udhalilishaji.

Akizungumza na Nipashe, mtuhumiwa huyo, alikiri kuitwa na chama chake katika kamati ya wadi na halmashauri ya wilaya hiyo na kupewa nafasi ya kujieleza kuhusu tuhuma hizo.

Alisema anaheshimu maamuzi ya chama hicho na anasubiri mahakama iamue kama ni kweli atakua amaefanya tendo hilo hatua iweze kuchukua mkondo wake.

"Hizi ni tuhumu tu hivyo zitabaki kuwa tuhuma, lakini kwa kuwa kesi ipo mahakamani tusubiri maamuzi ya mahakama kama itabaini kuwa sina hatia nitaendelea kuwa raia mwema," alisema.

Ilidaiwa na Mahakama ya Mkoa Vuga kuwa Aprili 4, mwaka 2018, majira ya saa 11:00 alfajiri mtuhumiwa huyo, alimchukua mtoto huyo (jina linahifadhiwa) ambaye hajaolewa, kwa kumtoa kwa Mmanga Mwanyanya na kumpeleka kwenye nyumba iliyopo Mwanyanya, bila ridhaa ya wazazi wake.

Ilidaiwa baada ya kumtorosha, majira ya saa 11:20 alfajiri, mshtakiwa huyo anadaiwa alimuingilia kimwili ilhali akijua kuwa sio mke wake, kitendo ambacho ni kosa chini ya vifungu vya 108 (1) (2) (e) na 109 (1) vya sheria namba 6 ya 2018 sheriaza Zanzibar.



Mchuuzi wa mikate akiwa ameisheheni kwenye pikipiki yake, wakati akisaka wateja katika eneo la Tandale, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Balozi Iddi akemea makundi kwenye chama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Balozi Seif Ali Iddi, amekemea tabia ya ubinafsi inayopenda kuendekezwa na wapambe wa viongozi kuwa ni chimbuko la migongano inayozaliwa katika baadhi ya Majimbo visiwani Zanzibar.

Alisema wapo Wabunge na Wawakilishi wanakimbiana katika utekelezaji wa majukumu yao ndani ya majimbo yao kutokana na sintofahamu zinazozaliwa na wapambe wao, makundi ambayo hudumaza maendeleo yanayokusudiwa.

Balozi Iddi aliyasema hayo katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadir Abdulatif Ismail wa kukabidhi vifaa vya miradi ya maendeleo pamoja na zawadi alizoahidi ikiwa ni mwendelezo wa kutekeleza Ilani ya CCM huko Shule ya Chaani Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema wananchi lazima wajibebeshe jukumu la kuwasaidia viongozi wao hasa Wabunge na Wawakilishi ili kuondokana na tabia ya majungu inayoonekana kuwa ugonjwa katika baadhi ya majimbo Zanzibar.

Mjumbe huyo alisema wakati umefika kwa wananchi kutowabebesha majukumu binafsi viongozi wao ili kuwapa fursa na muda wa kukamilisha ahadi walizowapa wakati wa kampeni za uchaguzi.

Alisema hakuna kipengele ndani ya Ilani ya CCM kinachomtaka Mwakilishi au Mbunge amtekelezee mwananchi mambo yake binafsi kama kumjengea nyumba au hata mahari ya harusi badala yake waachiwe waendeleze na kusimamia miradi ya jamii ikiwamo elimu, huduma za afya pamoja na majisafi na salama.

"Wananchi wanapaswa kuelewa kwamba misaada binafsi sio lazima katika majukumu ya Mbunge na Wawakilishi," alisema Balozi Iddi.

Akizungumzia watu wengine wa nje wanaojitolea kusaidia wananchi ndani ya majimbo, Balozi Iddi alisema sio vibaya hata kidogo, lakini kinachopaswa kuzingatiwa ni uwapo wa mawasiliano baina ya watu hao na viongozi wanaohusika na usimamizi wa majimbo.

Alisema hatua hiyo ya mawasiliano itasaidia kudumisha na kuendeleza umoja na mshikamano wa makundi yote chini ya mwamvuli wa amani na utulivu inayohamashishwa na viongozi kila mara wakati na mahali popote pale.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadir Abdulatif Ismail, alisema shughuli hiyo ya utoaji wa vifaa vya kuendeleza miradi mbalimbali ndani ya jimbo hilo tayari ni ya 27 tokea apewe dhamana ya kuliongoza jimbo hilo.

Aliwaambia wananchi wa jimbo hilo kwamba yeye ndiye aliyepewa jukumu la kuwatumikia atatumia nguvu na uwezo wake wa kuona jimbo hilo linabadilika kimaendeleo katika muda mfupi ujao.

Katika mkutano huo, Mwakilishi wa Jimbo la Chaani alikabidhi matofali 2,000, TV tatu, printa na mashine ya fotokopi, matangi ya

## HABARI KITAIFA

# Tacaids yataja chanzo cha maambukizi VVU kwa vijana

Na Enock Charles

MKURUGENZI Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (Tacaids), Dk. Leonard Maboko, amesema sababu za vijana kuongezeka kwenye maambukizi mapya ya Ukimwi ni kutopata elimu wakati wa kutoka katika utoto kwenda ujana.

Alitoa kauli hiyo Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mipango ya mfuko wa kudhibiti Ukimwi.

"Hawajapata elimu (vijana) sawasawa, hivyo inakuwa rahisi kufanya maamuzi ambayo hana taarifa za kutosha. Lakini pia vijana wa kike kutaka kupata vitu kwa haraka.

**Hawajapata elimu (vijana) sawasawa, hivyo inakuwa rahisi kufanya maamuzi ambayo hana taarifa za kutosha. Lakini pia vijana wa kike kutaka kupata vitu kwa haraka.**

"Ndiyo maana tuna miradi ambayo inagusa kaya masikini kwa kuwasaidia kupata elimu ya ujasiriamali katika mikoa mitatu," alisema.

Alisema hadi sasa Tanzania inao watu milioni 1.5 wenye maambukizi ya virusi vya ukimwi ambao ni sawa na asilimia 4.7.

"Lakini maambukizo mapya yamepungua kutoka 80,000 miaka minne iliyopita hadi 72,000. Katika kundi hili Watanzania 6,000 wanapata maambukizo mapya kwa mwezi na kwa siku ni 200.

"Pia kati ya watu 200, vijana 80 wenye umri wa miaka 15 hadi 24 pia huambukizwa kwa siku," alisema.

Alisema tatizo la ugonjwa wa Ukimwi linabadilika kila mara, hivyo kuchangia zaidi ya asilimia 40 ya vijana kuathiriwa huku asilimia 80 wakiwa ni wasichana.

Katika hatua nyingine, Mgodi wa Dhahabu Geita (GGM) kupitia mfuko maalumu wa Kili Challenge, umetoa wito kwa asasi za kiraia zinazotoa huduma za Ukimwi nchini, kuandaa andiko kuomba fedha zilizochangwa na kampuni hiyo kupitia wadau.

Meneja wa Kili Challenge, Manase Ndoroma, alisema Bodi ya Kili Challenge ilikaa na kuamua Sh. milioni 800 ambazo kati yake Sh. milioni 550 zitabakia kusubiri asasi mbalimbali zitakazowasilisha maombi yao kuomba fedha hizo.

Alisema Kili Challenge ni mfuko unaoratibiwa na GGM na Tacaids kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kuchangisha fedha kwa kupanda Mlima Kilimanjaro na hupelekwa kusaidia kutoa huduma za kutokomeza maambukizi ya VVU/ Ukimwi.

Makamu wa rais wa mradi endelevu wa kampuni ya AngloGold Ashanti, GGM, Simon Shayo, alisema kwa mwaka huu katika kampeni hiyo ya kuchangia afua za Ukimwi imekusanya Sh. bilioni mbili.

Alisema tangu kuanzishwa kwa Kilimanjaro Challenge, zimekusanywa zaidi ya Sh. bilioni 13 ambazo zimenufaisha asasi na taasisi mbalimbali 50 zinazoshughulikia masuala ya Ukimwi.




Meneja wa Mfuko wa Kili Challenge, Manace Ndoroma, akizungumza katika hafla ya utoaji fedha kwa baadhi ya taasisi zinazotoa huduma za Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi. Mchango huo unalenga kudhibiti maambukizi ya VVU kupitia kampeni ya mfuko huo inayoratibiwa na GGM pamoja na Tacaids. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wataalam elekezi wa washauriwa kuchangamkia maonyesho

Na Elizabeth Zaya

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewataka wataalamu elekezi wa mazingira hapa nchini kutumia fursa ya Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kukamilisha ada, tozo na michango mbalimbali wanayopaswa kulipia katika kipindi husika.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka kwenye maonyesho yanayoendelea jijini Dar es Salaam, Mhasibu wa Baraza hilo, Beatrice Kilimo amesema maonyesho ni fursa pekee kwa watalaamu elekezi kuchangamkia fursa hiyo.

"NEMC tupo kwenye Banda la Katavi chumba namba 53 na 54 tukiwa tumejikita katika kutoa elimu kwa umma kuhusiana mambo mbalimbali yanayohusu uhifadhi na utunzaji wa mazingira na huduma nyinginezo," Bi. Kilimo alisema.

Alisema pamoja na mambo mengine wanatumia maonyesho hayo ya biashara ya kimataifa maarufu kama Sabasaba kupokea tozo mbalimbali na ada za mwaka kwa wataalamu elekezi ambao hawajalipa mpaka sasa.

"Sisi kama Baraza tumejipanga kutoa elimu endelevu ya mazingira kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo na pia kwenda sambamba na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Dk. John Magufuli ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025," alisema Afisa huyo.

Kilimo mbali ya kuhamasisha watu na wadau mbalimbali wa mazingira kujitokeza kwa wingi kwenye banda la Baraza, alisema wanasajili pia miradi sambamba na utoaji wa risiti na hati za malipo.

"Tupo vizuri na tumeridhishwa na huduma zinazotolewa na waandaji wa maonyesho haya ambao ni Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) na watu wengi wanakuja kujifunza na elimu juu ya mazingira," alisema.

# Mil. 847/- kupeleka umeme kata 10 Kahama, Msalala

Na Shaban Njia, KAHAMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, limepokea Sh. milioni 847 kwa ajili ya kupeleka huduma ya nishati ya umeme kwenye kata 10 Halmashauri ya Mji wa Kahama na Msalala.

King Fokanya, Meneja wa Tanesco wilayani hapa, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari, na kueleza kuwa fedha hizo zimetolewa kwa mwaka huu wa fedha 2019/20.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 402 zitapeleka nishati hiyo kwenye kata hizo za Msalala na Kahama mjini, huku Sh. 445 zikitumika kwenye matengenezo ya kubadilisha nguzo, vikombe, maboresho ya transfoma na vifaa vilivyoharibika.

Afokanyanga alizitaja kata ambazo zinapelekewa huduma ya nishati ya umeme katika Halmashauri ya Mji wa Kahama ni Muhungula, Nyakato, Mbulu, Mhongolo, Nyashimbi, Nyihogo Sekondari, Kagongwa, Mwendakulima wakati Halmashauri ya Msalalani ni Isaka na Kakola.

"Fedha tulizozipata zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupeleka nishati ya umeme kwenye kata zetu 10, na itakuwa rahisi maendeleo kuwafikiwa wananchi wanaoishi ndani ya kata hizo, kikubwa wanatakiwa kutunza miundombinu na kuacha kulima jirani na nguzo za umeme," aAlisema Fokanya.

Hata hivyo Fokanya aliwataka wananchi kuacha tabia ya kufanyabiashara jirani na transfoma kwani kitendo hicho ni hatari na kinaweza kusababisha madhara makubwa wakati wowote ikiwamo kuacha kupanda miti katika njia za umeme ili kuzuia kukatikakatika kwa umeme.

ITV

IJUE SHERIAE: SAA 1:00 USIKU

JE, UNAIFAHAMU SHERIA YA USAFIRISHAJI, KWA NINI SHERIA HII ILITUNGWA, NANI WASIMAMIZI WAKE, WADAU WAKUU WA SHERIA HII NI NANI, SHERIA INAPOKIUKWA WADAU NA WASIMAMIZI WANAPASA KUWASILISHA MALALAMIKO YAO WAPI?. MWANASHERIA LEONARD MANYAMA KATIKA SEHEMU YA KWANZA ATAFAFANUA KIUNDANI.

## Trump aendeleza malumbano na Sur Kim Darrach

**NEWYORK, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameendeleza shutuma zake dhidi ya balozi wa Uingereza nchini humo, Sir Kim Darrach, akisema kuwa hatoshirikiana naye tena.

Katika matamshi yake katika mtandao wa Twitter Rais Trump pia alimshutumu Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May akisema kuwa ''ni habari njema kwamba Uingereza itapata Waziri Mkuu mpya''.

Balozi Kim katika barua pepe zilizofichuliwa siku ya Jumapili aliutajaa utawala wa Rais Trump kama usiofanya kazi na usiojielewa.

May alisema kuwa ana imani na Balozi huyo, lakini hakubaliani naye.

Theresa May alijiuzulu baada ya kukosa kuungwa mkono na bunge kuhusu mpango wake wa Brexit na chama tawala sasa kitalazimika kuchagua kati ya mgombea Boris Johnson au Jeremy Hunt kuchukua nafasi yake.

Idara ya maswala ya kigeni ya Marekani ilikataa kutoa tamko lolote kuhusu matamshi hayo ya Trump ambayo yanaweza kuibua maswali iwapo balozi huyo sasa ataruhusiwa kuingia nchini Marekani ama la.

Kwa kusema kwamba hatoshirikiana naye (Sir Kim Darroch), inaweza kumaanisha kwamba balozi huyo sasa hatakiwi nchini Marekani, kwa kuwa hiyo ndio njia rasmi ambapo serikali humtimua mwanadiplomasia wa kigeni.

Iwapo Rais Trump anamaanisha kwamba utawala wake wote hautashirikiana naye basi serikali ya Uingereza italazimika kuamua kumuondoa mjumbe wao mjini Washington.

Hii inamaanisha kwamba taifa la Uingereza litawekwa katika hali ya

**BBC.**

# Aeleza alivyoachwa kwenye ndege kisa usingizi mzito

**OTTAWA, Canada.**

MWANAMKE mmoja amesema aliachwa peke yake ndani ya ndege baada kulala usingizi mzito akiwa safarini.

Tukio hilo limemkuta Tiffani Adams, Juni 9 mwaka huu ambaye alikuwa akisafiri kwa kutumia Shirika la Ndege la Canada kutoka Jiji la Quebec kwenda Jiji la Toronto.

Alipoamka, alijikuta yumo ndani ya baridi kali, huku bado akiwa amefunga mkanda wa kiti chake, lakini ndege ilikuwa imeegeshwa na taa zote zimezimwa.

Amesema amekuwa akipatwa na "ndoto za kutisha" toka tukio hilo lilipomtokea. Shirika la Ndege la Canada limethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba wanafanya uchunguzi.

Mwanamke huyo ameandika kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Facebook kuhusu tukio hilo.

"Mishale ya saa sita usiku (saa chache baada ya ndege hiyo kutua) nilikuwa kwenye baridi kali huku nikiwa bado nimechomeka mkanda wangu kitini, na kiza totoro," alisema.

Mwanamke huyo alifanikiwa kumpigia simu rafiki yake, Deanna Dale na kumfahamisha mahali alipo na kabla hawajamaliza kuongea, simu yake ilizimika kwa kuishiwa chaji na hakuweza kuchaji simu yake kwani ndege ilikuwa imezimwa.

Deanna Dale alifanikiwa kuwapigia simu polisi wa Uwanja wa Ndege wa Toronto Pearson na kuwaarifu juu ya masaibu ya rafiki yake na mahala alipo.

Akiwa amekwama ndani ya ndege, Tiffani Adams aliweza kuona taa kwenye eneo la rubani na akajaribu kuiwasha ili watu waone kuna kitu ndani ya ndege hiyo na hatimaye kuonwa na dereva wa vigari vya kupakua mizigo ya wasafiri, ambaye anasema alipigwa na butwaa kumuona mwanamke huyo.

Mwanamke huyo alidai wafanyakazi wa gari la kifahari na chumba cha hoteli na Shirika la ndege la Canada baada ya kumnasua kutoka kwenye ndege hiyo, lakini akawagomea, akitaka kurejea nyumbani kwa haraka iwezekanavyo.

Shirika hilo limekiri kutokea kwa tukio hilo kwenye vyombo mbalimbali vya habari na kudai wanaendelea na uchunguzi wa kisa hicho.

***BBC***




Ndege aina ya Sling 4 iliyotengenezwa na wanafunzi 20 Afrika Kusini. Ndege hiyo inadaiwa kutua salama jijini Cairo nchini Misri wiki sita baada ya kuondoka. **PICHA: BBC .**

# Marekani 'yaichokoza' China kuhusu Taiwan

**NEWYORK Marekani.**

IDARA ya masuala ya kigeni nchini Marekani, imeidhinisha uuzaji wa silaha kwa Taiwan , utakaogharimu dola bilioni 2.2.

Mpango huo utahusisha kuuzwa vifaru 108 , makombora 250 na vifaa vingine vinavyohusiana.

Mwezi uliopita, wizara ya masuala ya kigeni nchini China iliitaka Marekani kusitisha uuzaji huo , ukiutaja kuwa suala nyeti na uamuzi mbaya.

China inaichukulia eneo la Taiwan kuwa miongoni mwa himaya yake ambayo inafaa kuunganishwa na nchi kavu kwa nguvu iwapo zitahitajika.

Msemaji wa wizara ya masuala ya kigeni wa China, Geng Shuang, aliitaka Marekani kuheshimu sera ya China ya taifa moja ambapo marekani inaitambua China na sio Taiwan.

Marekani ilidai uuzaji wa silaha hizo hautaathiri uwezo wowote wa kijeshi katika eneo hilo na tayari Idara ya Ulinzi ya Marekani imelieleza bunge la nchi hiyo kuhusu uuzaji huo wa silaha.

Msemaji wa Rais wa Taiwan, alisema katika taarifa kwa Reuters kwamba kisiwa hicho kitaendelea kuimarisha uhusiano wake wa kiusalama na Marekani.

***BBC.***

# Ndege iliyotengenezwa na wanafunzi yatua salama

**CAPE TOWN , Afrika Kusini.**

Ndege iliyotengenezwa na wanafunzi wa Afrika Kusini imetua salama Jijini Cairo Misri wiki sita baada ya kuondoka Cape Town, Afrika Kusini.

Ndege hiyo yenye viti vinne aina ya Sling 4 plane ilitengenezwa na kundi la wanafunzi 20 kutoka familia tofauti. Jumla ya wanafunzi sita walishiriki katika safari hiyo kama marubani na watoa msaada wa kiufundi.

Safari yao ya kilomita 12,000 ilikuwa na vituo nchini Namibia, Malawi, Tanzania (Zanzibar na Kilimanjaro), Uganda na Ethiopia.

Rubani Megan Werner, msichana wa miaka 17, aliyeanzisha mradi wa U-Dream Global ambao ndio umewezesha safari hiyo amesema amefurahia mno mafanikio yao.

"Nimefarijika sana kwa hiki tulichokifanya, tumeonesha utofauti ndani ya bara (Afrika) katika sehemu zote tuliposimama,lengo la mradi ni kuonesha Waafrika kuwa kila kitu kinawezekana kama utaweka akili yako katika kulifanikisha hilo," alisema.

Wanafunzi hao walikuwa wakitoa mihadhara kwa wanafunzi wenzao kwenye kila nchi waliyosimama.Ndege nyengine aina ya Sling 4, ilikuwa ikiambatana nao na kuendeshwa na marubani wenye uzoefu ili kutoa msaada pale unapohitajika.

Baba wa Megan, Des Werner ambaye ni rubani mwandamizi alikuwa ni sehemu ya timu ya msaada. Wanafunzi hao waliitengeneza ndege hiyo kwa wiki tatu kwa kuunganisha vifaa vilivyotengenezwa na kampuni moja nchini humo. Uundaji huo ulihusisha kuunganisha maelfu ya vifaa vidogo vidogo.

***BBC***

## Waziri afunguka mauaji ya Watanzania Msumbiji

**Na Romana Mallya**

KUTOKANA na mauaji ya Watanzania tisa nchini Msumbiji, serikali imewataka wananchi kufuata sheria za nchi kwa kuzingatia taratibu zilizopo za kuvuka mpaka kwenda nchi nyingine ili iwe rahisi kusimamia usalama wao wanapopatwa na matatizo.

Mauaji hayo yalitokea mwishoni mwa mwezi uliopita katika kijiji cha Nkole kilichopo upande wa Msumbiji ambapo pia raia wengine wawili wa nchi hiyo nao walipoteza maisha.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa hadhara katika kijiji cha Kihamba mkoani Mtwara, kuhusiana na tukio hilo ambalo Watanzania hao walikuwa Msumbiji kwa shughuli za kilimo cha mpunga.

"Nawaomba mfuate sheria za nchi yetu kwa kutumia utaratibu uliowekwa wa kuvuka mpaka mmoja kwenda nchi nyingine ili iwe rahisi kusimamia usalama wenu," alisema na kuongeza:

"Serikali inaendelea kuhakikisha hatulali usingizi hadi wahalifu wote wakamatwe. Ili muendelee kufaidi matunda ya serikali hii nawaomba mtoe ushirikiano wenu kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuhusu watu mnaowatilia mashaka ili zifanywe kazi."

Hata hivyo, alisema walifanya mauaji hayo mpaka sasa hawajapatikana, na kusisitiza kuwa watakamatwa.

"Nimeona nizungumze hayo mambo mawili muhimu kwenu, mengine tuachieni Serikali tutahakikisha tunaviwezesha vyombo vyetu hususani katika maeneo haya, nyinyi ni mashahidi kuwa hali ya usalama katika nchi hii ni nzuri," alisema.

Masauni alisema serikali itahakikisha kila inavyoweza kufanywa inalinda usalama na maisha ya wananchi wa Mtwara na Watanzania kwa ujumla.

"Serikali haiko tayari kuona uhai wa raia wake ukichezewa tunawahakikishia wananchi ulinzi na usalama lakini na nyie mtoe taarifa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama pindi mnapotilia shaka mtu yoyote ili uhalifu udhibitiwe," alisema.

Mauaji hayo yalitokea mwishoni mwa mwezi uliopita wakati Watanzania hao wakiwa shambani wakilima mpunga walivamiwa na watu wasiofahamika wenye silaha, na kuwashambulia na kusababisha vifo hivyo na kujeruhi Watanzania wengine sita.

# DC: Tunafanyia kazi madai viongozi Chadema kutekwa

**INATOKA UK. 3**

"Lile bwana mniache, mimi nina shughulika na hili suala kubwa la msiba sasa hivi," Njewike alisema. Jumapili Chadema kilidai, kutekwa na kuteswa kwa baadhi ya viongozi na wanachama wake Jimbo la Singida Mashariki na vijana wa ulinzi wa CCM (Green guard) katika Jimbo hilo.

Katibu wa chama hicho Kanda ya Kati, Idd Kizota alidai viongozi hao walikuwa katika ofisi za chama hicho katika jimbo hilo katika kikao cha ndani kwa lengo la kufanya uhaguzi wa ndani ya chama, na baadae kuvamiwa na vijana hao na viongozi wao wawili kutekwa na kupelekwa kusikojulikana .

"Walikuwa kwenye uchaguzi wa ndani ya chama katika ofisi ya chama na baadae walivamiwa na kikundi cha vijana wa green guard na kutokomea kusikojulikana na pia walivunja kioo cha gari yetu moja aina ya Ford Ranger, ingawa dereva alifanikiwa kuwakimbia," Kizota alisema.

Viongozi wanaodaiwa kutekwa na kuteswa ni Mwenyekiti wa Chadema Jimbo la Singida Mashariki, Agnesta Lambat na Diwani wa Misughaa, Jumanne Rajab ambao kwa mujibu wa Katibu huyo, Agnesta alilazwa hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma, huku Diwani akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Makiyungu mkoani Singida.

Akizungumzia madai hayo ya viongozi wa Chadema Jumapili, Kamanda Ngwike alidai anashangaa madai hayo ya watu kutekwa na kuahidi kuwa Jeshi la Polisi litatoa taarifa kuhusiana na suala hilo Jumatatu.

"Hii lugha ya kutekwa kutekwa kutekwa sijui inatoka wapi tutatoa taarifa kesho (Jumatatu) kuhusiana na hilo," Kamanda Ngiwike alisema.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage, alitangaza ratiba ya kufanyika kwa uchaguzi katika jimbo la Singida Mashariki Julai 31 mwaka huu.

Jaji Kaijage alisema fomu za uteuzi wa wagombea zitatolewa kati ya Julai 13 na 18, mwaka huu na uteuzi wa wagombea utafanyika Julai 18, na kampeni za uchaguzi zitafanyika kuanzia Julai 19 hadi 30.

Uchaguzi huo ni kwa ajili ya kujaza nafasi ya aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Tundu Lissu (Chadema), ambaye alivuliwa wadhifa huo na Spika wa Bunge, Job Ndigai, kwa maelezo kuwa amekosa sifa.



Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM taifa, Humphrey Polepole (kushoto), akikabidhi cheti kwa mwanafunzi Doreen Tupa wa Chuo Kikuu SAUT ambaye ni mmoja wa vijana wa UVCCM, vyuo vikuu mkoa wa Mwanza, kwenye mahafali yaliyofanyika Chuo Kikuu cha SAUT, jijini Mwanza hivi karibuni. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Anayedaiwa kumuua mke ana kesi ya kujibu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imemuona Godfrey Nkwambi, anayekabiliwa na kesi ya kumuua kwa makusudi mke wake Bahati Hussein ana kesi ya kujibu na imesema atajitetea Julai 18, mwaka huu.

Uamuzi huo ulitolewa jana katika mahakama hiyo iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji iliyoketi chini ya Naibu Msajili, Pamela Mazengo, baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wao.

Mapema jana, Daktari Bingwa wa uchunguzi wa vifo vyenye utata na magonjwa mbalimbali wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dk. Innocent Mosha, alieleza mahakama kuwa kifo cha Bahati kilisababishwa na majeraha yaliyokutwa shingoni kwake baada ya pingili zake mbili kutenguka.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Erick Shija kutoa ushahidi wake jana, shahidi huyo alidai, alipoufanyia uchunguzi mwili wa marehemu aligundua pia kulikuwa na mvilio wa damu kuzunguka pingili zake za shingo na mapafu yake yalikuwa yamejaa damu na hewa. Dk. Mosha ambae ni shahidi wa sita katika kesi hiyo amedai, Juni 23, 2012 akiwa kazini, alipokea maelekezo kutoka Jeshi la Polisi Kituo cha Stakishari, wakitaka kumfanyia uchunguzi mwili wa marehemu Bahati kwa kuwa walikuwa wanahisi kuwa ameuawa kwa kupigwa.

Alidai kuwa baada ya kupokea amri hiyo, alipata mashahidi wawili walikwenda pamoja na mpelelezi kwa ajili ya kumtambua marehemu akiwamo Muhidin Hamisi na Maxmillian na kwamba baada ya zoezi la utambuzi kabla ya kuanza kufanya uchunguzi alipata maelezo mafupi kutoka kwa mpelelezi E 1279 Detektivu Koplo Peter.

"Nilifanya uchunguzi katika sehemu ya nje ya mwili wa marehemu na ndani na katika sehemu ya nje ya mwili nilikuta michubuko kidogo sehemu ya shingoni huku macho yake yakiwa na mivilio midogo midogo ya damu na kucha zake zilikuwa zimebadilika rangi na kuwa za dark blue (bluu ilikoza)," alidai na kuongeza:

"Uchunguzi wa sehemu ya ndani ya mwili wa marehemu niligundua kuwa pingili mbili za shingo yake zilikiwa zimetenguka na kulikuwa na mvilio wa damu kuzunguka hizo pingili, pia mapafu yake yalikuwa yamejaa hewa na damu na hivyo kuonyesha chanzo cha kifo chake ni majeraha," alidai Dk. Mosha.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa umefunga ushahidi wake.

Msajili Mazengo alisema baada ya kusikiliza ushahidi wa mashahidi sita wa Jamhuri mahakama yake imemuona mshtakiwa ana kesi ya kujibu tuhuma za kumuua mke wake kwa makusudi.

Alisema utetezi wa mshtakiwa utasikilizwa Julai 18, mwaka huu.

Mapema wiki iliyopita watoto wawili wa marehemu akiwamo mtoto wa miaka 10,ambaye wakati mama yake anauawa alikuwa na miaka mitano, alidai mahakamani alimuona baba yake wa kambo (mshtakiwa) akimnyonga mama yake Bahati.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Juni 21, 2014 eneo la Ulongoni Nkwambi, alimuua kwa makusudi mke wake Bahati.

Mshtakiwa alifunguliwa mashtaka na kufikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

### MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008

**ENEO LINAUZWA EKA 15 LINAGUSA** LAMI LIPO MAENEO YA MASUGURU BAGAMOYO KILOMITA 9 MPAKA MSATA – 0718679428.

**PROJECTS GENERATE INCOMES AND CREATE EMPLOYMENT** *Learn DESIGNING projects *Find DONORS *Establish NGO 0784505108 /0769505108

### NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI,** Wanahitajika IT – Diploma, Sales Lady, Messenger – awe mvulana. Elimu kidato cha nne/ cha sita. Wawe wazoefu wa kutosha. Mawasiliano: 0715 885533. Email: jmtofficetraders96@gmail.com au jmtofficetraders@gmail.com.

*KWA MATANGAZO MADOGO, MADOGO*

***Tupigie***

***0767223311***

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU ABDUL NASSORO** WA SLP 139 KATORO WILAYA NA MKOA WA GEITA ANATANGAZA KUPOTOLEWA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SANLG YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 263 BWL RANGI NYEKUNDU CHASSIS NAMBA **LBRSPJB 56J9001388,** ENGINE NAMBA SL 157 FM1-18901575 .

NA KUFUNGULIWA
TAARIFA YA KUPOTEZA

KITUO CHA POLISI KATORO
**KUMB KTR/RB/1199/2019**
**YA JUNE 26.2019**

215317002

### KUPOTELEWA NA CHETI



**WINFRIDA N. RICHARD**


Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye namba CS140144814 kilichotolewa mwaka 2014 na **MOUNT MORIE SEC SCHOOL index nambaS.5168/0010** na Cheti cha kumaliza elimu ya msingi **KABANGA SHULE YA MSINGI** Mwaka 2008 chenye namba A0840982,vilivyopo**tea Mkoani Kigoma.**

**Yeyote atakaviona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.**

**Taarifa ya Polisi.**
**KAH/TR/RB/720/2019.**

215316102

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA (PASIPOTI)




**DR. MUTABAAZI JULIUS LUGAZIYA**
Anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria yenye **Na. AB 806502** iliyotolewa Dar es salaam tarehe **7 Septemba, 2016.**

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi Kumb. No. CD/RB/3096/2019.**

115315602

### CHETI KIMEPOTEA



**JOHN J. KASANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1456/0200** kilichotolewa na **ITIJI SEKONDARI** mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**
**MBE/MBE/RB/106357/2019.**

115314902

### KUPOTELEWA NA VYETI



**Hawa Abel Kitomary** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **Index number S0201-0072** kilichotolewa na Ashira Secondary School mwaka 2007. Cheti cha kidato cha sita chenye **Index namba S.0317-0506** kilichotolewa na Kibo Secondary School mwaka 2010.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya Polisi ni MHE/RB/713/2019.**

115315902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**WILAYA YA NYAMAGANA MWANZA**
**RM. COMMERCIAL CASE NO. 44/2019**

**MDAI...........................JOKER AFRICA LTD**

**DHIDI YA**
**MDAIWA...........................CAPE HOLDINGS LTD**

**KWA: CAPE HOLDINGS LTD**
**POPOTE ALIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Mdai mtajwa hapo juu amefungua madai dhidi ya cape Holdings ltd mahakama imepanga kutajwa kwa shauri hili tarehe 10/07/2019 hivyo unatakiwa kuwepo mahakamani tarehe hiyo na usipohudhuria mahakama itapanga tarehe ya kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila wewe kuwepo

Imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa mahakama hii tarehe 02 julai,2019 leo tarehe 02/07/2019

215316502

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LEILA SIRIKWA MBUYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA yenye namba za usajili T570 BCY rangi ya BLUE. Chassis namba **ACR300125401**. Engine namba. ZAZ0492823.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/RB/1247/2019**

215316602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;146/2019**

Ombi la **SAID MOHAMED JAMBWALI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MOHAMED IBRAHIM JAMBWALI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/07/2019.

215316202

**JAM COMPANY LTD**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na Sido Iringa tutauza mali za wadaiwa walioshindwa kurejesha mikopo yao na wale walioshindwa kulipa deni la pango, majengo ya Sido.

1. Nyumba ya John Markusi Kasuva na mkewe Rehema Mgesi kata ya Kitwiru Nyamhanga "E" Kitalu 85.
2. Dickens Lulandala mashine ya unga ipo ndani ya jengo la Sido inafanyakazi
3. Itaewon mashine ya kukamua alizeti inafanyakazi ipo ndani ya jengo la Sido.
4. Anneth Mbilinyi mashine ya unga ipo ndani ya jengo la sido inafanya kazi.
5. Bibiana Mboya na mume wake Bartazar Kinana Masawe nyumba ipo Mtwivila kubwa nzuri.

**Mnada tarehe 20/7/2019 Saa 5:00 (tano kamili) asubuhi. Masharti yatazingatiwa.**

**Wasiliana nasi: 0764 782526/0754 558799**

115316002

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS
POLICE FORCE
LOSS REPORT
DOD/DOD/RB/115067/2019

This is to identify that PAUL A. MWANGA Reported to the police on 8/7/2019 that under-mentioned property has been lost.

Property Type: Nyaraka

Property Name: Hati ya New Life in Christ

Property Number: So.5042

Property type: Nyeupe.

More derails imepotea

115315302

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**CITY BOYS ELECTRONICS CO LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TVS STAR HLX 150** yenye namba za usajili MC 914 CAZ . Chassis namba **MD625AF75J1G11377.** Engine namba. AF7GJ1210967.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/DOD/RB/15472/2019**

115315402

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MEDARD NGAIZA EDWARD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA IST yenye namba za usajili **T 404 CDQ.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/CHA/RB/116188/2019.**

115315102

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**JOSSAM LAITON MALEMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki (Boxer) yenye namba za usajili **MC 954 BTD**. Chassis namba **MD2A21BY5HWD50432.** Engine namba **PFZWHD37385.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/OST/RB/59908/2019.**

115315202

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO KWA BEI**

**NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# ZOLA: SARRI ALIONDOKA MAPEMA CHELSEA

**TURIN, Italia**

KOCHA msaidizi wa zamani wa Chelsea, Gianfranco Zola, anaamini kwamba Maurizio Sarri aliondoka mapema mno katika klabu hiyo.

Sarri aliomba kuondoka pale Chelsea baada ya mwaka mmoja na kurudi nyumbani kwake Italia na kuwa kocha wa Juventus, huku mikoba yake ikichukuliwa na Frank Lampard.

Zola, ambaye ameondoka na Sarri na kuwa msaidizi wake kule Juventus amemzungumzia Mtaliano mwenzake huyo na kusema: "Nafikiri mafanikio ya kazi ya Maurizio hayaji kwa mwaka mmoja, bali kwa mwaka wa pili.

"Ukiangalia namna anavyofanya, inamfanya achukue muda kidogo, pia naamini aliwahi mno kuamua kuondoka Chelsea.

"Lakini wachezaji anaofanya nao kazi huwa nao wanatumia muda kuzoea staili yake, hivyo alihitaji kupata muda zaidi wa kuendelea kuwa kocha pale Chelsea.

"Naamini kama angepata muda zaidi wa kuendelea kubakia Cheslea angeweza kupata mafaniko zaidi ya yale aliyofikia."

Sarri kwa kipindi cha mwaka mmoja aliokaa pale Chelsea aliiwezesha kutwaa taji la Ligi ya Europa pamoja na kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.



# BAYERN YASUBIRI UAMUZI WA SANE

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich inatarajia Leroy Sane atafanya uamuzi wake wiki ijayo kuhusu hatima yake.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, wamemfanya Sane ambaye ni winga wa Klabu ya Manchester City kama chaguo lao la kwanza kwenye usajili wa kipindi hiki cha majira ya joto.

Sane, ambaye anatajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 90, anatarajia kuripoti kwenye mazoezi ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu England, kabla ya kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola hakijaanza ziara yao barani Asia.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Bayern, Karl-Heinz Rummenigge alisema Jumatatu: "Tulitaka kufikiria kuhusu majaliwa yake wakati akiwa likizo. Sasa tunatakiwa kusubiri.

"Hali ya sasa ya Sane ni kwamba anarudi kutoka likizo wiki hii. Bado tunaendelea kutafuta mawinga baada ya kuwapoteza wawili (Arjen) Robben na (Franck) Ribery."

City wao wanaamini kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 atabakia hapo kwenye dimba la Etihad, ingawa mazungumzo ya kuongeza mkataba wake yakiwa yanaendelea kwa mwaka sasa.

Bayern bado haijatoa ofa rasmi kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, ambaye amefunga mabao 39 katika misimu mitatu pale City.

# Leicester yafanikiwa kumsajili Youri

**LEICESTER, England**

KLABU ya Leicester City imemsajili Youri Tielemans kwa mkataba wa kudumu kutoka Monaco baada ya kuwa kwenye kiwango cha juu msimu uliopita ambapo alikuwa akicheza kwa mkopo.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 22 amesaini mkataba wa miaka minne wa kukaa na Leicester ambao wamelipa kiasi ha pauni milioni 40.

Tielemana alifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho nne katika mechi 13 alizoichezea Leicester baada ya kutua hapo kwa mkopo wa miezi sita Januari mwaka huu akitokea kwa miamba hao wa Ufaransa.

Mara baada ya kusaini mkataba huyo,



Tielemans amesema: "Ni hisia kubwa kwa upande wangu kusajili hapa. Tangu nilipowasili hapa kwa mkopo msimu uliopita, wachezaji wote pamoja na maofisa wa timu wamekuwa wakarimu kwangu.

"Hivyo kuendelea kubakia hapa kwa miaka mingine minne, kunanifanya niwe kwenye wakati mzuri zaidi na naamini nitakaa muda mzuri zaidi wa kuimarisha kipaji changu hapa nikiwa na wachezaji wa Leicester.

"Naamini kikosi chetu kina wachezaji wenye vipaji na kwamba tuna uwezo wa kufanya vizuri zaidi msimu unaokuja.

"Kwa hakika kabisa nasubiri kwa hamu kubwa kuanza kucheza msimu mpya unaokuja ili kuendelea kuisaidia timu yetu."

## HABARI MICHEZO



# UNITED
## YAJITOSA KUMWANIA BAKAYOKO

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kwamba inamshawishi kiungo wa Chelsea, Tiemoue Bakayoko, ajiunge nao wakati kocha Ole Gunnar Solskjaer akiwa kwenye harakati za kuimarisha kikosi chake kipindi hiki cha majira ya joto pale Old Trafford.

Solskjaer tayari ameshasajili sura mpya mbili, Daniel James na Aaron Wan-Bissaka wakati huu wa kipindi cha majira ya joto.

Na sasa United wanapanga kumshawishi Bakayoko, ambaye alikuwa akicheza kwa mkopo kule AC Milan msimu uliopita, kwa mujibu wa gazeti la Marca.

Miamba hao wa Old Trafford wameripotiwa kwamba wamevutiwa na kiwango cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 na sasa wanataka kumsajili kutoka kwa wapizani wao wa Ligi Kuu England.

Bakayoko, ambaye alitua pale Stamford Bridge kutoka Monaco miaka miwili iliyopita kwa ada ya pauni milioni 40, amebakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake na Blues hao.

Arsenal na mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain pia waliripotiwa kumwania kumsajili kiungo huyo wa kati.

Huku Paul Pogba akihusishwa na mpango wa kuondoka hapo United katika kipindi hiki cha majira ya joto, United wanahitaji kuongeza mchezaji mwingine ili kujipanga zaidi kwenye msimu mpya wa Ligi Kuu.

Bakayoko kwa sasa yupo na wachezaji wenzake wa Blues nchini Ireland wakati kocha mpya, Frank Lampard akikiandaa kikosi hicho kwa ajili ya msimu mpya wa 2019-20.

Klabu za Ligi Kuu England wana mwezi mmoja wa kukamilisha usajili wa wachezaji wa kipindi cha majira ya joto ambapo dirisha hilo litafungwa rasmi Alhamisi ya Agosti 8 mwaka huu.

# Arsenal wakubali ada ya kumnunua Saliba



**LONDON, England**

ARSENAL wamefikia makubaliano ya ada ya pauni milioni 26 ili kumsajili beki wa kati wa klabu ya Saint-Etienne, William Saliba.

Klabu hiyo ya Ufaransa awali ilitaka kumtoa kwa mkopo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 kwa msimu mmoja.

Saliba alicheza mechi 16 wakati alipoanza kucheza kwenye Ligi Kuu Ufaransa maarufu Ligue 1, baada ya kupenya katika kikosi cha kwanza Septemba mwaka jana.

Safu ya ulinzi ya Arsenal msimu uliopita ilionekana kupwaya kwenye ligi Kuu England na hivyo kocha, Unai Emery anaweza kumfanya Saliba kuwa kwenye kikosi cha kwanza msimu huu.

Rais wa Saint-Etienne, Roland Romeyer, alidai kwamba mchezaji huyo alitakiwa kuendelea kucheza kwa mwaka mmoja zaidi hapo katika dimba la Geoffroy-Guichard ili kuimarisha kipaji chake.

Kama Arsenal itakubali kumwachia aendelee kucheza kwa mkopo pale Saint-Etienne ataweza kujiimarisha zaidi kabla ya usajili wake kukamilika kipindi cha majira ya joto hapo mwakani.

Hata hivyo, Arsenal inaweza kusubiri hadi mwakani ili kumchukua moja kwa moja mchezaji huyo.

## JUVENTUS YAKATAA KUMUUZA KEAN

**TURIN, Italia**

KLABU ya Everton imeripotiwa kuwa imegonga mwamba katika mpango wake wa kutaka kumsajili kinda wa Juventus, Moise Kean.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 ni mmoja wa kinda anayetajwa kuwa na kipaji cha hali ya juu barani Ulaya, akiwa amefunga mabao sita katika dakika 536 alizocheza kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu uliopita.

Kwa mujibu wa gazeti la La Gazzetta dello Sport, Everton walitoa ofa ya pauni milioni 27 kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo ambayo imekataliwa na Juventus.

Kean pia amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa Ajax kipindi hiki cha majira ya joto.

Ameichezea mechi tatu Timu ya Taifa ya Italia na kufunga mabao mawili.

Lakini pia aliichezea timu ya taifa ya Italia ya vijana wa umri chini ya miaka 21 kwenye michuano ya mataifa ya Ulaya kwa umri huo.

Everton wapo sokoni kwa ajili ya kununua wachezaji wa kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AINGIA MATATANI PSG

●●●Ni kutokana na kushindwa kuhudhuria katika mazoezi ya kwanza ...

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris St-Germain imesema kuwa itachukua hatua kali baada ya mshambuliaji wake, Neymar kushindwa kuhudhuria mazoezi ya kwanza ya timu hiyo, imefahamika.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, raia wa Brazil alitarajiwa kurudi katika mazoezi juzi Jumatatu.

Mshambuliaji huyo amehusishwa na uhamisho kurudi klabu yake ya zamani ya Barcelona.

Paris St-Germain imesema kuwa Neymar Jr hakuhudhuria kikao cha kwanza cha mazoezi kulingana na muda na eneo la mazoezi hayo.

"Hii ni kinyume na matarajio ya klabu, na klabu itachukua hatu kali dhidi ya Neymar," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Neymar alijiunga na PSG akitokea Barcelona kwa dau lililovunja rekodi la pauni milioni 200 mnamo Agosti mwaka 2017.

Ameifungia klabu hiyo mabao 34 katika mechi 37 na kuisaidia kushinda taji la Ligi Kuu mara mbili mfululizo, lakini pia amehusishwa na makosa kadhaa ya utovu wa nidhamu ikiwamo kupigwa marufuku kwa mechi tatu kwa kumsukuma shabiki baada ya PSG kufungwa kwenye fainali ya Kombe la Ufaransa.

Pia atakosa kushiriki mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kumtukana mwamuzi.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa klabu ya Santos ya nchini Brazil alivuliwa unahodha Mei kabla ya kupata jeraha la kifundo cha mguu wakati wa mechi ya kirafiki dhidi ya Qatar ambayo ilimfanya kukosa michuano ya Copa America ambayo taifa lake ndilo lililoibuka mshindi nyumbani.

Wiki iliyopita rais wa Barcelona, Josep Bartomeu, alidai kwamba Neymar anataka kuondoka PSG msimu huu.

Kwa mujibu wa ripoti katika vyombo vya habari vya Hispania, Neymar amekubali kupunguziwa mshahara wake kwa euro kwa milioni 12 kwa mwaka ili kusaidia katika kurudi katika klabu yake ya zamani ya Barcelona pale kwenye dimba la Nou Camp ambapo alicheza kati ya mwaka 2013 hadi 2017.

Miamba hao wa Katalunya tayari wamewasajili Frenkie de Jong kutoka Ajax kwa dau la pauni milioni 67 msimu huu na wanakaribia kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann kutoka Atletico Madrid.

## KWA UFUPI

**GRIEZMANN KUSHITAKIWA**

ATLETICO Madrid imefungua madai ya kinidhamu dhidi ya mshambuliaji wake Mfaransa Antoine Griezmann (28), ambaye anatarajia kujiunga na wapinzani wao katika La Liga, Barcelona kwa dau la pauni milioni 107.5. ***(Guardian)***

**MADRID KUMUUZA RODRIGUEZ**

MABOSI wa Real Madrid wanajiandaa kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez (27), kwa ajili ya kupata fedha za kuongezea kumnunua kiungo Mfaransa wa Manchester United, Paul Pogba (26), ambaye thamani yake ni pauni milioni 150. ***(Mail)***

**NAPOLI YAINGIA SOKONI**

KLABU ya Napoli imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Real Madrid, James Rodriguez (27), pamoja na mshambuliaji wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Argentina, Mauro Icardi, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Goal.com)***

**BAYERN YAMSUBIRI SANE**

BAYERN Munich imesema kuwa inamtarajia winga Mjerumani Leroy Sane, ambaye ana umri wa miaka 23, atafanya uamuzi wa kujiunga na klabu yao akitokea Manchester City hapo wiki ijayo. ***(Mail)***

**GERRARD: SIONDOKI RANGERS**

KOCHA wa Rangers, Steven Gerrard, ameibuka na kueleza kuwa taarifa zinazozagaa kuhusu yeye kujiunga na Newcastle United ni "taarifa za uongo". ***(Star)***

**OZIL ANUKIA UTURUKI**

KLABU inayoshiriki Ligi Kuu Uturuki ya Fenerbahce imesema kuwa iko tayari kufanya mchakato wa kumsajili kiungo wa Arsenal, Mjerumani Mesut Ozil, ambaye ana umri wa miaka 30. ***(Fanatik - in Turkish)***

**BAKAYOKO AGOMBEWA ULAYA**

ARSENAL, Manchester United na Paris St-Germain zote zimeonyesha nia ya kumwania kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Tiemoue Bakayoko (24), ambaye ni mali ya Chelsea. ***(RMC Sport - in French)***

**LUKAKU: NATUA INTER**

STRAIKA wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku (26), amesema anamatumaini atakuwa tayari mchezaji wa Inter Milan wakati timu hiyo itakapokutana na klabu hiyo ya Old Trafford katika mchezo wa kirafiki utakaochezwa Julai 20 mwaka huu. ***(Mirror)***

**NERES AGOMBEWA EPL**

WINGA wa Ajax, David Neres (22), anahusishwa na tetesi za kujiunga na Manchester United na Everton, lakini nyota huyo Mbrazil amesema kuwa hatima yake iko chini ya mabingwa hao wa Ligi Kuu Uholanzi. ***(Algemeen Dagblad, via Express)***

**ORIGI MAMBO SAFI**

KATIKA kuhakikisha kuwa straika wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Divock Origi anaendelea kubakia Liverpool., nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 ambaye amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake amepewa mkataba mwingine wa muda mrefu. ***(Star)***

**HEATON ATAKIWA VILLA**

MABOSI wa Aston Villa wamewasilisha ofa ya pauni milioni 7 kwa Burnley ili kumsajili golikipa wa Timu ya Taifa ya England, Tom Heaton (33). ***(Sun)***

**SALIBA KUTUA ARSENAL**

ARSENAL imekaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili beki wa Saint-Etienne, William Saliba. Thamani ya Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 18 imetajwa kuwa ni pauni milioni 25. ***(Evening Standard)***

**MALCOM ANUKIA EVERTON**

EVERTON inajiandaa kutoa kiasi cha pauni milioni 35 ili kumnasa mshambuliaji wa Barcelona, Malcom. Arsenal pia inatajwa kumwania Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(RMC Sport - in French)***

HABARI MICHEZO

# MWAKYEMBE AKUBALI KUTIMULIWA AMUNIKE

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amesema kuwa hawezi kubishana kuhusiana na uamuzi wa kuachana na Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) ambao umefanywa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Siku mbili kabla ya TFF haijatoa taarifa rasmi za kuachana na Amunike, Waziri huyo alifanya mazungumzo na kocha huyo na kueleza kuwa Serikali ina imani naye na itamsaidia kutekeleza programu za maendeleo ili kuinua kiwango cha soka hapa nchini.

Uamuzi wa TFF na Amunike kuvunja mkataba umekuja siku chache baada ya Taifa Stars kufungwa mechi zote tatu za hatua ya makundi katika Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon), ambazo bado zinaendelea nchini Misri.

Mwakyembe alisema kuwa wakati Amunike anatua nchini, aliahidi kuipeleka Taifa Stars kwenye fainali za Afcon, na kueleza kwamba ahadi hiyo ambayo ilikuwa ni ndoto za Watanzania, ilifanikiwa.

Waziri huyo alisema kuwa Amunike alifanikiwa kuuvunja " mwiko" wa kukaa miaka mingi bila kushiriki fainali hizo, ambazo kwa mara ya kwanza mwaka huu, zilishirikisha timu 24.

"Mimi sina tatizo na uamuzi wa TFF, naamini labda watatuletea kocha bora kuliko Amunike," alisema kwa kifupi Mwakyembe.

Aliongeza kabla ya uamuzi huo haujatangazwa, alipata nafasi ya kufanya mazungumzo na Mnigeria huyo ambaye alimweleza mipango na programu mbalimbali za maendeleo alizonazo kwa ajili ya maendeleo ya soka la hapa nchini.

Waziri huyo alisema pia anaungana na Watanzania wengine kuomboleza msiba wa wafanyakazi watano wa Kampuni ya Azam Media ambao ulitokea juzi katika eneo la Kizonzo, katikati ya Igunga mkoani Tabora na Shelui, Singida.

"Nasikitika tumepoteza vijana wadogo ambao bado wana damu changa, naungana na Azam Media katika kipindi hiki kigumu walichokuwa nacho sasa hivi," alisema Waziri huyo.

Aliwataka wananchi kuacha tabia ya kusambaza picha za ajali na kueleza kwamba serikali imejipanga kuwachukulia hatua watu hao.



Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, akisaini katika kitabu cha maombolezo ya kuwaaga wafanyakazi watano wa Kampuni ya Azam Media waliofariki juzi. **PICHA: MTANDAO.**

# TFF, Simba watoa pole Azam Media

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania ( TFF), limetuma salamu za rambirambi kwa uongozi wa Azam Media kwa kuondokewa na wafanyakazi wake watano.

Wafanyakazi waliofariki ni pamoja na Salim Mhando, Silvanus Kassongo, Said Haji, Charles Wandwi na Florance Ndibalema.

Akizungumza wakati wa kuaga marehemu hao jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema kuwa shirikisho hilo linaungana na Azam Media katika kipindi hiki kigumu na cha majonzi.

Kidao alisema amesikitishwa na taarifa za kuondokewa na wafanyakazi hao ambao walikuwa njiani kwenda kutekeleza majukumu yao.

"Nimesikitika kusikia mashujaa hawa wamefariki wakiwa kazini, sisi tupo pamoja na Azam Media mpaka mwisho," alisema Kidao.

Aliongeza kuwa ujio wa Azam TV umesaidia kuutangaza mpira wa Tanzania ikiwa pamoja na kuzidi kuinua vipaji vya wachezaji vijana wa hapa nchini.

"Ujio wa Azam TV umeleta mafanikio makubwa kwa kutusaidia kuonyesha michezo mbalimbali na kuhakikisha mpira wetu unakua," alisema Kidao.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema kuwa baada ya kupata taarifa hizo wameamua kuacha kutaja majina ya wachezaji wapya iliyowasajili.

"Jana (juzi), tulikuwa tutangaze majina ya wachezaji wote tuliowasajili lakini baada ya kupata taarifa hizi, tulisitisha mara moja," alisema Manara.

Aidha alisema Simba inaungana na Azam Media katika kipindi hiki kigumu walichonacho kwa kuondokewa na vijana wao.

"Azam Media imepoteza wafanyakazi mashujaa, tuendelee kuwaombea wenzetu kwenye safari yao ya milele," alisema Manara.

## Usajili Zanzibar kufanyika kisasa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesema kuwa halitaongeza muda wa usajili wa wachezaji kwa timu zinazoshiriki Ligi Kuu visiwani hapa, na kuzikumbusha timu zote kufuata kalenda iliyotolewa.

Dirisha la usajili la Ligi Kuu Zanzibar lilifunguliwa rasmi tangu June 25 na litafungwa ifikapo Julai 30 mwaka huu. Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Ali Mohammed Ameir, alisema kuwa shirikisho hilo linazitaka klabu kukamilisha mchakato wa kusajili na kuanza maandalizi ya msimu mpya mapema ili kuwa na vikosi imara.

Ameir alisema kuwa timu zote zinatakiwa kuheshimu kalenda hiyo iliyotolewa ili kuepuka usumbufu ambao umekuwa ukijitokeza mara baada ya dirisha la usajili kufungwa.

"ZFF haitakuwa na msamaha kwa timu yoyote ambayo itachelewa kukamilisha usajili kwa makusudi, na badala yake itajikita katika kanuni ya mashindano kama ilivyotoa mwongozo," alisema Ameir.

Kiongozi huyo alisema kuwa anaamini kila timu ikifuata vema kalenda ya ZFF na programu zake, msimu ujao utakuwa na ushindani na bingwa atakayepatikana atakwenda kuiwakilisha vema Zanzibar kwenye mashindano ya kimataifa.

## Uchaguzi Mkuu Mwenge J'mosi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

UCHAGUZI Mkuu wa Klabu ya Mwenge unatarajia kufanyika Jumamosi katika mji wa Wete ulioko kwenye Kisiwa cha Pemba, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa timu hiyo, Ali Seif, alisema kuwa maandalizi ya uchaguzi huo yamekamilika na anawaomba wanachama wote ambao wako hai kujitokeza kushiriki katika mkutano huo. Seif alizitaja nafasi ambazo zinawaniwa katika uchaguzi huo kuwa ni pamoja na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Katibu Msaidizi, Mweka Hazina pamoja na Mshauri Mkuu wa timu.

Alisema kuwa tayari mchakato wa kutoa fomu kwa ajili ya watu wanaotaka kugombea umeshaanza na anaamini wadau wenye sifa watajitokeza kwa lengo la kusaidia timu yao iweze kufanya vema katika msimu ujao wa Ligi Kuu Zanzibar.

"Lengo la kufanya uchaguzi ni kuwapa fursa ya wanachama kugombea nafasi za uongozi Ili kuipelekea mbele timu yetu ya Mwenge katika msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar, kama mnavyofahamu sasa ligi yetu inaushindani mkubwa," alisema.

Kiongozi huyo aliwataka mashabiki na wanachama wa Mwenge kuendelea kuunga mkono juhudi zinazofanywa na wachezaji pamoja na viongozi wao.

# Michezo

Jumatano Julai 10, 2019

Nipashe




Neymar aingia matatani PSG HABARI UK 30




Beki mpya wa Simba, Gadiel Michael (kulia) akisaini mkataba wa miaka miwili wa kuitumikia klabu hiyo. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Crescentius Magori. **PICHA: SIMBA SC**

# GADIEL YAMETIMIA SIMBA

●●● Mabingwa hao wasalimu amri kwa straika wake Mganda Emmanuel Okwi...

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE tetesi zilizokuwa zinaenea kuhusiana na mchakato wa usajili wa beki wa Yanga, Gadiel Michael kutua Simba zimemalizika baada ya uongozi wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kumtangaza rasmi nyota huyo kuwa ni mali yake.

Hata hivyo, Simba imeonekana kukubali kukosa saini ya mshambuliaji wake Mganda Emmanuel Okwi, ambaye alikuwa amemaliza mkataba na sasa amepokea ofa kutoka katika klabu zaidi ya tano, ikiwamo Kaizer Chiefs inayoshiriki Ligi Kuu Afrika Kusini.

Hii ni baada ya jina la Okwi kutokuwamo katika orodha ya wachezaji 27 ambao Simba imewawasilisha kwenye usajili wake katika Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwa ajili ya kushiriki kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa ambao mwisho wake ulikuwa jana.

Gadiel alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa kikosi cha kwanza cha Yanga, ambayo pia msimu ujao itamkosa nahodha wake, Ibrahim Ajibu na Beno Kakolanya, ambao pia wametua kwa Wekundu wa Msimbazi.

**Beki huyo wa zamani wa Azam FC, ametua Simba akiwa ni mchezaji huru, baada ya Yanga kushindwa kufikia mahitaji yake aliyowapa ili asaini mkataba mpya wa kubakia klabuni hapo.**

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema jana kuwa Gadiel, ambaye pia ni mlinzi wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), amesaini mkataba wa miaka miwili.

Magori alisema kuwa lengo la Simba kusajili wachezaji waliofanya vema katika msimu uliopita, ni kukiimarisha kikosi chake ili kiweze kufanya vizuri kwenye msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki.

"Kwa heshima, tunapenda kutangaza usajili muhimu wa eneo la ulinzi, Gadiel Michael, mchezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), amesaini mkataba wa miaka miwili wa kuichezea timu yetu ili kuiwezesha kuleta makombe na mafanikio zaidi," alisema kiongozi huyo.

Nyota wengine walioko katika kikosi cha Simba ni pamoja na Aishi Manula, Ally Salim, Paschal Wawa, Erasto Nyoni, Gerson Viera, Tairone Da Silva, Wilker Da Silver, Francis Kahata, Deo Kanda, Hassan Dilunga, Mzamiru Yassin, Said Ndemla, Meddie Kagere, Clatous Chama, John Bocco na Mohammed Hussein "Zimbwe Jr".

Wachezaji wengine ni Yusuph Mlipili, Paul Bukaba, Kennedy Juma, Jonas Mkude, Rashid Juma, Miraji Athumani, Shomari Kapombe na Shiboub El Sharaf.

Simba itaanza msimu mpya wa kuikaribisha Azam FC katika mchezo wa Ngao ya Jamii utakaochezwa Agosti 17 mwaka huu na itafungua pazia la Ligi Kuu Bara kwa kucheza dhidi ya JKT Tanzania ifikapo Agosti 23 mwaka huu.

# Yanga yatamba mambo ni moto

**Na Shufaa Lyimo**

IKIWA ndio iko katika siku ya nne ya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Yanga, umesema kuwa kikosi chao kinaendelea vema na mazoezi yake, ambayo yanafanyika huko mkoani Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema wachezaji wote wa timu hiyo walioko Morogoro ni wazima na wanaendelea na mazoezi huku wakitarajia kumpokea kocha wao mkuu, Mwinyi Zahera wiki ijayo.

Mwakalebela alisema kuwa uongozi unaamini kambi hiyo itawaimarisha wachezaji wao na kuwaonya wawe tayari kukabiliana na ushindani katika mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la FA.

**"Wachezaji wetu wote wanaendelea vizuri na mazoezi, wanafuata programu zinazotolewa na benchi letu la ufundi, wanafanya vema kwa sababu wanajua kuwa msimu ujao wa Ligi kuu Tanzania Bara, wanatakiwa kuchukua kikombe," alisema Mwakalebela.**

Kiongozi huyo aliwataka mashabiki wao kuendelea kuwapa ushirikiano kama walivyofanya katika msimu uliopita, huku akiwaambia ubingwa wa ligi utarejea Jangwani.

"Tunaomba mashabiki wetu wazidi kutupa ushirikiano katika kipindi hiki cha maandalizi ya kuelekea msimu ujao ambao utaanza hivi karibuni, wasiwe na wasiwasi, tumesajili kikosi imara, tutakuwa na mambo mengi


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002